# Nipashe

Jumatatu Septemba 30, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580036

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper





UKURASA 13



## Watakaopiga kura uchaguzi serikali za mitaa wajulikana

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

**WAZIRI AWAONYA WAVUVI HARAMU UCHAGUZI MITAA**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema serikali itamkamata na kumfikisha mahakamani kwa makosa ya uhujumu uchumi mgombea wa chama chochote cha siasa...

UKURASA WA 5

**MBUNGE AJITOSA UNUNUZI PAMBA BIL. 7/- JIMBONI**

WAKULIMA wa pamba katika Kata ya Mwamanga wilayani Magu mkoani Mwanza, wamemshukuru Mbunge wa Jimbo la Magu, Bonventra Kiswaga, kwa kununua pamba yao...

UKURASA WA 7

**WAHAMIAJI HARAMU WAMTISHA LUGOLA**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewataka wananchi wa mikoa ya mipakani nchini kutoa taarifa za wahamiaji haramu ili kudhibiti matukio ya ujambazi, utekaji katika maeneo hayo...

# Makonda azuia mawaziri Dar

**ASEMA** wasubiri kufanya ziara mkoani humo hadi Novemba ili... *Endelea ukurasa wa 2*



Ofisa wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Monica Wabukundi, akiwasikiliza vijana kwenye stendi ya mabasi ya Mjini Bukoba, wakati gari la matangazo la NEC lilipokuwa likitoa elimu ya mpigakura, kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapigakura. **PICHA: NEC**

## Afichua ugumu kuongoza Bunge

UKURASA 4

## Chadema yazindua mkakati kupata kura za wanawake

UKURASA 2

**MICHEZO** KAMUSOKO, LWANDAMINA WAELEZA WALIPOSHIKWA YANGA UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## Mil. 26.9 kupiga kura S/Mitaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATANZANIA milioni 26.9 wenye sifa za kupiga kura, wanakadiriwa kuandikishwa kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Katika idadi hiyo, wanaume wanakadiriwa kuwa 12,852,328, huku wanawake wakiwa 14,108,157.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao kazi cha Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wasimamizi wa uchaguzi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, aliwataka wasimamizi hao kutoa elimu ya kutosha ili wananchi hao wajiandikishe kupiga kura kwa kuwa uchaguzi uliopita wa mwaka 2014 watu wengi hawakujiandikisha.

"Serikali Kuu tumeshaanza mikakati mikubwa ya kutoa elimu kupitia vyombo mbalimbali vya habari, lakini kuna siku maalum mmetengewa suala la elimu, nyie wasimamizi wa uchaguzi lazima mjipange tunataka uchaguzi wa mwaka huu uvunje rekodi, maana wa mwaka 2014 inatuonyesha watu wengi hawakujiandikisha katika daftari la wapiga kura," alisema.

Aliwataka kuhakikisha mwaka huu watu wanajiandikisha kwa wingi na kila msimamizi wa uchaguzi atapimwa kwa jinsi alivyowezesha eneo lake watu kujiandikisha kwa kiwango kikubwa.

"Imani yangu kazi hii tutaenda kuifanya vizuri sana na kwa vile kule chini tuna wasaidizi wetu, twende tukaifanye kazi hii kwa uzuri zaidi, lakini kazi hii tuna vitu vya kutuongoza tuna elimu ya mpiga kura, kitabu maalum, lakini tuna mwongozo na kanuni katumieni fursa hiyo muhimu ya kuhakikisha mnaenda kutoa elimu katika maeneo mahsusi," alisisitiza.

Alihimiza watu waelimishwe ili wafahamu na kutimiza haki yao ya kupiga kura na kuweka mazingira wezeshi ya uchaguzi kufanyika vizuri.

"Hatutarajii kuona siku ya uchaguzi hakuna karatasi ya kupigia kura watu wanaandika kwa karatasi ya mkono hatutarajii mwaka huu, tunataka kila eneo, kila halmashauri ajenda ya upigaji kura iwe imeandaliwa mapema," alisema.

Alisema ofisi yake itafuatilia kila kitu kinaenda vizuri na kama kushindwa washindwe wenyewe wasimamizi hao.

"Lakini huku sisi juu ambao tumepewa jicho pana kuangalia uchaguzi huu, naomba niwaambie tumejipanga vizuri sana kuhakikisha uchaguzi huu unaenda

INAENDELEA UK.8

# Makonda azuia mawaziri Dar

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewaomba mawaziri wanaotaka kufanya ziara za miradi katika mkoa huo, kusitisha kwa muda ili kupisha utekelezaji wa maagizo ya Rais John Magufuli aliyoyatoa.

Alisema mwezi huu na Oktoba watamalizia pia utekelezaji wa mikakati waliyopeana na kuanzia hapo mawaziri wataweza kufika na kuendelea na ziara zao za kikazi.

Makonda aliyasema hayo jana wakati akikagua mradi wa ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Vingunguti ambao ujenzi wake umefika asilimia 25.

"Nawaomba mawaziri ambao wanataka kufanya ziara katika mkoa huu, tutekeleze miradi ambayo tumepewa maelekezo na Rais Magufuli alipofanya ziara na baada ya hapo waendelee kama walivyopanga," Makonda alisema.

Kuhusu ujenzi wa machinjio hayo, alilipongeza Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kutekeleza mradi huo kwa haraka. Makonda alimwagiza Meya wa Manispaa ya Ilala, Omary Kumbilamoto, kukaa na Baraza la Madiwani kwa ajili ya kutenga fedha za kujenga barabara ya kuelekea katika machinjio hayo yenye urefu wa kilometa moja.

"Baraza la Madiwani likae litenge fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ya kuingia katika machinjio haya ya kisasa ili wafanyabiashara wanaokuja wasikwame kwa sababu ya ubovu wa barabara," Makonda alisema.

Alisema pia kuwapo kwa machinjio hayo ni fursa kwa manispaa kujenga reli ya kuingia eneo hilo ili mizigo isafirishwe kwa treni.

Aidha, aliwataka kuangalia namna ya kuwalipa fidia wakazi wa maeneo hayo ili kuandaa eneo kwa ajili ya kupanua machinjio hayo kwa miaka ijayo.

Makonda alisema ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu na kuukabidhi kwa ajili ya kuanza shughuli za kuchinja ng'ombe.

Naye Mhandisi Elisante Ulomi, alisema wanamalizia kazi ya kushindilia kifusi kwa ajili ya kuanza kusuka nondo na kumwaga zege.

Alisema mwishoni mwa Novemba wataanza kupaua, wakati kazi za kufunga umeme na kumalizia kazi za ndani zikiendelea.


Naye Meya wa Ilala, Omary Kumbilamoto, alisema watatekeleza maagizo yote yaliyotolewa na Makonda na kwamba lengo ni kuhakikisha mradi huo unakamilika Desemba na unakuwa kivutio.

Mbali na mradi huo, Makonda alitembelea mradi wa ujenzi wa soko la Kisutu na kuagiza mradi huo kukamilika Mei mwakani.

Wiki iliyopita, Mkonda alikutana na viongozi wakuu na watendaji Mkoa wa Dar es Salaam na kuwaagiza kila mmoja kutekeleza majukumu yake ipasavyo, vinginevyo watawachukulia hatua watalaoshindwa kuwajubuka katika utekelezaji wa majukumu yao.

Kikubwa aliahidi kuanza kufuatilia utekelezaji wa muradi ya maendeleo ili ikamilike kwa wakati.

Hatua hiyo ilitokana na Rais John Magufulo kuonekana kutofurahishwa na kusuasua kwa utekelezaji wa miradi mingi mkoani humo.



Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Shinyanga, Joseph Mwikoni, akitoa elimu ya namna ya kutumia mtungi wa kuzimia moto 'Fire Extinguisher' kwenye kongamano la watoto wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Makedonia Shinyanga Mjini. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Chadema yazindua mkakati kupata kura za wanawake

**Na Enock Charles**

ZIKIWA zimebaki siku 54 kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa serikali za mitaa, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), kimezindua mkakati wa kuwashirikisha wanawake katika uchaguzi huo.

Chama hicho kimeeleza kuwa kimeamua kuja na mkakati huo kwa kuwa kinaamini wanawake ni waaminifu katika masuala ya uchaguzi kuliko wanaume.

Uchaguzi wa serikali za mitaa umepangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu katika halmashauri zote 185.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mkakati huo uliopewa jina la Bavicha Queen Mzigoni jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chadema, Patrick Ole Sosopi, alisema chama kinawaamini wanawake ndiyo maana kimeona kuna haja ya kuwa na mkakati huo ili kuwashirikisha.

"Programu hii ya kuwashirikisha wanawake katika uchaguzi ambayo tunaizindua leo (jana) hapa makao makuu, tutaipeleka nchi nzima kwa kuzingatia kuwa mchango wa wanawake katika siasa ni mkubwa na wa kuaminika," Sosopi alisema.

Aliongeza kuwa mkakati huo umelenga kuwakutanisha vijana wa kike nchi nzima na unatarajiwa kuzinduliwa katika mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar ili kuwezesha chama hicho kuibuka na ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.

Akizungumza katika uzinduzi huo, Mbunge wa Ubungo, Saed Kubenea (Chadema), alisema chama hicho kinawategemea vijana kupata ushindi katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu na uchaguzi mkuu mwakani.

"Chama kinawategemea vijana na mimi nina imani sana na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti ingawa unaelekea kumaliza muda wako, mimi bado nina imani na wewe," Kubenea alisema.

TANGAZO


ULIPO
TUPO
Thamini kesho
yako na yake
SimBanking
*150*03#
www.crdbbank.co.tz
CRDB
BANK
Tunakusikiliza

# Afichua ugumu kuongoza Bunge

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

## ■Ni kiongozi pekee wa chombo hicho ambaye hajawahi kumfukuza mbunge bungeni miaka minne ya Bunge la 11

MWENYEKITI wa Bunge, Najma Murtaza Giga, ameeleza namna ilivyo vigumu kuongoza vikao vya chombo hicho cha kutunga sheria.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dodoma hivi karibuni katika Mkutano wa 16 wa Bunge la 11, Giga alisema bila kuwa na uvumilivu, kiongozi wa Bunge anaweza kuugua ugonjwa wa moyo.

Alisema ugumu huo unatokana na Bunge kuwa na wabunge wanaotofautiana kielimu, kiumri na hulka, akibainisha kuwa pande zote mbili (CCM na upinzani) zina wabunge wenye lugha za staha na lugha mbaya.

Hata hivyo, Nagma ndiye kiongozi pekee wa Bunge la 11 ambaye hajawahi kumtoa mbunge ukumbini katika miaka minne ya hilo. Viongozi wenzake (Spika Job Ndugai, Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson na Wenyeviti, Andrew Chenge na Mussa Zungu) wamewahi kuwatoa wabunge kadhaa wa upinzani kutokana na kutokuheshimu Kiti cha Spika.

Katika mahojiano hayo, Giga alisema hataisahau siku ambayo kulikuwa na mvutano mkubwa wa wabunge wa CCM na upinzani uliomlazimu Spika Ndugai kuingia ukumbini ghafla kuutuliza.

Siku hiyo, wabunge wa upinzani waliamua kupiga kelele bungeni wakipinga kitendo cha mmoja wa wabunge wa CCM aliyesikika akimtusi mbunge wa upinzani kwa kumwita 'mbwa'.

Giga pia alieleza namna alivyolazimika kusitisha masomo yake kwa miaka takribani 10 kutokana na matatizo ya kifamilia na kuingia katika maisha ya ndoa.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mfanyakazi huyo wa zamani wa Tevisheni ya Zanzibar (TVZ):-

**SWALI:** Ni changamoto ipi kubwa iliyowahi kukukabili maishani mwako?

**GIGA:** Nilipitia changamoto mbalimbali, sikuweza kuendelea na masomo ya chuo kikuu baada ya kumaliza kidato cha sita kutokana na matatizo ya kifamilia na kutakiwa kuingia katika maisha ya ndoa.

Jambo hili kwa kweli lilinirudisha nyuma lakini sikukata tamaa, nilijitahidi sana kuomba ruhusa, ndani ya miaka 10 nilipewa ruhusa nikaendelea na masomo yangu ya elimu ya juu na baadaye niliweza kumshawishi mwenzangu, kwa ruhusa yake nikaendelea na majukumu mengine ya kitaifa.

**SWALI:** Katika uongozi wako bungeni, kipi unakiona ni tatizo?

**GIGA**: Katika kuliongoza Bunge kuna changamoto zake. Nafasi ile ni ya lawama, huwezi kufanya kitu ukawaridhisha wote.

Kwa hiyo, unatakiwa kuweka mambo sawa. Ile ni nafasi ya kitaifa ambayo haijali chama chochote, unatakiwa uwe makini kuhakikisha kwamba kanuni na taratibu zote zinafuatwa.

Changamoto kubwa inakuja kutokana na Bunge kuwa na maoni tofauti, lina watu wenye elimu tofauti, wanatoka maeneo tofauti, hulka na tabia zao pia zinatofautiana.

Kwa hiyo, si rahisi kuwaridhisha watu wote kwa namna ambayo unaona wewe. Hiyo ni changamoto kubwa sana. Kila mtu ana uelewa wake na kila mtu anaona anachofanya yeye ni sahihi.

Ukiwa kwenye kiti kile ni lazima uwe mvumilivu na subira ya hali ya juu kuhakikisha kwamba hutawaliwi na hisia na hukasiriki.

Inabidi usikilize kwa umakini kila mtu na panapotokea tatizo, wakati huohuo na muda mfupi sana unatakiwa ufikirie la kufanya ili kuweka mazingira sawa.

**SWALI:** Ni kikao kipi cha Bunge ulikiongoza na pengine hutakisahau katika maisha yako?

**GIGA:** Siku zenye matatizo ni nyingi, inatokea migogoro ya ghafla na wakati mwingine huwezi kufikiria kwa sababu pale sekunde moja inaweza kuharibu mambo yote.

Mara nyingi hutokea pale anapozungumza mtu jambo ambalo wewe hukulisikia, lakini wabunge wengine wameshasikia na unashindwa kufanya uamuzi wa haraka na huyo ameshasema neno baya na wameshalipokea kuwa ni tusi.

Sasa pale kelele zinakuwa zimezidi na mimi sikusikia huyo mtu alisema nini. Kila mtu anazungumza, pale unakosa 'balance' ya kuweza kuamua haraka ufanye nini. Hilo jambo hutokea lakini baadaye hukaa sawa ni changamoto ya kawaida bungeni.

Pale kwa kweli lazima uwe mvumilivu kwa sababu kitendo cha kuwa pale mezani, uwe ni Spika au msaidizi wa Spika, lazima uvumilie tu. Kama utakuwa na hasira na ukataka kuchukua hatua kwa kila linalotokea bungeni, ni lazima utaugua ugonjwa wa moyo au presha.

Kuna siku ambayo ilikuwa mbaya kwangu ni ile ambayo Spika alitokea kunusuru mvutano, ni ile siku mbunge mmoja wa CCM baadaye nilikuja kugundua alikuwa ametamka kwamba "kama kuna mbwa bungeni atoke".

Kelele zilikuja nyingi sana bungeni kiasi kwamba sikuweza kushika vizuri kilichotamkwa na huyo mbunge na kuwakera wenzake.

Kwa kweli hata mimi baada ya kugundua alitamka maneno hayo, sikupenda kwa sababu kwanza nilikuwa kwenye mfungo wa mwezi mtukufu na nisingependa atoe kauli hiyo.

**SWALI:** Ni wabunge wepi katika Bunge hili la 11 wamekupa shida katika uendeshaji wa shughuli za Bunge?

Ni vizuri kuwataja kwa majina lakini kuna wabunge kutoka pande zote wanaozungumza vizuri na wanatumia lugha ya staha. Mfano, upinzani kuna Dk. (Semesi) Sware, anazungumza vizuri kwa lugha ya staha.

Lakini pia pande zote mbili zina wabunge ambao lugha zao ni hatari tu, huwezi kukwepa watu kama hao ndio maana nikasema mle ndani kuna watu wenye maoni na hulka tofauti.

**SWALI:** Upo bungeni kupitia Viti Maalum. Je, utawania jimbo mwaka 2020?

**GIGA:** Ni kweli nina ndoto hiyo, lakini kwa kuwa hii ndio mara yangu ya kwanza nimekuja kupitia kundi langu la wazazi, sitawakatisha tamaa kwa mara hii, nitawaunga mkono tena ili twende nao sambamba walau kwa miaka 10 kisha baadaye ninaweza kufikiria kwenda jimboni.

**SWALI**: Tutarajie kumwona Giga anachukua fomu ya kuwania urais wa Zanzibar?

**GIGA:** ... (kicheko) Hapana! Nafikiri kazi ambazo nazifanya ndio zitaelekeza wapi napaswa kwenda, siyo mimi nataka kitu fulani. Mafanikio yangu ndio yataelekeza niende wapi.

**SWALI:** Unafikiri kuhama kwa Maalim Seif Sharrif CUF na kujiunga na ACT-Wazalendo kutakuwa na changamoto kubwa kwa CCM katika uchaguzi mkuu ujao hasa upande wa Zanzibar?

**GIGA:** Sisi CCM tuko 'very stable' (imara). Tumesimama imara kama kawaida yetu. Tutapambana kuhakikisha chama chetu kinashinda bila wasiwasi.

Na hata huku kuhama kwake (Maalim) na kuingia ACT, kwetu CCM ni faraja kwa sababu kuyumba kwao ndiyo mafanikio yetu ambao tuko imara.

**SWALI:** Kwa hali ilivyo kisiasa nchini, unatarajia kuona mbunge kutoka upinzani akirejea bungeni baada ya uchaguzi wa mwakani?

**GIGA:** Nafikiria itategemeana na uamuzi wa wananchi, kama kuna mbunge wa upinzani wanamtaka, atarudi. Ni mawazo yao.

Lakini kwa hali ilivyo, nguvu kubwa ya CCM na chama kinavyokwenda juu zaidi na wao wenyewe wanaweza kuvunjika moyo. Na wakivunjika moyo sisi ndio tunafurahi.

**SWALI:** Ulizipokeaje taarifa za kushambuliwa kwa Tundu Lissu?

**GIGA:** Kwa kweli, kama binadamu sikuzifurahia. Lingeweza kumtokea yeyote, hata mbunge wa CCM. Si jambo zuri na wala sikulipokea kwa kufurahia kwamba yule ni mpinzani wetu.

Huwezi kufurahia shambulio dhidi ya mtu yeyote duniani. Sisi sote ni kitu kimoja na tuko hapa bungeni kutekeleza majukumu ya kitaifa, haijalishi mtu ana mawazo gani, ana itikadi gani, kushambuliana, kupigana si jambo zuri.

**SWALI:** Lissu amepoteza ubunge na shambulio dhidi yake ndiyo kiini cha kukumbwa na changamoto hiyo. Unasemaje kuhusu hili?

**GIGA:** Kupoteza ubunge kwa Lissu nafikiri nisiseme sana kwa sababu ni mambo ya kikanuni yamevunjwa, kuna taratibu hazikufuatwa. Yeye kama mbunge alipaswa kutoa taarifa kuhusu aliko kwa Spika.

Kilichomtokea Lissu ni jambo la kawaida, na si yeye peke yake, wako wengi wamekumbwa na changamoto hiyo. Kuna wengine ndani ya Bunge hili hili la 11 wameondoka kwa kutozingatia kanuni.

Hata mimi nisipofuata utaratibu kwa kutohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Bunge, ninaweza kuvuliwa ubunge.

**KUHUSU GIGA**

Mwenyekiti huyo wa Bunge alizaliwa Septemba 5, 1967. Ni mtoto pekee wa Bwana na Bibi Abdallah Khamis. Jina la Giga ni la mumewe. Ni mama wa watoto watano (mmoja wa kiume).



Mwenyekiti wa Bunge, Najma Murtaza Giga

## HABARI KITAIFA



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Wilaya ya Iringa, Christopher Kajange (mwenye koti la bluu), akitapa maelezo toka kwa mmoja wa wajasiriamali alipotembelea shughuli za vikundi wakati wa mafunzo ya kibiashara kwa wanufaika wa mradi wa elimu unatekelezwa na Shirika la SOS jana. Kulia ni ofisa mradi wa shirika hilo, Lawi Barani. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Mbunge ajitosa ununuzi pamba bil. 7/- jimboni

**Na Anthony Gervas,** MAGU

WAKULIMA wa pamba katika Kata ya Mwamanga wilayani Magu mkoani Mwanza, wamemshukuru Mbunge wa Jimbo la Magu, Bonventra Kiswaga, kwa kununua pamba yao iliyokuwa imekosa wanunuzi yenye thamani ya Sh. bilioni saba.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Diwani wa kata hiyo, John Nzilanyingi, alisema wakulima hao wamemshukuru mbunge huyo kujitosa kuinunua pamba yao iliyokuwa imekosa wanunuzi tangu msimu wa mwaka huu uanze.

"Wakulima wamemshukuru mno Mbunge wa Jimbo la Magu, kujitosa kuwasaidia kuinunua pamba yao kwa bei elekezi ya serikali ya Sh. 1,200 kwa kilo, iliyokuwa imekosa wanunuzi tangu msimu wa pamba ulivyoanza," alisema Nzilanyingi.

Pia alisema mbunge huyo ameonyesha mfano mzuri wa kuigwa kuwakomboa wakulima wa kata hiyo, ambao walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya kilio hicho na hivyo kuamua kuwakwamua kiuchumi.

Alisema pamoja na kushuka bei ya zao hilo katika soko la dunia na kufikia Sh. 700, lakini mbunge huyo aliamua kujitosa kununua kwa bei elekezi bila kujali hasara ambayo anaweza kuipata ili kuwaondolea kero hiyo wakulima hao.

Alisema zao la pamba ni uti wa mgongo kwa wakulima wa Kanda ya Ziwa ambalo wanalitegemea kuwakwamua kiuchumi kama vile lilivyo zao la korosho kwa wakulima wa Nyanda za Juu Kusini.

# Waziri awaonya wavuvi haramu uchaguzi mitaa

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, amesema serikali itamkamata na kumfikisha mahakamani kwa makosa ya uhujumu uchumi mgombea wa chama chochote cha siasa atayetumia rasilimali za uvuvi kujipatia sifa za ziada za kuchaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa.

Amesema wagombea wote hawataruhusiwa kutumia rasilimali za nchi kujipa sifa ya kuchaguliwa na yeyote atakayewadanganya na kuwahadaa wananchi kwamba akichaguliwa, ataruhusu uvuvi haramu kwenye eneo lake, atashushwa jukwaani na kuburuzwa kortini.

Amesisitiza kuwa hakuna kipindi ambacho wavuvi haramu watasakwa, kukamatwa na kushtakiwa kama kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Akizungumza na wavuvi katika Mwalo wa Kagongo wilayani Mwanga kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu alikoshiriki kuteketeza nyavu haramu, Waziri Mpina alisema wananchi wengi wamejipanga kujihusisha na uvuvi haramu hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi kwa kisingizio kwamba serikali itaogopa kuwakamata kwa kuwa ni kipindi cha kuomba kura.

Waziri Mpina alisema wananchi watambue serikali iko macho na usimamizi wa sheria za nchi hauwezi kusimama kwa kisingizio cha kuwapo kwa uchaguzi.

Kutokana na kushamiri kwa uvuvi haramu, Waziri Mpina pia alitangaza kuundwa kwa kanda mpya za ulinzi wa rasilimali za uvuvi za Bwawa la Nyumba ya Mungu na Bwawa la Mtera na kumwagiza Katibu Mkuu (Uvuvi) kuhakikisha ifikapo Oktoba Mosi, mwaka huu, maofisa hao wawe wameshawasili kwenye kanda hizo. Mpina pia alisema serikali kuanzia sasa itakuwa inawakamata na kuwafungulia mashtaka ya uvuvi haramu watendaji wote wa vijiji na kata zitakazobainika kushamiri uvuvi haramu kwa kuwa, "haiwezekani vitendo viovu vya uvunjifu wa sheria vifanyike huku kukiwa na viongozi waliopewa dhamana na serikali kulinda rasilmali hizo".

Waziri huyo pia aliwaagiza Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri za Mwanga, Moshi na Simanjiro kukomesha uvuvi haramu kwenye Bwawa la Nyumba ya Mungu na wakishindwa kuudhibiti hadi kufikia Desemba mwaka huu, atazifungia halmashauri hizo kukusanya ushuru wowote na wananchi watafanya shughuli hizo bure.

Mpina pia alieleza kusikitishwa na Halmashauri ya Mwanga ambayo inakusanya mapato kutokana na shughuli za uvuvi, lakini imeshindwa kuwajengea hata choo wavuvi katika mwalo huo na kuagiza ifikapo Desemba 30, kuwe na choo katika eneo hilo vinginevyo atazuia ukusanyaji wa mapato na viongozi husika watawajibishwa kwa makosa ya kudharau kazi za wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, alimhakikishia Waziri Mpina kuwa atasimamia kikamilifu maelekezo yake kwa kuwa serikali ya awamu ya tano haina mzaha katika kupambana na wahalifu hasa wanaojishughulisha na uvuvi haramu.

# Mfumo wa kimtandao waanza kufuatilia utafiti majaribio dawa

**Na Devota Mwachang'a**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa nchini (NIMR) zimeanzisha mfumo wa kielektroniki ya ufuatiliaji wa utafiti wa majaribio ya dawa ili kurahisisha na kusaidia udhibiti wa majaribio na taasisi zinazosimamia maadili ya ufanyaji utafiti.

Lengo la kuanzishwa mifumo hiyo ni kuhakikisha usalama wa dawa kwa mtumiaji.

Hayo yalibainishwa katika mkutano wa pili wa mwaka wa mradi unaolenga kufuatilia na kuhakikisha usalama wa dawa kwa watumiaji (SMERT) uliofanyika TMDA Dar es Salaam, na kuhudhuriwa na wataalamu kutoka vyuo mbalimbali, hospitali na taasisi mbalimbali za utafiti nchini.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu TMDA, Akida Khea, alisema uanzishwaji wa mfumo wa kielektroniki ni sehemu ya mafanikio ya Mradi wa SMERT; kwa kuwa utafiti unapofanywa huhusisha dawa, hivyo madhara yatokanayo na dawa hizo, ni lazima yatolewe taarifa kujua chanzo cha tatizo.

"Awali taarifa zilijazwa kwenye makaratasi sasa kupitia mfumo huu matokeo ya utafiti yatawasilishwa kwa njia ya mtandaoni (Online Application) ambapo mtafiti anajaza taarifa zake na tafiti anayotaka kuifanya kuhusiana na dawa, pia mfumo huo umesaidia mtu yeyote duniani akisajili majaribio yake huonekana kote," alisema Khea, anayeshughulikia uthibiti wa bidhaa tiba.

Mkurugenzi wa NIMR Mbeya na Mtafiti Mkuu wa Mradi (Tanzania-Uingereza), Dk. Nyanda Elias, alisema: "Kabla ya mfumo wa kieletroniki kuanzishwa, kulikuwa na changamoto ya kutumia muda mrefu kabla ya mradi ama tafiti kuruhusiwa kwenda kufanya, hii iliathiri utekelezaji wa utafiti kwa ile miradi ya muda mrefu kutokana na kibali kuchelewa."

Dk. Nyanda alifafanua kuwa katika miaka miwili ya utekelezaji wa mradi huo, umewajengea uwezo na kuwafanyia mafunzo kwa wataalamu kwenye kamati za kikanda za maadili nchi nzima.

Mkurugenzi wa Kuratibu na Kukuza Utafiti NIMR, Dk. Paulo Kazyoba, alieleza kuwa utafiti wa afya lazima ufanyiwe tathmini ya maadili iwe ya majaribio ya dawa au kutafuta taarifa kwa wananchi.

Naye Mwakilishi wa Chuo Kikuu cha St. Andrews Uingereza, Dk. Wilber Sabiiti, alisema: "Tanzania ipo makini kwenye ufanyaji wa utafiti, iliona fursa ya kuendeleza uwezo wa utafiti wa maadili na uthibiti wa dawa, hivyo kuamua kutuma maombi ya ufadhili kwetu, tuliunga mkono juhudi zao na kuwapa ufadhili."

Sabiiti ambaye ni mtaalamu wa ugunduzi wa dawa mpya, alisema kunapogundulika ugonjwa mpya dawa za majaribio lazima ziangaliwe kwa usalama wa afya ya mtumiaji, na uangalizi wake unahitaji watafiti wenye maadili ambao wanaweza kuangalia na kulinda afya ya jamii.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

23 -09-2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumapili tarehe **29-09-2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Dar -Es-Salaam kuelekea Geita, gari hizo zenye namba za usajili:

**T660 BZU/T 310 DDH**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 20**
**Upana - mita 4.2**
**Kimo - mita 4 .6**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam hadi Geita Kupitia Dodoma,** gari zitasafiri muda wa mchana tu (**Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215437302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# TFF imtangaze kocha Stars kuokoa balaa hili

**KWA** muda sasa Kocha Mkuu wa Azam FC, Etienne Ndayiragije, amekuwa akikaimu nafasi ya kocha mkuu wa Taifa Stars, tangu Mnigeria Emmanuel Amunike alipotimuliwa mapema Julai mwaka huu. Katika majukumu hayo ya kuinoa Stars, Ndayiragije amekuwa akisaidiwa na Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Suleimani Matola pamoja na Kocha Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda.

Kwa ujumla kocha mkuu wa timu yoyote ya taifa ili aweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, hana budi kuwa huru katika kazi hiyo, huku akipata nafasi ya kutosha kuzunguka huku na kule katika mechi mbalimbali za Ligi Kuu husika ili kuweza kutazama viwango na uwezo wa wachezaji mbalimbali watakaounda kikosi chake.

Si katika Ligi Kuu husika tu, bali pia kwenye ligi mbalimbali zinazoendelea nchini na hata nje ya nchi ambako kuna wachezaji wazawa wanaocheza huko pindi anapotaka kujiridhisha zaidi na viwango vyao kabla ya kuwajumuisha kikosini.

Lakini kwa Ndayiragije na wasaidizi wake wote ni wazi wamekuwa wakibanwa na majukumu ya waajiri wao, klabuni, hivyo kukosa muda wa kutosha kuzunguka huku na kule kutazama uwezo wa wachezaji kabla ya kuwaita Taifa Stars.

Ndiyo sababu wachezaji wanaoitwa Taifa Stars, wengi ni waliowahi kupita mikononi mwa Matola, Ndayiragije na Mgunda au walioko katika klabu wanazozifundisha ama wale waliokuwamo timu ya taifa kwa muda mrefu. Mfano mzuri ni wakati huu ambao Ligi Kuu Bara ikiendelea tulitarajia kumuona Ndayiragije amegawana majukumu na wasaidizi wake Matola na Mgunda kwenda kushuhudia mechi mbalimbali za ligi hiyo ama hata kwenda kuona namna wachezaji wao walioko Yanga walivyocheza dhidi ya Zesco kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Lakini Ndayiragije alikuwa bize katika kuiongoza Azam dhidi ya Triangle FC nchini Zimbabwe kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, huku Matola na Mgunda wakipambana kuziongoza Polisi Tanzania na Coastal Union kwenye mechi zao za Ligi Kuu.

Kwa utaratibu huo, kuelekea mechi ijayo ya marudiano ya Taifa Stars dhidi ya Sudan kuwania kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), Ndayiragije atajuaje kama uwezo wa mchezaji wa Simba ama Yanga walioko Stars umepanda ama umeshuka? Ni wazi atawaita kwa mazoea tu, lakini pia atakosa nyota wapya wanaoonyesha uwezo dimbani kutoka klabu hizo na nyingine za Ligi Kuu.

Kwa ujumla kazi aliyoifanya Ndayiragije na wasaidizi wake kwa kufanikiwa kwanza kuitoa Kenya kwenye kinyang'anyiro hicho cha kufuzu CHAN kwa mikwaju ya penalti 4-1 kufuatia sare tasa nyumbani na ugenini na sasa wakikabiliwa na mchezo wa marudiano dhidi ya Sudan ugenini baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, ni kubwa.


Lakini ikumbukwe Ndayiragije na wasaidizi wake wameiwezesha Taifa Stars kufuzu kucheza hatua ya makundi kuwania tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 baada ya kuitoa Burundi. Hivyo, walipoifikia ni mafanikio makubwa na wanapaswa kupongezwa hasa kutokana na majukumu ya kuwatumikia mabwana wawili kwa wakati mmoja.

Sote tumeona namna Ndayiragije anavyolemewa na majukumu na kushindwa kuiongoza vema klabu yake, jambo ambalo ni wazi limechangia Azam FC kutolewa Kombe la Shirikisho Afrika, lakini kwa mfano huo huo tunaona namna Mtibwa Sugar ilivyoanza vibaya msimu huu wa Ligi Kuu, hali hiyo ni wazi imetokana na Kocha Mkuu, Zuberi Katwila kuwa na Kikosi cha timu ya Taifa cha U-20 kwenye michuano ya Cecafa U-20 nchini Uganda.

Nipashe tunaona ni wakati muafaka kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF) kuteua rasmi kocha mkuu wa Stars na Taifa U-20 na kama inaona Ndayiragije na wasaidizi wake pamoja na Katwila wanatosha, basi wakae meza moja na klabu zao ili kukubaliana na kuwaidhinisha rasmi kubeba majukumu hayo ya taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la Mauya kwa Ajibu, refa Mwandembwa anatosha?

Na Adam Fungamwango

**MOJA** ya mambo ambayo hayatosahaulika kwenye Ligi Kuu msimu uliopita ni kitendo cha mchezaji wa Mbao FC, Rafael Siame kuokoa maisha ya mchezaji wa Coastal Union Adeyum Salehe.

Kwenye mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa CCM Kirumba, Adeyum alianguka mwenyewe uwanjani dakika ya 44 na kung'ata ulimi hali iliyosababisha nusura apoteza maisha.

Siame, aliyekuwa karibu yake, pamoja na kwamba si mchezaji wa timu yake, alimkimbilia haraka na kuingiza kidole mdomoni ili kuurudisha ulimi kwenye hali ya kawaida na kufanikiwa.

Ni jambo ambalo halikuzungumzwa sana, wala Siame kupata tuzo kutoka kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), lakini kilikuwa ni kitendo cha uungwana sana na cha kibinadamu.

Moja kati ya matakwa ya Shirikisho la Soka duniani (FIFA) ni mchezaji kulinda usalama wa mchezaji mwenzake, iwe wa timu yake au timu pinzani na kitendo chochote cha kumsababishia kuhatarisha maisha yake, au kukatisha ndoto yake ya kucheza soka hakikubaliki.

Alhamisi iliyopita kwenye mechi ya Ligi Kuu kati ya Kagera Sugar dhidi ya Simba kulitokea tukio ambalo limekuwa gumzo kubwa sasa sehemu mbalimbali ikiwamo kwenye mitandao ya kijamii kama kawaida.

Ni cha mchezaji wa Kagera Sugar Zawadi Mauya, kumpiga mateke yapatayo manne kwa makusudi Ibrahim Ajibu.

Ukiangalia tukio hilo utagundua kuwa Mauya hakuwa anacheza rafu, ila alikuwa anampiga mchezaji mwenzake mateke kwa makusudi. Haikujulikana dhamira hasa ya mchezaji huyo.

Marudio yanaonyesha kuwa alimpiga kwanza mateke mawili. Baadaye akampiga la tatu ambalo badala ya Ajibu kuanguka lilimfanya yeye mwenyewe aliyepiga kupepesuka na kutaka kuanguka.

Aliposimama anaenda tena kumpiga teke lingine la nne, ambalo hili ukilitazama kwa jicho la tatu alikuwa na lengo la kumchota mtama kabisa, lakini alifanikiwa kuufyatua mguu mmoja wa Ajibu na mwingine ukabaki, hali iliyosababisha asiweze kuanguka chini.

Wakati Mauya akicheza rafu hizo, Ajibu ndiyo alikuwa na mpira. Na Mauya hakuonekana kabisa kuwa na nia na mpira. Alichotaka yeye ni kumpiga mwenzake mateke ya makusudi.

Rafu za aina ile nilikuwa nikiziona zamani kwenye miaka ya '80 na '90 kwenye mechi za uswahilini. Kwa miaka hii hata huko mchangani huwezi kuzikuta rafu za aina ile.

Cha ajabu na cha kusikitisha, wakati tukio lile likitokea, mwamuzi Emmanuel Mwandembwa alikuwa karibu na tukio. Lakini alichofanya ni kumpa Mauya kadi ya njano tu.

Sijui Mwandembwa alitaka kitu gani zaidi Mauya aongeze ili atoe kadi nyekundu. Kwa waliotazama karibuni wote, wanakiri kuwa ile haikuwa rafu bali ni uhuni uliopitiliza.

Baada ya mashabiki wengi wa soka kulizunguzia tukio hilo baya na lenye kutia najisi soka la Tanzania, huku wengi wakimsakama mchezaji huyo kwenye mitandao ya kijamii, akaamua kuomba radhi kwenye mtandao wake wa kijamii.

"Nachukua nafasi hii kukuomba radhi rafiki, na mchezaji mwenzangu Ibrahim Ajibu kwa mchezo usio kuwa wa kiungwana hapo jana, ni tukio ambalo hutokea ndani ya mchezo ikiwa umefungwa na damu ikiwa imechemka. Na pia niuombe radhi uongozi wangu wa Kagera Suger na Simba pamoja na mashabiki zangu kwa ujumla, asanteni sana."

Napenda kumpongeza mchezaji huyo kwa kutambua kuwa alichofanya ni kosa na wala haikuwa rafu ya kawaida ya mpira. Lakini anapaswa kuwa makini na tabia hiyo kwani itakuja kumharibia katika maisha yake ya soka huko mbele ya safari.

Hakuna timu ambayo inaweza kumsajili mchezaji asiye na nidhamu, kwani anaweza kuigharimu wakati wowote. Wachezaji wote ni ndugu moja kwani wanaweza kukutana siku nyingine kwenye klabu moja.

Mauya anatakiwa aige mfano wa Siame na si alivyofanya. Kuhusu Mwandembwa ni kwamba Kamati ya Waamuzi na ile ya Saa 72 inaweza kufanya kazi yake, lakini naye inapaswa ajiulize kama kweli anatosha kuendelea kuifanya kazi hiyo.

Waamuzi wana dhima ya kwanza kulinda afya ya wachezaji, hivyo wanapoona kuna mchezaji mechi imemshinda na anachotaka ni kuvunja wenzake miguu anatakiwa ampumzishe na si kumlealea.

Inaonekana sasa siyo Ligi Kuu, bali ni mechi za mchangani. Vinginevyo kuna mchezaji siku nyingine anaweza kumvunja mwenzake mguu kwa makusudi akitegemea huruma kutoka kwa refa kama ilivyokuwa kwa Mauya.

Waamuzi kutokuwa makini na kuachia mambo ya kihuni uwanjani, ndiko kunazalisha majeruhi wengi ambao wakati mwingine wanakuja kuigharimu timu ya taifa.

Wakati mchezaji fulani anatakiwa aiwakilishe nchi, anakuwa ni majeruhi ambayo yalisababishwa tu na aina ya mchezaji kama Mauya na refa kumvumilia bila kumwadhibu ipasavyo.

## HABARI KITAIFA




Mmoja wa madereva akihudumiwa wakati wa uzinduzi wa kampeni ya uelimishaji umma, faida za matumizi ya mafuta ya Total Excellium jana, katika kituo cha mafuta cha Total Port Access. Temeke, jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Lugola ataka mipaka ilindwe kudhibiti ujambazi

**Na Felix Mwagara,** KATAVI

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewataka wananchi wa mikoa ya mipakani nchini kutoa taarifa za wahamiaji haramu ili kudhibiti matukio ya ujambazi, utekajі katika maeneo hayo.

Lugola alisema uhalifu katika mikoa hiyo licha ya kuwa imedhibitiwa kwa kiasi kikubwa, lakini bado baadhi ya mikoa ukiwamo wa Katavi, wahalifu hutumia njia zisizo rasmi kuingia nchini na kufanya matukio ya uhalifu.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Ikola wilayani Tanganyika jana, Lugola aliwataka wananchi hao kutoa taarifa kwa vyombo vya dola, iwapo kuna mtu au watu wanawatilia shaka ili kudhibiti matukio mbalimbali ya uhalifu.

"Mnapaswa kuwa wazalendo kwa kutoa taarifa za wahamiaji haramu katika maeneo yenu ili kuisaidia serikali yenu kuwasambaratisha wahamiaji haramu ambao wanafanya uhalifu wakishirikiana na Watanzania wasiowaaminifu waishio mipakani, hii haiwezekani na kamwe serikali haiwezi kuchezewa," alisema Lugola.

Alisema Tanzania ina serikali makini katika kuwalinda watu wake, hivyo kwa majambazi ambao wanafanya matukio mbalimbali ya utekaji lazima washughulikiwe ipasavyo bila kuonewa huruma.

"Wahamiaji haramu wapo mitaani kwetu, na mnawajua, hivyo mnapaswa kutoa taarifa kwa maofisa Uhamiaji, Jeshi la Polisi au vyombo vingine vya dola nchini, ili serikali iweze kuwatia mbaroni haraka iwezekanavyo," alisema Lugola.

Ofisa Uhamiaji Mkoa wa Katavi, Kamishna Msaidizi, Vicent Haule, alikiri kuwapo na changamoto hiyo na kuahidi kuwasaka wahamiaji haramu kupitia vyanzo vyote vya uchunguzi.

Haule alisema maeneo ya mipakani yana changamoto licha ya kuwa ofisi yake inafanya kazi usiku na mchana kupambana na wahamiaji haramu, na wapo tayari kupokea taarifa za wahamiaji hao watakapopewa na wananchi.

"Tunamshukuru sana mheshimiwa waziri kwa kutupa maelekezo mbalimbali, hasa ya kuhusu masuala ya wahamiaji haramu, na uraia hasa pale makazi ya Katumba na Mishamo, kwasababu amewataka wakazi waliopewa uraia wasivunje sheria za nchi kwa kwenda Burundi na kurudi nchini bila kufuata sheria," alisema Haule.

Pia Lugola aliwataka polisi kuwasaka na kuwakamata majambazi na kuwasambaratisha bila woga na kusema kuwa mhalifu hawezi kuchekewa.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Tanganyika, Lilian Matinga, alimshukuru Waziri Lugola kwa kufika katika wilaya hiyo na kuahidi maagizo yote aliyoyatoa kwa wilaya hiyo watayafanyia kazi kupitia vikao vyao vya kamati ya ulinzi na usalama.

# NMB sasa yahamasisha kadi kwa watalii, wateja

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

UONGOZI wa Benki ya NMB umesema kuwa inazidi kuboresha mifumo ya huduma zao za kadi ili kuhamasisha watalii pamoja wananchi wakawaida kutumia kadi kwenye malipo na ununuzi.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Idara ya Huduma za Kadi wa Benki ya NMB, Philbert Casmir, wakati akizungumza kwenye maonyesho ya utalii visiwani Zanzibar, ambapo benki hiyo imetoa mchango mkubwa katika kudhamini.

Alisema kutokana na ukuaji na maendeleo ya teknolojia duniani, ndivyo wanavyo buni mbinu ambazo wataweza kwenda sambamba ili kuwafanya wateja wao kupata huduma bora na za kimataifa.

Alisema mifumo ya kidigitali na matumizi ya kadi za MasterCard ambazo zinatumika kitaifa na kimataifa zimekuwa zikiondoa usumbufu kwani huduma hizo zinaweza kutumika ndani na nje ya nchi.

Alisema benki hiyo hivi sasa ipo karibu na wananchi mjini na vijiji hivyo kuingia katika masuala ya utalii, kwa kiasi kikubwa itasaidia kuzidi kujitangaza na kuvutia wateja wengi zaidi pamoja na wageni wanaofika nchini.

Naye Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameomba ushirikiano na taasisi nyingine katika kutangaza utalii wa Zanzibar ili kuongeza idadi kubwa ya watalii.

Alisema wananchi wa Zanzibar wananufaika na utalii kupitia Sera ya Utalii kwa wote na kubainisha kuwa sera hiyo ipo wazi kuweza kunufanisha wananchi hasa kwa kuwa na usalama wa nchi.

Kwa upande wake Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahamoud Thabiti Kombo, alisema kuwa maonyesho hayo ni agizo la Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, ambapo lengo ni kuitangaza Zanzibar kiutalii baada ya mafanikio makubwa ya mwaka jana.

Alisema kuwa maonyesho ya kila mwaka yanawasaidia wajasiriamali wadogo wadogo kujitangaza kupitia utalii ili waweze kunufaika na matunda ya utalii kwa kuuza bidhaa na kukuza biashara zao.

Meneja wa tawi la Zanzibar, Abdalla Duchi, amewataka wananchi wa Zanzibar kuchangamkia fursa za utalii zinazopatikana nchini ili kujikwamua na umaskini.

Aliwataka wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati kutumia fursa zinazotolewa na benki hiyo katika maeneo mbalimbali kwa kujisajili kuwa mawakala, ambapo itafungua fursa za ajira sambamba na kutoa huduma kwa wananchi wa kawaida ikiwamo watalii wanaokuja kutembea Zanzibar.

Aliongeza kuwa Benki ya NMB ina wateja zaidi ya milioni tatu, huku ikiongoza kwa matawi mengi Zanzibar yakiwamo matatu, mawili Darajani na Mwanakwerekwe na moja Chakechake Pemba, huku ikiwa na jumla ya mawakala 84 Zanzibar, matawi 229 Tanzania nzima na mawakala 6,000 Tanzania nzima mjini na vijijini.

## Total yanoa madereva

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mafuta ya Total Tanzania, imewahimiza madereva kote nchini kutumia mafuta ya Total Excellium ili kubaini tofauti na mafuta mengine yote yasiyo na excellium, ili wakiishagundua tofauti, ndipo wafanye uamuzi ni mafuta gani ya kutumia kwenye magari yao, au vyombo vya moto.

Wito huo, ulitolewa na Mkurugenzi wa Mtandao wa Total, Marieme Sow, katika kampeni ya uelimishaji umma, faida za matumizi ya mafuta ya Total Excellium.

Marieme Sow alisema mafuta ya vituo vya Total, yameongezwa kiambata cha excellium kilichotengenezwa mahsusi na watafiti wa kampuni hiyo ambacho husafisha injini za gari kwa kadri inavyotembea.

Mariane Saw alisema, ili madereva waweze kuona faida na utofauti kati ya kutumia mafuta ya Total Excellium na mafuta mengine, inawabidi kutumia mafuta ya excellium mfululizo bila kuchanganya changanya mafuta.

Alitoa wito kwa madereva kufanya utafiti huo kwa kutumia mafuta ya mfululizo na kupima utofauti wa matumizi ya mafuta na wepesi wa magari yao.

Marieme aliongeza kuwa madereva wa umbali mrefu hususan madereva wa mabasi na malori ambao hutumia mafuta ya Total Excellium wamekuwa wakishuhudia jinsi injini zao zinarekodi utendaji bora zaidi, hutumia mafuta kidogo na ni safi zaidi kwa sababu ya Total Excellium.

Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa Total Tanzania, Marsha Msuya Kilewo, alisema japo uagizaji wa mafuta nchini hufanywa kupitia mfumo wa ununuzi wa pamoja hivyo mafuta yote yanayoingizwa Tanzania yanakuwa na ubora ulio sawa.

Kileo, aliongeza kuwa licha ya uwekezaji mkubwa uliofanywa na Total kutengenezwa viambata vinavyounda mafuta ya Total Excellium, lakini mafuta hayo bado yanauzwa kwa bei zile zile elekezi ambazo ziko sawa na mafuta mengine.

Total kwa sasa ina vituo vya huduma zaidi ya 100 nchini vikiwamo vya Gapco, vinavyomilikiwa na Total na vinatumia mafuta ya Total Excellium.



Wasamaria wema wakimsaidia dereva wa pikipiki aliyedondoka na magunia ya mkaa na kumshinda nguvu na kusababisha kushindwa kuimudu katikati ya barabara eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Majaliwa aelekeza utunzaji wa wazee

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewataka vijana na jamii kwa ujumla wasikwepe jukumu la kuwatunza wazee kwa sababu nguvu zao za uzalishaji mali zimepungua kutokana na kazi waliyoifanya wakiwa vijana kwa ajili ya maendeleo na ustawi wa familia zao na Taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, Waziri Mkuu amesema serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kutokomeza mauaji ya wazee uliozinduliwa Januari, 2019 ili kutokomeza ukatili kwa wazee ifikapo 2023 na kuhakikisha wazee na watu wenye ulemavu wanatambuliwa na kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu.

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana wakati akizindua kambi ya utoaji wa huduma za afya kwa wazee na watu wenye ulemavu katika viwanja vya Kichanganimjini Iringa. Kambi hiyo imeandaliwa na Mbunge wa Viti Maalumu, Dk. Ritta Kabati katika kuadhimisha Siku ya Wazee Duniani.

Alisema wajibu wa kuwahudumia au kusaidia wazee na watu wenye ulemavu ni wa kila mmoja na wanapaswa watambue kwamba wazee hao wamelitumikia Taifa kwa muda mrefu tena kwa namna mbalimbali ikiwamo kuwaletea na kuhakikisha wanapata mafanikio hayo ambayo wanajivunia sasa.

"Kwa msingi huo, tunao wajibu wa kuwajali wazee wetu kwa hali na mali ikiwa ni sehemu ya matunda ya uwajibikaji wao kwetu na kwa Taifa kwa ujumla. Hivyo basi, tutumie vema kambi hii kuwasaidia wazee wetu na watu wenye ulemavu kwa kutambua afya zao na kuwapatia matibabu ya kiafya ili waendelee kuwa salama na wenye furaha nasi tuvune busara zao."

Kutokana na umuhimu wa kuwatunza wazee na kuwasaidia watu wenye ulemavu, Waziri Mkuu ametoa rai kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, wananchi na wadau mbalimbali kuendelea kuimarisha upatikanaji wa fursa, haki na ustawi wa wazee ikiwamo kuondokana kabisa na vitendo vya ukatili dhidi yao.

"Vituo vyote vya kutoa huduma za afya vya umma kutoa huduma bora na za haraka kwa wazee wetu wenye vitambulisho. Tengeni dirisha maalumu kwa ajili ya kuwahudumia ili wasikae kwenye foleni muda mrefu. Serikali itaendelea kuweka miundombinu na mazingira rafiki ili kuwawezesha kupata mahitaji yao."

Alisema serikali itaendelea kusimamia maelekezo yake kwa halmashauri zote nchini kuwatambua wazee wasiojiweza na kuwapatia vitambulisho vya matibabu bila malipo. "Namshukuru Mbunge wa Viti Maalum, Ritha Kabati, amebainisha mafanikio yanayoendelea kupatikana kutokana na utekelezaji wa agizo hilo.

Waziri Mkuu ameendelea kuziagiza halmashauri zote nchini kuhakikisha zoezi hilo linakuwa endelevu kwa kuwatambua na kuwapatia vitambulisho wazee wote nchini wasio na uwezo ili waweze kunufaika na huduma ya matibabu bila malipo pamoja na huduma zingine za kijamii.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Iringa, Tiniel Mmbaga, alisema kukamilika kwa jengo hilo kutawawezesha kutoa huduma bora kwa jamii na kwa wakati kwani awali maofisa watano walikuwa wakirundikana katika chumba kimoja hali iliyosababisha wateja kushindwa kueleza matatizo yao baada ya kukosekana kwa usiri.

Shughuli hiyo, ilihudhuriwa na Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga; Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais- Tamisemi, Josephat Kandege, Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu. Stela Ikupa na maofisa wengine wa serikali.






## Mil. 26.9 kupiga kura S/Mitaa

INATOKA UK. 2

vizuri niwatake kila mmoja katika eneo lake aende akafanye vizuri," alisema.

"Sitarajii majanga yoyote yatokee, mi natarajia neema, chaguzi hizi huwa zinaanza majanga wale wageni wawaulize wazoefu, ndio maana mwaka huu tumeandaa mazingira yote wezeshi kuepusha majanga kwa hiyo, mtu janga alitafute mwenyewe kwamba huyu ameshindwa mwenyewe, imani yangu kubwa tutaenda kufanya uchaguzi huu ukae vizuri."

Alisema uandikishaji unatakiwa kufanyika ndani ya siku 47 kabla ya siku ya uchaguzi.

"Sasa kama hujaanza kuandikisha katika maeneo yako jihesabu kwamba unaanza kufeli uandikishaji unatakiwa kufanyika Oktoba 8 -14, mwaka huu na utadumu kwa siku saba unapaswa kutafsiri kanuni ipasavyo," alisema.

Awali Katibu Mkuu Tamisemi, Mhandisi Joseph Nyamhanga, alisema ofisi hiyo imeandaa madaftari ya kuandikisha wapiga kura na tayari wameshasambaza maeneo husika.

Alisema inakadiriwa kuwa na vituo vya kupigia kura 110,000 na kusisitiza kuwapo na usimamizi mzuri katika vituo hivyo.

Mwaka 2014, katika uchaguzi huo Watanzania 11,491,661 kati ya 18,587,742 waliandikishwa kupiga kura.

## Waziri: NEMC haitakuwa kikwazo kwa wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu,** LINDI

NAIBU Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, amelipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambalo kwa namna linavyopambana kuweka mazingira rafiki ili kuendelea kuwavutia wawekezaji hapa nchini.

Akizungumza katika ziara yake mkoani Mtwara, Sima amesema licha ya changamoto zilizopo, ofisi yake imeendelea kufanyia kazi mabadiliko mbalimbali ya kanuni na sheria ili kwenda sambasamba na azma ya serikali ya ujenzi wa uchumi wa kati na viwanda pasipo kuathiri mazingira.

"Tunapozungumzia mazingira tunazungumzia juu ya uhai wetu, hivyo kama wizara yenye jukumu la kusimamia mazingira tunalazimika kusimamia ustawi wa jamii bila kuathiri uwekezaji," alisema Sima.

Alisema ofisi yake imechukua hatua kadhaa ikiwamo kurekebisha baadhi ya tozo hali ambayo imepunguza malalamiko mengi kutoka kwa wawekezaji.

"Huko nyuma tulikuwa tukitoza asilimia moja ya jumla ya mradi au biashara, lakini sasa tumegawanya miradi ambapo kila mradi utakuwa na tozo yake. Mfano huko nyuma wamiliki wa visima vya mafuta walikuwa wanatozwa mpaka Sh. milioni 10, lakini kwa marekebisho ya sasa watakuwa na tozo ya Sh. milioni 4," alisema Sima.

## HABARI KITAIFA



Watoto wa marehemu mzee Alipipi Mwakanga wakiweka shada la maua kwenye kaburi la baba yao, wakati wa mazishi ya mzazi wa mwandishi wa habari wa gazeti la Nipashe, Gwamaka Alipipi, yaliyofanyika Mbezi Magari Saba, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waziri Mkuu awabana Njombe mazao ya misitu

**Na Silvanus Kigomba,** IRINGA

WAZIRI Mkuu, Kasim Majaliwa, ameagiza kuanzishwa uchunguzi dhidi ya viongozi wa mkoa wa Njombe kwa kushindwa kukusanya ushuru wa mazao yanayozalishwa hasa kwenye mazao ya misitu.

Waziri Mkuu Majaliwa alitoa agizo hilo wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Halmashauri ya Mji wa Mafinga, baada ya kutembelea kiwanda cha kuchakata mazao ya misitu cha Qwihaya cha wilayani Mufindi

Majaliwa alikuwa akijibu malalamiko ya Mkurugenzi wa kiwanda hicho, Leonard Mahenda, aliyemweleza kuwa pamoja na kuzalisha nguzo zenye ubora, wamebakia na shehena hiyo baada ya wafanyabiashara wa mazao hayo kuhamia mkoani Njombe ili kukwepa tozo ya asilimia tano inayotozwa na halmashauri za mkoa wa Iringa.

Mahenda alisema kuwa tozo hiyo, imeondoa ushindani wa soko kwa mazao ya misitu yanayozalishwa mkoani Iringa kutokana na halmashauri katika mikoa mingine inayozalisha mazao ya misitu ikiwamo Njombe kutotoza tozo hiyo na hivyo mazao yake kuwa na bei ya chini zaidi.

"Ushuru wa halmashauri ni tozo iliyowekwa kwa mujibu wa sheria na niwapongeze halmashauri za mkoa wa Iringa kwa kukusanya tozo hii kwa ufanisi mkubwa na naagiza uchunguzi ufanyike kubaini kwanini viongozi wa mkoa wa Njombe wameacha kukusanya ushuru huu," alisema Majaliwa.

Majaliwa aliongeza kuwa ukusanyaji wa mapato ya serikali ni moja ya masuala yanayopewa kipaumbele na serikali na anashangaa kuona bado kuna viongozi wanazembea katika suala la ukusanyaji mapato.

"Hawa wasiokusanya mapato ya halmashauri kwenye maeneo yao ni wazi wanayo maslahi binafsi katika uzembe huu, hivyo ni lazima tuchunguze kujua wanauhusiano gani na wenye hizo kampuni ama tujue kama kampuni hizo ni zao wenyewe," aliongeza Majaliwa.

Mwishoni mwaka jana, mkoa wa Iringa ulibadili utaratibu wa kutoka Sh. 5,000 kwa gogo na kuanza kutoza asilimia tano kama inavyohitajika kwenye sheria hali iliyosababisha kupanda kwa makusanyo ya Halmashauri za Wilaya ya Mufindi na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ambazo ndiyo wazalishaji wakubwa wa miti mkoani Iringa.

# TGNP yataka viongozi wanawake kuandikwa

**Na Deogratias Mushi**

HABARI za wanawake ambao wameonyesha majukumu muhimu katika maeneo tofauti ya uongozi zinapaswa kuandikwa kwa vizazi vijavyo, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP Mtandao, Lilian Liundi amependekeza.

Akizungumza kwenye mazungumzo ya Jopo la Jedwali la Mzunguko katika makao makuu ya TGNP Mtandao jijini Dar es Salaam, Lilian alisema kuna wanawake katika historia ya Tanzania ambao wamefanya michango ya kupongezwa, lakini kwa bahati mbaya, hakuna chochote juu yao ambacho kimerekodiwa.

Aliwaalika washiriki kushiriki hadithi kuhusu viongozi wa wanawake, ili kuzishiriki na TGNP Mtandao ambayo hivi karibuni iligawana ubia na Women Fund Tanzania (WFT) na SOMA, ili kuhakikisha kuwa historia ya viongozi kama hii haififii.

Lilian alisisitiza kwamba wanawake wengine zamani walifanya juhudi katika mapambano ya Uhuru wa Tanzania, lakini historia imewasahau, kwa sababu tu walikuwa wanawake.

"Kulikuwa na harakati katika ardhi ya Pare, Mkoa wa Kilimanjaro unaojulikana kama 'Mbiru' ambapo wanawake walifanya mashetani dhidi ya wanaume zao wakilazimishwa kulipa ushuru mkuu. Utawala wa kisiasa wa wakati huo uliwasikiliza wanawake, na kutikisa mfumo huo wa ushuru," alisema.

Alitaja mfano mwingine huko Kondoa Irangi, ambapo wanawake walitembea kwenda kwenye mlima kusali juu ya msiba ambao wanawake walikuwa wanakabili, ambao ulipewa na 'miungu'.

Alisisitiza kwamba kuna haja ya kuweka kumbukumbu ya wanawake maarufu kama Bibi Titi Mohammed, Binti Matola na Tatu Bin Said ambao walimsaidia Mwalimu Nyerere kupigania ukoloni na baadaye nchi hiyo kupata Uhuru mwaka1961.

Tamasha la jinsia la mwaka huu limekusanya wanaharakati wa haki za wanawake kutoka asili mbalimbali, kutafakari juu ya maendeleo ya Transformative Feminist Movement (TFM), kusherehekea mafanikio yake, na kushiriki masomo, changamoto na mikakati sugu.

## TBS yaja na dawa ya ukaguzi wa sampuli

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

KUTOKANA na malalamiko ya mara kwa mara ya wafanyabiashara kuhusu ucheleweshwaji wa ukaguzi wa sampuli, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limeamua kuwekeza kwenye ujenzi wa maabara ya kisasa ambayo ikikamilika kwake kutarahisisha shughuli za upimaji na ukaguzi.

Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora toka TBS, Gervas Kaisi, alisema hayo wakati akizungumza na wanahabari, baada ya kukutana na wajasiriamali wakiwamo wasindikaji kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Kaisi alisema kukamilika kwa maabara hiyo itakayoanza kazi wakati wowote toka sasa, kutarahisisha upimaji na ukaguzi wa sampuli na hata kukitokea dosari yoyote itaweza kufanyiwa kazi kwa haraka.

Mtaalamu wa Lishe kutoka Umoja wa wanafunzi Wajasiriamali waliohitimu Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA-SUGECO), Jolenta Joseph, alisema kutokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili wasindikaji na kushindwa kushindana kwenye soko kitaifa na kimataifa, wameamua kuwakusanya wajasiriamali hao ili kupewa mbinu za kisasa za usindikaji.

Mtaalamu huyo alisema licha ya wajasiriamali wakiwamo wasindikaji kupewa elimu na wadau mbalimbali likiwamo TBS, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na kwa Morogoro SUGECO, bado wengi wao wamekuwa wakishindwa kuuza bidhaa zao badala yake zinazotoka nje kuuzika zaidi. Hata hivyo alisema sababu kubwa imekuwa ni kukosa elimu sahihi ya usindikaji kisasa na kukosa vifungashio bora.

Baadhi ya watumiaji wa huduma zikiwamo bidhaa zinazosindikwa, Anna Hoza, Emma Kalenga na Badra Mbwijo, waliwataka wasindikaji kuacha kufanya hujuma kwenye bidhaa wanazozalisha kwa nia ya kujipatia kipato kwa njia rahisi.

## Wakazi 600,000 kupata majisafi

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

ZAIDI ya watu wapatao 600,000 kwenye wilaya nne za Mkoa wa Tanga, watanufaika na mradi wa majisafi na salama unaotekelezwa na serikali katika miji 28 kupitia mkopo wa dola milioni 500 zilizotolewa na India kwa ajili ya mradi huo.

Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alieleza hayo baada ya kukagua chanzo cha maji kilichopo katika Kijiji cha Mandera Kata ya Mswaha wilayani hapa kinachotarajiwa kutumika kutega maji kabla ya kuyasambaza kwenye miji hiyo.

Aweso alisema kukamilika kwa mradi huo ambao tayari hatua za awali zimeshakamilika ikiwamo kupata fedha hizo kutoka India utawanufaisha zaidi ya wakazi 600,000 wa miji ya Pangani, Muheza, Korogwe na Handeni.

Katika ziara hiyo, Aweso aliongozana na wataalamu kutoka Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Tanga (TangaUwasa), Taasisi ya Wakala wa Usambazaji Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (Ruwasa) na wa mradi wa Handeni HTM alikagua pia kituo cha kutega maji cha Hale Wilaya ya Korogwe.

Akifafanua mchanganuo wa mradi huo, alieleza kuwa miji hiyo minne ni miongoni mwa miji 28 ambayo itakayonufaika na mradi huo utakaogharimu jumla ya dola milioni 500 zilizotolewa kama mkopo na India.

Naye Mkurugenzi wa Mradi wa Maji Handeni HTM, Yohana Mgaza, alieleza kuwa chanzo cha Mandela kinasafirisha maji hadi Segera wilayani Handeni kwenye tangi kabla ya kusambazwa katika miji husika na kwamba huduma hiyo itakuwa ya saa 24.

Mgaza alieleza kuwa sambamba na miji hiyo, kukamilika kwa mradi huo watu wengine watakaonufaikanao ni wakazi wa vijiji vilivyo jirani na chanzo hicho ambavyo ni Mswaha, Majengo, Mafureta, Mswaha Darajani na Mauruirutuba.

# Makubaliano wamiliki viwanda mabonde maji ulipaji wa ada

**Na Frank Monyo**

WIZARA ya Maji kupitia Bonde la Wami/Ruvu, wamekubaliana na wamiliki wa viwanda vyote vilivyopo katika ukanda wa mabonde ya maji tisa nchini kulipa ada ya matumizi ya maji kwa mabonde hayo, ili kuwezesha shughuli za kulinda na kuendeleza vyanzo vya maji.

Akizungumza baada ya makubaliano hayo yaliyofanyika jana jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na mwakilishi wa wenye viwanda, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema maji ni bidhaa muhimu katika uzalishaji bidhaa mbalimbali viwandani, hivyo rasilimali za maji zinapaswa kulindwa kwa faida ya nchi na vizazi vijavyo.

Alisema sheria ya kulipa ada ya matumizi ya maji kwa wenye viwanda vilivyopo maeneo ya mabonde ipo ingawa ilikuwa haitekelezwi kutokana na changamoto mbalimbali, kupitia kikao hicho wamekubaliana na kuweka mazingira mazuri ambapo viwanda hivyo vitakuwa vinatoa mchango wao.

Alisema wamefanya mazungumzo hayo na kukubaliana kushiriki katika kulinda na kutunza vyanzo vya maji kwa sababu kimsingi wenye viwanda ndio wadau wakubwa wa matumizi ya maji ukitoa watumiaji wa majumbani na kilimo.

"Tumekuwa na mazungumzo mazuri na wenzetu wenye viwanda kupitia mwakilishi wao, tumezungumza nao namna ambavyo watashiriki katika kulinda vyanzo vya maji kwa sababu katika muundo wetu wa usimamizi wa rasilimali za maji moja ya msingi mkubwa ni kushirikisha wadau kwa maana ya watumiaji wa maji," alisema na kuongeza:

"Tumekubaliana watachangia kwa kulipa ada ambazo zipo kisheria kwa mfano; viwanda ambavyo vipo ukanda wa Ziwa Victoria watalipa kupitia Bonde la Ziwa Victoria na kwa vile ambavyo vipo Dar es Salaam vitalipa Bonde la Wami/Ruvu," alisema.

Mwakilishi wa wamiliki wa wenye viwanda, Hussen Suphian, aliishukuru serikali kwa kuwapa nafasi ya kuwasilisha changamoto zao ambazo walikuwa wanazipitia katika ushirikishaji katika jambo hilo na kufikia maamuzi.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Uwekezaji, Angellah Kairuki (kushoto), akizungumza jambo na Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Salum Shamte (kulia), baada ya kuwasili kwenye Mkutano Mkuu wa 19 wa Mwaka (AGM) wa taasisi hiyo, uliofanyika jijini Dar es Salaam. (Katikati) ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Kairuki aitaka TPSF ishiriki kuboresha sheria biashara, uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, ameitaka Bodi ya Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) kushirikiana na ofisi yake kupitia na kufanya marekebisho ya Sera ya Uwekezaji ya mwaka 1996 na Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997.

Lengo la ushirikiano huo ni kuweka mazingira rafiki katika sekta nzima ya biashara na uwekezaji.

Akizungumza katika Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 19 wa taasisi hiyo mwishoni mwa wiki, Kairuki alisema kuna umuhimu mkubwa wa TPSF kushiriki katika zoezi hilo ili kutatua changamoto zinazohusu masuala ya uwekezaji wa ndani na nje ya nchi.

"Ni mategemeo yangu nyinyi kama sekta binafsi mnaofanya shughuli mbalimbali za kibiashara mkigusa nyanja mbalimbali za maisha mtakuwa wazalendo kwa kuwekeza katika nchi yenu, mabadiliko hayo yataweka utaratibu utakaotoa kipaumbele kwa wawekezaji wa ndani ili kuhakikisha rasilimali za nchi zinawanufaisha," alisema.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa ubia kati yake na sekta binafsi kwa kuipongeza pia taasisi kwa jukumu inalotekeleza kama taasisi mwamvuli wa sekta binafsi nchini pamoja na kuwa mwenyekiti wa kwanza wa sekta binafsi zote chini ya Baraza la Biashara la ukanda wa SADC kwa mwaka 2019/2020.

"Nitumie fursa hii kuipongeza tena taasisi kwa kuendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwa serikali. Ni muhimu sana mkatambua kuwa katika uchumi wa kisasa wa karne ya 21 uimara wa taasisi za sekta binafsi ni nguzo muhimu sana," alisema.

Aliitaka TPSF kutekeleza kwa vitendo kauli ya Rais John Magufuli ya kuitaka taasisi kupanua wigo wa muundo wake kwa kufungua matawi vijijini, wilayani na mikoani ilikuwa na ushirikishaji mkubwa.

Aidha, Waziri Kairuki alisema serikali imetambua maeneo kutoka sekta binafsi na kuyaweka kama maeneo ya kipaumbele. Maeneo hayo ni pamoja na uanzishwaji wa viwanda nchini, kuendeleza na kuimarisha miradi mikubwa ya kuendeleza miundombinu ya msingi na kutekeleza mabadiliko na maboresho ya sheria zinazolenga kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara na uwekezaji.

Mwenyekiti wa TPSF, Salum Shamte, alisema mkutano huo ulikuwa wenye mafanikio makubwa na kuishuru serikali mchango mkubwa ikiwamo kurudisha mrejesho juu ya mambo yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Rais Magufuli.

"Kama taasisi tunafarijika kuona serikali ikituunga mkono kwa kushiriki nasi hasa katika kujadili changamoto zinazotukumba Watanzania hasa katika sekta ya biashara na uwekezaji. Tumeshajadili na wanachama na tumeridhia kuanza mchakato wa kurekebisha muundo wa taasisi hii ili kutanua wigo kwa Watanzania waliopo mikoa mingine nje ya Dar es Salaam kujiunga na taasisi hii," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF, Godfrey Simbeye, aliishukuru wizara kwa uwekezaji kwa kuipa upendeleo taasisi yake kushiriki katika kurekebisha sera za uwekezaji katika biashara.

# Wazazi watakiwa kulipia watoto chakula shuleni

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAZAZI wa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru, wametakiwa kuwalipia watoto chakula cha mchana wanapokuwa shuleni ili kuwajengea uwezo wa kimasomo.

Hatua hiyo pia inasaidia kundokana na dhana potofu kuwa serikali inagharamia kila kitu na kutoa elimu bure.

Rai hiyo, ilitolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Wilson Mahera, wakati akifungu mafunzo ya siku tatu kwa kamati ya usalama wa mtoto (MTAKUWWA).

Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa na tabia ya kuwafanyia watoto ukatili kwa kuwanyima chakula wanapokuwa shuleni kwa madai kuwa elimu ni bure, jambo ambalo linakwamisha juhudi za serikali pamoja na kudhorotesha kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Aidha, alisema serikali kwa kushirikiana na mashirika na taasisi wamekuwa mstari wa mbele kutetea haki za watoto na kupambana na ukatili dhidi ya watoto. Alisema baadhi ya wazazi wamekuwa kikwazo kwenye harakati hizo, kwa kushindwa kwa makusudi kuwalipia chakula cha mchana wanafunzi wanapokuwa shuleni kwa kuwa na dhana potofu elimu ni bure, hivyo kila kitu hakilipiwi. Aliwasihi wazazi kuwaonea huruma watoto na kutambua mwongozo wa sera ya elimu bila malipo kwani imeweka wazi majukumu ya serikali na majukumu ya wazazi.

Alisema jukumu la wazazi ni kuwapatia chakula cha mchana watoto wanapokuwa shuleni, kumpatia vifaa vya shule na mahitaji yake ya msingi na jukumu la serikali ni kutoa elimu bila malipo yoyote.

Mkurugenzi wa Shirika la Kijiji cha Watoto wanaoishi katika mazingira magumu (SOS), Grace Nkya, alisema shirika hilo linajihusisha na kazi ya kupambana na ukatili dhidi ya watoto na kuwalea watoto wanaoishi katika mazingira magumu na hatarishi.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Arusha, Denis Mgiye, alisema lengo la kutoa mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati ya Mtakuwwa wilaya ili wapambane na ukatili wa watoto na kutafuta njia ya kukabiliana na changamoto hizo.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (katikati), akikagua nguzo zaidi ya elfu mbili zikiwa zimehifadhiwa katika kituo cha kupoza na kusambaza umeme cha Singida, wakati wa ziara yake ya kukagua ujenzi upanuzi wa kituo hicho, kinachojengewa uwezo wa kupoza na kusambaza umeme wa Kilovolti(kV) 400. **PICHA: ZUWENA MSUYA**

# Sababu mifugo ya Tanzania kuzuiwa Kenya

**Na Zanura Mollel,** NAMANGA

ZAIDI ya mifugo 1,208 ya wafanyabiashara nchini, imezuiwa nchini Kenya, katika soko la Birika kwa kile kilichodaiwa kuwa mifugo hiyo imezuiwa kinyume cha taratibu, kitendo kilichosababisha mwingiliano wa kibiashara kati ya pande hizo mbili.

Mifugo iliyozuiwa ni mbuzi na kondoo 1,190, na ng'ombe 18, mali za wafanyabiashara kutoka mikoa tofauti nchini.

Akizungumza na Nipashe mfanyabiashara Hamis Nyambi, kutoka Mkoa wa Singida, alisema mifugo hiyo, imezuiwa tangu Septemba 26, mwaka huu na raia wa Kenya, huku Jeshi la Polisi nchini humo likiwaamuru warejee nchini Tanzania na kuiacha mifugo sokoni hapo.

"Tumerudi tupo kwenye soko letu upande wa Tanzania, hatujui hatima ya mifugo yetu iliyozuiwa Kenya na tumefuata taratibu zote za kisheria," alisema na kuendelea: "Mbaya zaidi mifugo yetu inaendelea kuibiwa, tunapigwa na kunyanganywa fedha tunaomba serikali yetu itusaidie."

Alisema walifuata taratibu zote za kusafirisha mifugo kwenda nje ya nchi na walishalipa mapato katika Mamlaka ya Mapato Kenya ( KRA), lakini cha kushangaza walipoanza safari ya kwenda kufanya biashara nchini humo, walizuiwa na watu waliokuwa wamebeba silaha za jadi.

Alisema baada ya purukushani hizo, kutokea walisimama kwa ajili ya kufanya mazungumzo ya amani, lakini wakati wakitoa maelezo, raia hao walifungua milango ya magari na kuanza kushusha mifugo hiyo kwa nguvu na wakiingiza mifugo katika soko la Birika lililopo Wilaya ya Kajado.

"Nashangaa tuliomba Jeshi la Polisi lituongoze wakakubali, lakini tulipofika soko la Birika wakatugeuka wakaungana na wananchi wao, na kutuamuru tuondoke turudi nchi kwetu, huku wakitutolea maneno ya vitisho kuwa tukiendelea kusimama eneo hilo watatupeleka magereza," aliongeza Nyambi.

Maxmillian Kisiga, mfanyabiashara kutoka Mkoa wa Singida, alisema raia hao Wakenya walimwalazimisha washushe mifugo sokoni hapo, ili rai hao wapate ajira ya kupakia na kushusha mifugo kwenye magari hadi soko kuu la Kariobangi mjini Nairobi.

"Hawataki tuende na watu wetu wa kupakia wala kushusha na tulishalipa kodi KRA, lakini bado sokoni hapo walitaka tuwalipe Sh.125000, za Tanzania ikiwa ni ushuru wa soko na malipo ya wapakiaji," alisema Kisiga.

Aidha, alisema walipofika soko kuu la Kariobangi bado walilipishwa tena ushuru wa soko Sh. 2000 za Kenya, kitendo ambacho kimesababisha kuwapo kwa mlolongo wa malipo ya kodi.

Alisema usumbufu huo, hadi sasa umedumu kwa muda wa mwaka mmoja na kumekuwa na matukio ya kuibiwa kwa mifugo katika soko hilo.

"Tukitoka na mbuzi 300, hapa nchini hadi tufike sokoni la Kariobangi tunajikuta tuna mbuzi 270, wengine wanaibiwa na kufa, kutokana na hali ya kupakia na kuwashusha kila kituo, " aliongeza Kisiga.

Wameiomba serikali ya Tanzania kukutana na serikali ya Kenya kuzungumza ili kutatua changamoto hizo, na kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wa mifugo kufanyabiashara pamoja.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa mifugo wilayani Longido, Saruni Laizera, alisema soko la Birika Wilaya ya Kajado nchini Kenya, halipo kisheria na hata baadhi ya viongozi upande wa nchi hiyo walikiri kuwa soko hilo halipo kisheria.

# Bajeti mafunzo ya wataalamu mifugo

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAKURUGENZI wa Halmashauri nchini, wametakiwa kutenga bajeti kwa ajili ya kuwapeleka wataalamu wa mifugo kupata elimu ya uhimilishaji wa mbegu kwa njia ya mirija ili wafugaji hao waweze kufikiwa na huduma hiyo kwa haraka.

Agizo hilo lilitolewa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, wakati akifungua mafunzo ya wiki tatu kwa wataalamu wa mifugo kutoka mikoa mbalimbali nchini, waliokuwa wakipata mafunzo ya kutumia teknolojia ya uhimilishaji kwa njia ya mrija yanayofanyika katika kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC) Usa River wilayani Arumeru.


Alisema wakati huu ndio wa pekee kwa wakurugenzi kutumia fursa hiyo kuhakikisha wanapeleka wataalamu wao kwa wingi, kupata elimu kwa vitendo juu ya uhimilishaji kwa njia ya mrija ili waweze kuwasaidia wafugaji katika maeneo yao.

Alisema serikali imejitahidi kuhakikisha mbegu hizo zinafika kwenye halmashauri mbalimbali nchini, lakini changamoto iliyopo ni kutokuwapo kwa wataalamu wenye taaluma hiyo ya uhimilishaji mbegu kwa njia ya mrija ambayo inatakiwa kuwafikia wafugaji wote nchini.

"Naombeni sana mafunzo haya mnayopata hapa yakawe chachu ya mabadiliko katika kutoa elimu hii ya uhimilishaji kwa wafugaji naomba sana msiende kuwa madalali wa kuwauzia mbegu hizo kwa bei kubwa, badala yake mtumie bei iliyoelekezwa na serikali isiyozidi 5000, pia natoa onyo kwa wote wenye tabia kama hiyo kuacha mara moja," alisema Prof. Gabriel.

Mkurugenzi wa Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji (NAIC), Dk. Paulo Mollel, aliwataka wafugaji kuhama katika ufugaji wa kizamani na kufuga kisasa kwa kutumia teknolojia hiyo ya uhimilishaji kwa njia ya mrija ili waweze kupata maziwa mengi zaidi na ng'ombe walio bora.

Alisema mafunzo hayo, ni awamu ya pili kutolewa kwa wataalamu hao, na kuwa baada ya mafunzo hayo wanatarajia kupata wataalamu wazuri waliobobea katika teknolojia hiyo ya wataweza kuwa mabalozi wazuri kwa wataalamu wengine.



## Timu ya wataalamu kutafiti magugu maji Ziwa Jipe

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, amesema serikali imeunda timu ya wataalamu watakaofanya utafiti wa namna bora ya kukabiliana na tatizo la uvamizi wa magugu maji katika Ziwa Jipe.

Ziwa Jipe ambalo lipo kwa sehemu kubwa katika Wilaya ya Mwanga, limeendelea kuwa katika hali mbaya kutokana na sehemu kubwa kufunikwa na magugu maji na kusababisha viumbe hai wakiwamo samaki kukimbilia upande wa pili wa ziwa hilo uliopo nchi jirani ya Kenya.

Dk. Mghwira, alidokeza juzi kuhusu timu hiyo ya wataalamu kupewa jukumu la kuandika maandiko ya kutafuta fedha kwa wahisani ili kukabiliana na tatizo hilo, wakati wa kikao cha Halmashauri Kuu ya Mkoa wa Kilimanjaro ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisema serikali imechukua hatua, kwa kuwa ziwa hilo ni rasilimali muhimu na hivyo ni lazima kuwe na mpango wa muda mfupi na ule wa muda mrefu wa kulinusuru.

"Jamani serikali imejiandaa vyema kupambana na magugu maji yaliyovamia na kutishia uhai wa Ziwa Jipe, baada ya timu ya wataalamu watakaofanya utafiti wa namna bora ya kukabiliana na tatizo la uvamizi wa magugu maji," alisema.

Kwa mujibu wa Mghwira, magugu maji yatakayoondolewa katika ziwa hilo, yatatumika kutengeneza mbolea, kwa vile utafiti wa awali unaonyesha magugu maji yanafaa kutengeneza mbolea nzuri ya mboji.

Mwaka jana, Ofisi ya Makamu wa Rais, kupitia kwa waziri mwenye dhamna ya mazingira, ilisema Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (Nemc), imeazimia kutangaza kupita tangazo la serikali kuwa eneo hilo (Ziwa Jipe) ni eneo nyeti la kimazingira.

Azimio hilo la kutangaza kuwa eneo mahsusi, ama nyeti kimazingira, litasaidia katika kuandika maandiko mbalimbali ya miradi na kupata fedha kutoka kwa wadau na washirika wa maendeleo.

Pia litaliweka ziwa hilo chini ya uangalizi maalumu na kuweka masharti ya matumizi bora ya eneo hilo.

# Kampuni zaonywa kusuasua mradi wa maji

**Na Mwandishi Wetu,** MWANGA

NAIBU Katibu Mkuu mpya wa Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, amezionya kampuni za M.A Kharafi & Sons na Badr East Africa Enterprises kutokana na kusuasua kwa utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji utakaomaliza adha ya maji katika wilaya za Mwanga, Same na Korogwe.

Mradi huo utavihudumia vijiji 29 vya wilaya mbili za mkoa wa Kilimanjaro na moja ya mkoa wa Tanga.

Sanga alikwenda kukagua maendeleo ya utekelezaji wa mradi huo mwishoni mwa wiki katika Bwawa la Nyumba ya Mungu, ikiwa ni wiki moja tangu alipoteuliwa na kuapishwa na Rais John Magufuli kuwa Naibu Katibu Mkuu. "Sijaridhishwa na kasi yenu ya ujenzi wa mradi, kama kuna changamoto mnakutana nazo zilizo nje ya uwezo wenu mhakikishe mnawasiliana na wizara mapema iwezekanavyo ili tupate ufumbuzi. Serikali inachohitaji ni kuona matokeo na haipo tayari kumvumilia mkandarasi ambaye anachelewesha mradi bila ya kuwa na sababu za msingi," aling'aka naibu huyo.

"Wanachohitaji wananchi ni maji, serikali haitomvumilia mkandarasi ambaye atashindwa kwenda na kasi inayokubalika."

Baada ya kujionea shughuli zilizokuwa zikiendelea na kupokea taarifa ya mradi kutoka kwa makandarasi hao, Mhandisi Sanga alieleza kutoridhishwa na kasi ya utekelezwaji wake na alisisitiza kuhakikisha kuwa mradi unakamilika kwa wakati.

Aliwataka makandarasi kuwa wepesi kwenye kufanya mawasiliano na wizara kila wanapokutana na changamoto yoyote ambayo ipo nje ya uwezo wao ili ufumbuzi upatikane haraka bila kuchelewesha shughuli za ujenzi wa mradi.

Pia Sanga aliwakumbusha makandarasi hao kuhakikisha ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kwenye ujenzi wa mradi huo unafanyika nchini badala ya kuagiza kutoka nje ya nchi, hasa ikizingatiwa kwamba vingi vinapatikana.

Hata hivyo, makandarasi hao kwa nyakati tofauti wakati wanajitetea, walimwahidi Mhandisi Sanga kwamba wataongeza kasi ya utekelezaji wa mradi huo pamoja kwa kuzingatia maelekezo aliyoyatoa. Awali, akiwasilisha taarifa ya mradi huo, Mratibu wa Mradi huo kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Emma Magembe, alisema mradi umesanifiwa kuzalisha kiasi cha lita milioni 103.68 kwa siku.

Mahitaji ya sasa, kwa mujibu wa Mhandisi Magembe ni lita milioni 78.38 ambayo yanatokana na Bwawa la Nyumba ya Mungu na kwamba mradi huo unalenga kuwanufaisha wananchi wapatao 438,931.

Pia Mhandisi Magembe alisema mradi huo unatekelezwa kwa awamu mbili, ya kwanza unahusisha ujenzi wa miundombinu ya uzalishaji maji na usambazaji kwenye mji wa Same na Mwanga na awamu ya pili inahusisha usambazaji wa maji kwenye vijiji 29 vya Wilaya za Mwanga, Same na Korogwe.

Mradi wa maji wa Same/Mwanga ni miongoni mwa inayotekelezwa na serikali katika mikoa ya Kilimanjaro na Tanga.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga (wa tatu kutoka kulia), alipotembelea eneo la chanzo cha maji (Bwawa la Nyumba ya Mungu) cha mradi wa Same/ Mwanga akimsikiliza Mratibu wa Mradi kutoka Wizara ya Maji, Mhandisi Emma Magembe. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Serikali yavunja uongozi soko la kimataifa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

HATIMAYE serikali imeuvunja na kuuzika rasmi uongozi wa soko la mitumba la kimataifa lililopo katika Uwanja wa Kumbukumbu ya King George, maarufu kama Memorio katika Manispaa ya Moshi.

Taarifa zilizopatikana jana na baadaye kuthibitishwa na Ofisa Tarafa ya Moshi Magharibi, Senzia Lushino, zinaeleza kuwa serikali imefikia uamuzi huo, baada ya kujiridhisha viongozi wake wameshindwa kulisimamia na kulifanya likithiri kwa uchafu.

Alipoulizwa jana kuhusu taarifa hiyo Lushino alisema, "Ni kweli tumevunja uongozi wa soko hilo baada ya kupokea malalamiko, lakini ziko sababu za msingi, kwa mfano kushindwa kusimamia suala la usafi wa mazingira na kusababisha uchafu kukithiri. Inaelezwa kwamba Ofisa Tarafa huyo alichukua hatua hiyo, baada ya kusikiliza kero za wafanyabiashara wa soko hilo.

"Na jambo la pili ni tuhuma dhidi ya fedha zilizochangwa na wafanyabiashara kwa ajili ya kugharamia usafi wa soko hilo. Kimsingi tumeshamwondoa madarakani mwenyekiti wa soko hilo Godfrey Shayo," alisema.

Alisema pia, serikali inamwondoa madarakani mwenyekiti wa soko hilo kwa tuhuma ya kushindwa kuitisha vikao na kushirikisha viongozi wenzake.

Alieleza kuwa Rais Magufuli alitoa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga ili waweze kufanya biashara zao bila bughudha, lakini uongozi wa soko ulikuwa unawauzia hata maeneo ya kuweka vibanda.

"Hili soko la Meimoria lina wafanyabiashara zaidi ya 500 na wanakusanya zaidi ya shilingi milioni tano kila siku ya gulio, na gharama za matumizi ya kufanga usafi ni Sh. 800,000 kila mwezi. Cha kushangaza uongozi wa soko hauna akiba hata ya Sh. 100,"alieleza Lushino.

Alisema kuanzia sasa, wafanyabiashara hao watalipa Sh. 200, kila wiki kwa ajili ya kuchangia gharama za usafi katika soko hilo.

Hata hivyo, alipotafutwa kujibu madai hayo, mwenyekiti huyo (Shayo) alikana tuhuma zinazoelekezwa kwake, akidai hata yeye na viongozi wenzake walikuwa wanafanya kazi kwa kushirikiana.

Katika mkutano huo, wafanyabiashara wa soko hilo walimchagua William Mollel kuwa mwenyekiti wa muda atakayesimamia shughuli za uendeshaji wa soko hilo ikiwamo usafi wa mazingira.

NIPASHE JUMATATU SEPTEMBA 30, 2019

Nipashe

# Spotika




FATI ANAVYOTEMBELEA MWAMVULI WA MESSI UK.20




# MSHIKEMSHIKE...

Mshambuliaji wa Inter Milan, Alexis Sanchez, akipata upinzani kutoka kwa beki wa Sampdoria (nyuma), wakati akitaka kupasua ngome ya timu hiyo kwenye mechi ya Ligi Kuu Italia, Serie A iliyomalizika kwa Inter kushinda 3-1 juzi. **HABARI UK.30**

## ISIKUPITE

USHINDI wa Manchester City dhidi ya Everton juzi, umemfanya David Silva kuwapo katika kikosi hicho kikiibuka na ushindi mara 200 kwenye mechi 289 za Ligi Kuu England alizoichezea, hivyo kuwa mchezaji aliyewahi zaidi kufikisha idadi hiyo. Nguli wa Chelsea, John Terry, alifikisha mechi 200 za ushindi katika michezo 305, huku kipa wa klabu hiyo Petr Cech (akifikisha kutokana na mechi 310) na Ashley Cole (mechi 318) mwingine akiwa nguli wa Manchester United, Ryan Giggs (mechi 315) .



## SOKA



# TIERNEY ANAVYOWEZA KULETA TOFAUTI ARSENAL

**LONDON, England**

KWA msaada wa wachezaji wenzake wa zamani wa Kieran Tierney, Kris Commons na Adam Bate inaonyesha kwa nini usajili huo mpya unaweza kuisaidia Arsenal kuimarika.

Arsenal imekuwa na matatizo makubwa kwenye safu yake ya ulinzi na Tierney amesajiliwa hapo kwa ajili ya kujaribu kumaliza tatizo hilo.

Tierney alianza kuichezea kwa mara ya kwanza Arsenal Jumanne iliyopita kwenye mchezo wa Kombe la Ligi ['Carabao Cup'] dhidi ya Nottingham Forest ambapo walishinda mabao 5-0.

Tierney alitangaza kurudi kwenye mazoezi ya kikosi cha Arsenal kupitia kwa mchezaji mwenzake, Shkodran Mustafi, kuelekea kwenye mchezo huo. Ulikuwa wakati mzuri kwa mchezaji huyo raia wa Scotland kupona katika wakati muafaka.

Ronny Deila, kocha raia wa Norway ambaye ndiye aliyempa kwa mara ya kwanza nafasi ya kucheza soka la kulipwa Tierney, hivi karibuni alisema kwamba wachezaji wakubwa watamsaidia mchezaji huyo kijana kuweza kufikia mafanikio yake, kwani ana imani kubwa naye.

Scott Brown, ambaye alikuwa nahodha wa Tierney kule katika Klabu ya Celtic, akimzungumzia mchezaji mwenzake huyo wa zamani, anasema kiwango chake ndicho kinachozungumza zaidi.

Kris Commons alikuwa mchezaji mwenzake mwingine ambaye alishuhudia wakati wa siku zake za kwanza za kucheza soka katika kikosi cha wakubwa na ana kumbukumbu nzuri kuhusu Tierney pamoja na Deila na Brown.

Anasema hakuwa na shaka kabisa wakati aliposhuhudia Arsenal wakilipa pauni milioni 25 kumsajili Tierney wakati wa kipindi cha majira ya joto kilichopita.

Lakini ilikuwa hamasa na morali ya Tierney mwenyewe iliyozungumza zaidi tangu mwanzo wake wa kucheza soka la kulipwa.

"Labda alikuwa anapenda kucheza bure," anasema Commons akiiambia Sky Sports. "Alikuwa fiti kiakili. Umbo lake lilikuwa la kuvutia uwanjani.

"Alikuwa hajali kuwamo au kutokuwamo kwenye sehemu ya kikosi cha kwanza, yeye alipenda kucheza. Ukiangalia hisia zake unaziona wazi kabisa na inaonyesha ukimuona namna anavyocheza soka uwanjani.

"Alikuwa kama mtoto ambaye alipenda kuwa nje ya uwanja na kufanya kile alichokuwa anapenda kukifanya."

Katika umri wake wa miaka 22, Tierney ambaye ni beki wa kati, lakini kiasili ni mchezaji wa beki ya kushoto ana nafasi kubwa zaidi ya kufika mbali. Na anaweza kuwa fiti zaidi kucheza beki ya kushoto kuliko Sead Kolasinac na kwa uhakika kabisa hilo linaweza kumsaidia zaidi kocha, Unai Emery.

Ingawa anaweza asiwe sawa na Kolasinac kwa umbo, lakini yeye ni imara zaidi kwa nguvu.

"Anaimarika zaidi kwa sasa," anasema Commons. "Unaweza kuona namna misuli yake ilivyo, kwa uhakika kabisa atakuwa na nafasi na msaada mkubwa zaidi kwa kikosi cha Arsenal."

Tierney pia ana uwezo wa kusaidia mashambulizi kwa Arsenal kwa kupanda na kushuka haraka. Kama Emery ataamua kumtumia kwa pamoja na Hector Bellerin, Arsenal watakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kusukumiza mashambulizi mbele.

"Wakati nilikuwa ninacheza na Kieran mara zote yeye alikuwa anapenda kucheza kushoto na alikuwa na msaada mkubwa mno kwa kupandisha mashambulizi mbele," anasema Commons.


"Kuna wakati alikuwa anacheza kama winga, kwani alikuwa akisukumiza mashambulizi mbele na yeye alikuwa ana uwezo wa kupanda na kushambulia kama winga.

"Sina shaka naye kabisa, kwani naamini baada ya muda mfupi ataleta mabadiliko makubwa zaidi kwa kikosi cha Arsenal.

"Kwa kipindi nilichocheza naye, kwa uhakika kabisa nilikuwa namuona mmoja wa wachezaji ambao wana nafasi ya kuwa wakubwa zaidi duniani kwa siku chache zijazo."

Arsenal imekuwa na tatizo kubwa kwenye safu ya ulinzi na sasa Tierney anaonekana kama ndiye mwarobaini wa kulimaliza tatizo hilo na ni suala la muda tu tunaweza kushuhudia tofauti kubwa mno kwa timu hiyo.

### JE, WAJUA?



Kevin De Bruyne hadi sasa ametoa pasi za mwisho nane kwenye Ligi Kuu England msimu huu, ni Cesc Fabregas pekee katika msimu wa 2009-10 aliyetoa pasi nyingi zaidi katika kikosi chake kwenye mechi saba za kwanza katika msimu mmoja zaidi yake.

## MICHEZO



Kiungo wa Yanga, Abdulaziz Makame, akimlamba chenga mchezaji wa Zesco kwenye mechi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa iliyochezwa jijini Dar es Salaam.

# YANGA, AZAM ZILIVYOFIA MAPEMA HAPA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

MATUMAINI ya timu za Tanzania kufanya vema kwenye michuano ya kimataifa msimu huu yamefifia rasmi Jumamosi iliyopita, baada ya wawakilishi wawili, Yanga na Azam kufungwa na kutolewa kwenye michuano hiyo.

Yanga, iliyokuwa ikiiwakilisha Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, ilihitimisha safari yake hiyo kwa kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya Zesco ya Zambia, mechi ikichezwa Uwanja wa Levy Mwanawasa nchini Zambia.

Kwa maana hiyo Yanga imetolewa kwa jumla ya mabao 3-2 kwani, mechi ya kwanza wiki mbili zilizopita jijini Dar es Salaam, ililazimishwa sare ya bao 1-1.

Imeshindwa kutinga hatua ya makundi kama ilivyokuwa kwa watani zao wa jadi Simba msimu uliopita ilivyoitoa Nkana FC kwa jumla ya mabao 4-3, ilifungwa mabao 2-1 ikiwa ugenini, Zambia na kushinda mabao 3-1 nchini Tanzania.

Yanga sasa imetupwa kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, ikisubiri ratiba ili ijue timu gani itakumbana nayo kwenye mechi ya mchujo ili kukata tiketi ya kucheza hatua ya makundi ya kinyang'anyiro hicho.

Hali ni mbaya kwa Azam FC, iliyokuwa ikiiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho, ikiwa ugenini ikichapwa bao 1-0 kama ilivyokuwa kwenye mechi ya kwanza wiki mbili zilizopita nchini Tanzania na kutupwa nje kwenye michuano hiyo kwa jumla ya mabao 2-0.

Ni nini kimetokea kwa timu hizo kutupwa nje ya michuano iliyokuwa inawakilisha na nini kimesababisha?

**1. Kutotumia vema viwanja vya nyumbani**

Sababu moja ya msingi sana kwa timu za Yanga na Azam kutolewa kwenye michuano iliyokuwa ikiwakilisha ni kushindwa kutumia vema viwanja vyao vya nyumbani.

Pamoja na kwamba Yanga ilikuwa na matumaini zaidi ya kushinda ugenini kwa madai kuwa huwa inafanya vema sana ugenini kuliko nyumbani, lakini hali hiyo si ya kutegemea sana kwani huwa inatokea mara chache sana.

Dunia nzima ya soka, timu zote huwa zinaona fahari zaidi kushinda nyumbani na mara nyingi hutumia viwanja hivyo kumaliza mchezo, au kuiweka timu pinzani kwenye hali ngumu. Timu yoyote inayoshindwa kushinda nyumbani, inakuwa kwenye mashaka makubwa.

Na ndivyo ilivyotokea. Na hii tunaweza kusema kuwa Yanga na Azam zilitolewa hapa hapa Tanzania baada ya matokeo ya mechi za kwanza.

Sare ya bao 1-1 nyumbani, iliwapa kazi rahisi Zesco kumaliza mchezo nyumbani. Kama Yanga ingeshinda bao 1-0, basi pamoja na kipigo cha mabao 2-1 ugenini, kingewawezesha kusonga mbele kwa bao la ugenini. Timu hizo zingekuwa zimefungana mabao 2-2 kwa matokeo ya jumla, lakini bao ililolipata nchini Zambia lingewawezesha kutinga hatua ya makundi.

Bao la dakika za majeruhi la Thabani Kamusoko Uwanja wa Taifa, liliumaliza mchezo wenyewe.

Kwa upande wa Azam, kipigo cha bao 1-0 nyumbani, huwa inatokea mara chache sana kwa timu kupindua matokeo ugenini hasa kwenye soka la Kiafrika.

Ndiyo maana haikushangaza kuona Azam ikikubali kipigo kingine cha bao 1-0 dhidi ya Triangle ya Zimbabwe.

**2. Yanga bado haichezi kitimu**

Pamoja na kwamba wachezaji mmoja mmoja wa Yanga wameonekana kupambana sana kwenye mechi zote nne za Ligi ya Mabingwa, dhidi ya Township Rollers ya Botswana na pia Zesco FC, lakini wameonekana kukosa muunganiko na bado hawachezi kitimu.

Wachezaji wa Yanga wameonekana kucheza kwa bidii, wakijitolea kucheza kwa ari, nguvu, bidii na kujitolewa, lakini wanakosa maarifa kidogo, hasa cha kufanya ili kulifikia lango la wapinzani kirahisi na kufunga mabao.

Moja kati ya sehemu ya kujivunia ya Yanga ni mabeki wa kati. Kelvin Yondani, na Mghana Lamine Moro ambao wameonekana ni mabeki wakakamavu na wenye uwezo mkubwa wa kupambana na mastraika hatari, lakini tatizo linaanzia kwa mabeki wa pembeni.

Kwa sasa Kocha Mkuu Mwinyi Zahera anawatumia Ally Ally na Ally Sonso kama mabeki wa pembeni hata kwenye mechi dhidi ya Zesco, wakati mwingine hata Mapinduzi Balama, lakini kiasili Ally na mwenzake Sonso ni mabeki wa kati, Mapunduzi ni kiungo, hivyo inawapa tabu sana kucheza nafasi hizo, pamoja na kujituma kwao, lakini wanasababisha makosa mengi yanayoifanya timu kufungwa mabao mepesi.

**3. Mfumo wa mipira mirefu tatizo**

Yanga iliendelea kutumia mfumo wake ule ule wa mabeki kupiga mipira mirefu kwenda mbele, badala ya kutumia viungo kusafirisha mashambulizi.

George Lwandamina anaonekana aliisoma hiyo na kutengeneza mfumo ambao haukuwapa nafasi Yanga kufanya wanavyotaka.

Na ukitazama mipira yote mirefu aliyekuwa akipelekewa ni Mnamibia Sadney Ukhrob ambaye alilazimika muda mwingi awe anakimbizana na mpira na mabeki watatu wa Zesco ambao walikariri kuwa mipira yote mirefu anapelekewa straika huyo.

Alikosa muda wa kumpumzika. Hakuna straika yeyote duniani ambaye atataka muda wote awe anapelekewa mipira mirefu yeye ili awe anakimbizana na mabeki. Itafika wakati atachoka. Na ndicho kilichotokea. Sadney alitakiwa atafutiwe mipira ambayo ataipokea kutoka kwa viungo akiwa karibu nao na kuuweka mpira mguuni ili ajue la kufanya.

**4. Kupaki basi pia kumeigharimu**

Kwenye mechi zote mbili dhidi ya Zesco, staili ya kujilinda zaidi kuliko kushambulia, kumeisababishia Yanga kutolewa kwenye michuano hiyo.

Kwenye mechi ya kwanza nchini timu hizo zilipotoka sare ya bao 1-1, kitendo cha kuridhika na bao moja, badala ya kutafuta la pili, ikawa imerudi nyuma kulinda bao hilo. Hapo ndipo ilipokaribisha mashambulizi, kabla ya Kamusoko kufunga bao dakika za majeruhi.

Kwenye mechi ya Jumamosi, baada ya kuona dakika zinazidi kuyoyoma na bao ni 1-1, ilionekana kama Yanga ilihitaji zaidi sare hiyo ili iende kwenye matuta kuliko Zesco.

Wenyeji walianzisha mashambulizi mfululizo, huku Yanga wakikubali kushambuliwa hadi kufikia kujifunga wenyewe kutokana na kuzidiwa na mashambulizi.

**Azam nayo ijipange**


Msimu huu inaonekana kuwa Azam haiko vizuri upande wa mabeki, lakini pia ushambuliaji, badala yake imeimarika kwenye viungo tu.

Kwenye mechi zote mbili, Azam imeonekana kupata nafasi nyingi, lakini imeshindwa kuzitumia.

Kwa sababu imeshatolewa, uongozi wa Azam unatakiwa ukae chini na kufanya usajili wa maana unaoweza kuirudisha tena kuwa timu ya kuogopwa si kwenye michuano ya kimataifa tu, hata kwenye Ligi Kuu kwa sababu haionekani kutisha hata ikicheza na timu za hapa hapa Tanzania kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

## NJE YA UWANJA

KIPA wa Juventus, Gianluigi Buffon, amevunja rekodi ya kucheza mechi nyingi ngazi klabu iliyokuwa ikishikiliwa na Paolo Maldini. Buffon amerudi Turin baada ya kuitumikia Paris Saint-Germain kwa msimu mmoja, na Jumamosi alicheza mechi yake ya 903 hapo Juve wakati wakishinda mabao 2-0 kwenye Serie A dhidi ya SPAL, hivyo kuivunja rekodi ya Maldini.



# MAKOCHA WA5

## WALIOKALIA KITI CHA MOTO LIGI ULAYA



**LONDON, England**

MSIMU mpya wa 2019/20 umeanza kushika kasi sasa, huku Ligi Kuu barani Ulaya zikishuhudia timu zikiwa zimeshacheza mechi tano au sita, na tayari tumeshuhudia kocha wa kwanza ametimuliwa katika klabu yake.

Javi Gracia ambaye alikuwa kocha wa Watford alitimuliwa katika wiki ya kwanza ya Septemba kutokana na timu hiyo kuanza vibaya kwenye Ligi Kuu.

Lakini kitu kimoja muhimu ni kwamba, Gracia hatakuwa kocha wa kwanza kupoteza kazi yake msimu huu.

Kwa hali jinsi ilivyo kwa msimu huu 2019/20 hadi sasa, nani anaweza kujua makocha wangapi wanaweza kupoteza kazi zao?

Makala haya yanakuchambulia makocha watano ambao wanaweza kuwa kwenye presha kubwa zaidi kwa sasa, na mmoja wao au zaidi wanaweza kujiunga na Gracia.

**1. Ole Gunnar Solskjaer**

Mambo yanaonekana kwa sasa kuwa ni magumu kwa Ole Gunnar Solskjaer ambaye amerudi kwa 'Mashetani Wekundu' hao kama kocha baada ya kuitumikia akiwa kama mchezaji.

Alimalizia msimu wa 2018/19 kwa kushinda mechi mbili tu kati ya tisa za mwisho, na katika mchezo wake wa mwisho walifungwa na Cardiff City ambao wameshuka daraja.

Walianza msimu wa 2019/20 kwa kuwafumua Chelsea mabao 4-0, na ilionekana kama sasa mambo yatakwenda vizuri, lakini baada ya mechi tano baadaye, mambo yamekwenda tofauti kabisa.

Tangu hapo, United imeshinda mechi moja tu ya ligi - kwa kuifunga Leicester City shukrani kwa bao la penalti ya Marcus Rashford - huku wakipokea kipigo kutoka kwa West Ham na Crystal Palace, na mechi zote zikipigwa kwenye dimba lao la Old Trafford.

Sare dhidi ya Wolves na Southampton ilikuwa ngumu kwao, lakini ikapata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Astana ya Kazakh kwenye Kombe la Ligi ya Europa.

Na sasa mambo yanaonekana magumu kwa kikosi hicho cha pale Old Trafford. Wakati wachezaji wapya waliosajili kama Aaron Wan-Bissaka, Harry Maguire na Daniel James wameanza msimu kwa kuwa na kiwango kizuri, wachezaji wengine muhimu wamekumbwa na majeraha kama vile Luke Shaw, Paul Pogba, Anthony Martial na Marcus Rashford.

Ingawa Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa United, Ed Woodward bado anaamini kwamba Solskjaer ana uwezo wa kubadilisha upepo hapo Old Trafford, ni ngumu kuwa na uhakika kwamba, Mashetani Wekundu hao watamvumilia kama mambo yakizidi kwenda kombo.

**2. Nuno Espirito Santo**

Wakati msimu wa 2018/19 wa Ligi Kuu ya England ulipomalizika na kushuhudia Wolves ikimaliza nafasi ya saba, ilionekana wazi kwamba kocha wake, Nuno Espirito Santo hangefanya vibaya msimu huu. Kocha huyo raia wa Ureno alikiongoza kikosi chake kwa matokeo ya kuvutia akipata ushindi kwa timu kama Chelsea, Tottenham, Arsenal na Manchester United - na wachezaji kama Ruben Neves na Raul Jimenez wakionyesha kiwango cha kuvutia na wachambuzi wengi walikitabiria kwamba kikosi hicho cha pale Midlanders msimu huu kitamaliza nafasi ya sita.

Bahati mbaya kwa kocha huyo ambaye ni golikipa wa zamani, mambo yanaonekana kwenda ndivyo sivyo. Baada ya kuanza kwa msimu mpya (kabla za jana), Wolves nashika nafasi ya 13 kwenye msimamo wa Ligi Kuu.

Sare dhidi ya Leicester City na Manchester United haikubaliki, lakini kipigo kikubwa kutoka kwa Chelsea na Everton kiliharibu kabisa mambo.

Msimu uliopita, safu ya ulinzi ya Wolves ilikuwa ngumu mno kuipita katika timu sita za juu, ikiruhusu kufungwa mabao 46, lakini msimu huu tayari imeshafungwa mabao 11.

**3. Marco Silva**

Wakati msimu huu wa 2019/20 ukianza, kuna timu nyingi zilitabiriwa kwamba zitamaliza katika sita bora kwenye msimamo. Mashabiki wengi walihisi kwamba, msimu huu moja kati ya Leicester City, Everton, Wolves au West Ham inaweza kutinga kwenye sita bora.

Lakini wakati Leicester na West Ham angalau zikionekana kama zinauelekeo huo, timu nyingine mambo ni magumu. Wolves wanaweza kujitetea kwa ratiba yao katika mechi za Ligi ya Europa, lakini vipi kuhusu Everton?

Kwa Marco Silva na Everton yake, ni ngumu kutafuta sababu ya kushindwa kuwa na matokeo mazuri hadi sasa msimu huu. Everton ilipata ushindi wa 3-2 dhidi ya Wolves na ushindi wa 1-0 dhidi ya Watford, lakini wamekumbana na vichapo vinne, viwili kati yake wakivipata kutoka kwa timu zilizopanda daraja Sheffield United na Aston Villa kabla ya Jumamosi kuadhibiwa na Manchester City.

Hivyo, kwa namna mambo yanavyokwenda pale Goodison Park, kocha Silva ana wakati mgumu wa kuendelea na nafasi yake hiyo hadi mwisho wa msimu kama mambo hayatabadilika.

Silva alimuuza kiungo bora kabisa kwenye kikosi hicho, Idrissa Gueye aliyetua kule Paris St. Germain kipindi cha majira ya joto kilichopita na licha ya kuimarisha kikosi chake kwa kuwanunua wachezaji kama Fabian Delph, Moise Kean na Alex Iwobi, mambo bado hayajakaa sawa kwa kocha huyo raia wa Ureno.

**4. Unai Emery**

Bila shaka, mshindi wa Kiatu cha Dhahabu kwa ufungaji mabao wa msimu uliopita, Pierre-Emerick Aubameyang bado anaendelea na kazi yake ile ile. Hadi sasa amefunga mabao 11 katika mechi 6 za ufunguzi, na Arsenal wameruhusu kufungwa mabao 10.

Takwimu zinaonyesha kwamba, safu ya ulinzi ya Arsenal ni mbovu kwani imekuwa ikifanya makosa mengi yanayosababisha kufungwa mabao, licha ya kumwongeza David Luiz.

Emery anaweza kujitetea kwamba, mabeki wake, Rob Holding, Hector Bellerin na Kieran Tierney bado hawajarudi kutoka chumba cha majeruhi, lakini kikosi hicho kujikuta kikizuiwa na Watford kulizua maswali mengi.

**5. Zinedine Zidane**

Tukiondoka kwenye Ligi Kuu ya England na kuiangalia moja ya klabu kubwa barani Ulaya, ni wazi kwamba kocha ambaye yupo kwenye presha kubwa zaidi kwa sasa ni gwiji wa Ufaransa, Zinedine Zidane, ambaye aliichukua Real Madrid Machi mwaka huu baada ya kuondoka klabuni hapo kwa mwaka mmoja.

Real Madrid kwenye Ligi Kuu Hispania, La Liga kiwango chake si kibaya kivile, kwani wameshinda mechi nne kati ya saba.

Lakini maswali mengi yanaibuka kutokana na wachezaji waliosajiliwa katika kikosi hicho, kwani mchezaji wao mpya, Eden Hazard bado hajaonyesha kiwango chake tangu alipotua hapo akitokea kule Chelsea.

Matokeo mabaya zaidi yalikuwa kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi, wakati walipofungwa na Paris St. Germain mabao 3-0.

Matokeo yakiendelea kuwa si ya kuvutia kwa kikosi hicho, kuna uwezekano mkubwa Zidane anaweza asimalize msimu huu akiwa na Real Madrid, huku tayari kocha wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino akitajwa kama ndiye anayeonekana kuwa mrithi wake kama akitimuliwa.

## Nukuu

"Nadhani hapana [hawezi kuwa tayari kuanza dhidi ya Manchester United leo]. Labda ndani ya mawazo yake ndiyo. Tunahitaji kumsikiliza daktari. Dakika za kwanza zilikuwa zakushangaza kwake [kwenye mechi ya Kombe la Ligi dhidi ya Nottingham Forest]... Kitu cha muhimu zaidi ni mtazamo wake. Anataka kutusaidia," **Kocha wa Arsenal, Unai Emery akimzungumzia Hector Bellerin.**



"Messi amefanya kile anachokifanya kila msimu, hajaweza kuifikisha Barcelona ngazi tofauti na kuweza kutwaa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Unashinda kwa sababu ya kufanya kitu fulani cha kipekee, ambacho kwa Van Dijk alikifanya. Messi ameshinda tuzo [ya Mchezaji Bora wa Dunia 2019] kwa sababu walianza tuzo mwaka 2016, na kwa miaka miwili ya kwanza, Cristiano Ronaldo alishinda na mwaka jana Luka Modric akashinda. Sasa lazima wampe Messi," **Mchambuzi wa soka England na mchezaji na kocha wa zamani, Paul Merson, akiamini beki wa Liverpool, Virgil van Dijk alipaswa kutwaa tuzo hiyo.**



"Tayari tulishacheza pamoja tukiwa Real, miaka mingi imepita, na nimemuona mchezaji mwingine, mtu aliyepevuka zaidi, akiwa na familia. Nilifurahia kucheza pembeni yake kabla na ni mwenye furaha kuwa tupo pamoja tena," **Gonzalo Higuain akimzungumzia Cristiano Ronaldo wanayecheza naye kwa sasa Juventus.**



## Michezo




Meddie Kagere (kulia) akishangilia na wenzake baada ya kuiandikia Simba bao dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba Alhamisi iliyopita.

# KILICHOSABABISHA SIMBA KUVUNJA MWIKO KAITABA

**a Adam Fungamwango**

HATIMAYE mwiko umevunjwa, ndivyo unavyoweza kusema, baada ya Alhamisi iliyopita Simba kuichapa Kagera Sugar mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

Simba imekuwa ikipata tabu sana ikicheza na Kagera Sugar, si tu kwenye Uwanja wa Kaitaba, bali hata ikicheza Dar es Salaam.

Imekuwa ikipata shida hata kutoka sare. Simba ilifungwa mechi tatu mfululizo 'nje ndani', kabla ya matokeo ya Alhamisi iliyopita.

Mara ya mwisho Simba kuifunga Kagera Sugar ilikuwa ni Januari 22, 2018, Ligi Kuu ya msimu wa 2017/18 kwenye Uwanja wa Kaitaba iliposhinda mabao 2-0 yaliyofungwa na Said Ndemla na John Bocco.

Baada ya hapo ilikumbana na vipigo mfululizo, cha kwanza ni kwenye Uwanja wa Taifa wakati wa ikikabidhiwa Kombe la Ubingwa wa Ligi Kuu, mgeni rasmi akiwa na Rais John Magufuli. Ilikuwa ni Mei 19, 2018, Ligi Kuu ya msimu wa 2017/18 ilipochapwa bao 1-0.

Msimu uliofuata, ikienda mkoani Kagera, Simba iliambulia kipigo cha mabao 2-1 Aprili 20, mwaka huu Uwanja wa Kaitaba na mechi ya mzunguko wa pili msimu uliopita ikichezwa Uwanja wa Uhuru na Simba kupoteza kwa mara nyingine kwa bao 1-0, Mei 9, mwaka huu.

"Mengi yamesemwa kabla ya mechi hii, Kagera Sugar walikuwa wakiongea maneno mengi mno, lakini sisi tumewajibu kwa vitendo." Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems.

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar kwa upande wake alisema kuwa timu yake ilipoteza mechi kutokana na ubora mkubwa walionao Simba.

"Ni timu kubwa katika timu nne au tano za Afrika kwa sasa ukizitaja Simba itakuwamo, wao walikuwa hatari sana upande wa ushambuliaji. Tulifanya makosa. Simba ukiruhusu wakushambulie mara tatu mfululizo, basi mara moja ni lazima wakufunge. Tumeachana na hilo tunaangalia mechi nyingine." Ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga, Mecky Maxime.

Zifuatazo ni sababu ambazo zilisababisha Simba kufanikiwa kuvunja mwiko wa kunyanyaswa na Kagera Sugar.

**1. Simba ilienda Kagera kwa tahadhari**

Kutokana na rekodi mbovu, viongozi, benchi la ufundi na wachezaji walikwenda Kagera kucheza mechi hiyo huku wakiwa na tahadhari kubwa.

Simba ilikwenda kucheza mechi hiyo ikiwa na uangalifu zaidi kuliko hata ilivyokuwa kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya UD Songo.

Hata wachezaji wapya, waliambiwa wanakwenda kucheza na timu ya aina gani, pamoja na rekodi yao huko nyuma.

**2. Kagera Sugar waliichukulia poa Simba**

Wakati Simba ikienda kwa tahadhari, benchi la ufundi ya Kagera Sugar na wachezaji wake walionekana kuichukulia poa mechi hiyo kuwa inaweza tu kushinda kwa sababu ya historia na wanaonekana hawakujiongeza zaidi.

Nadhani hata Maxime alikariri mfumo wa Simba, lakini akakuta kitu tofauti hasa kwenye kipindi cha kwanza ambako mechi hiyo ndipo ilipomalizwa.

**3. Aussems alimpiga changa la macho Maxime**

Kama Maxime alidhani kuwa Simba ingecheza kwenye mfumo wao wa siku zote ambao unamfanya kuibuka na ushindi, basi alikosea.

Siku zote, Simba hufanya mashambulizi yake kupitia pembeni na hasa mabeki wa kulia na kushoto, huku wakijaza viungo wengi wachezeshaji kati.

Walichokuwa wakifanya Kagera Sugar ni kunyonya mashambulizi ya Simba na haraka wanapiga mipira mirefu pembeni kwa kuwatumia mawinga wao machachari, kabla mabeki wa pembeni hawajarejea. Mfumo huo huonekana kuwapa tabu sana Simba.

Aussems anaonekana aliangalia mechi zilizopita. Alichofanya aliwaheshimu wapinzani wake na kuwaacha viungo wa Kagera kukaa na mpira, huku viungo wa Simba wakiziba mianya yote ya kuwafikia mabeki kirahisi.

**4. Tshabalala tu ndiye aliyeruhusiwa kupanda zaidi**

Beki wa pembeni Mohamed Hussein 'Tshabalala' ndiye aliyeruhusiwa kupanda zaidi na kupiga krosi kuliko Shomari Kapombe.

Kwenye mechi ya Alhamisi, Kapombe alionekana kusaidiana zaidi na Deo Kanda, ambaye ni winga asilia hivyo upande wa kulia, beki huyo hakutakiwa kukaa sana mbele, kusaidia mashambulizi, kazi hiyo upande wa kulia ilikuwa kwa Kanda ambaye alisaidia kupatikana kwa bao la kwanza.

Hii ilisababisha Kagera hata wanapokwenda kwenye lango la Simba wanakuta kuna idadi kubwa ya wachezaji, tofauti na mechi iliyopita.

**5. Tairone aliilinda nafasi ya Tshabalala**

Wakati Tshabalala akiwa juu, na wachezaji wa Kagera Sugar wanapopata mpira kama kawaida yao walikuwa wakiitupa eneo la wazi ambalo beki huyo ametoka, kwa lengo lile lile la kupata nafasi mawinga wao kuchachafya na kwenda kupiga krosi za hatari.

Walichokutana nacho ni kwamba beki huyo anakuwa hayupo, beki wa kati Tairone Santos da Silva alikuwa akifika kwa wakati na kutibua mipango yote.

Wakati huo ni kwamba Mbrazil mwingine Gerson Fraga anakuwa ameshasogea nyuma na kuziba nafasi ya mwenzake aliyekwenda pembeni.

Kiungo mwingine Mzamiru Yassin naye anakuwa anasubiria lolote litakalotokea, Kapombe na Paschal Wawa nao wanakuwa wameshachukua nafasi zao, kama itatokea krosi ikapigwa.

Hiyo iliwafanya wachezaji wa Kagera japo walikuwa wakikaa na mpira muda mrefu, lakini hawakuwa na la kufanya kwa sababu njia walizotegemea zilikuwa zimezibwa.


**6. Bao la mapema liliwachanganya**

Kikubwa zaidi ni kwamba wachezaji wa Kagera Sugar walichanganywa na bao la mapema, dakika ya nne likifungwa na Meddie Kagere.

Ni kama liliwashtua na kuwatoa kwenye mchezo mzima. Bao la pili ndilo lilikuja kuwamaliza kabisa.

Hii ndiyo operesheni nzima iliyofanywa na Simba kwa lengo moja tu la kwenda mkoni Kagera kuvunja mwiko.

**NAJUA WAJUA**



KIKOSI cha Jurgen Klopp, Liverpool kimeshinda mechi 16 za Ligi Kuu England mfululizo, idadi ambayo inazidiwa na Manchester City tu kwenye ligi hiyo (iliyoshinda mechi 18 kati ya Agosti na Desemba 2017).

## SOKA

# ARSENAL INAVYOTESWA NA UNITED JUMATATU



Pogba

Bellerin

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United leo Jumatatu watakuwa katika dimba la Old Trafford kucheza na Arsenal kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, EPL.

Man United wanaingia kwenye mchezo huo wakiwa nafasi ya 11 na pointi 8.

Imeshinda mechi sita, ikashinda mbili, ikafungwa mbili na kutoka sare mbili, ikifunga mabao nane na kufungwa mabao sita.

Wao Arsenal wapo nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu wakiwa wamejikusanyia pointi 11 kutoka mechi sita walizocheza hadi sasa.

Wameshinda tatu kati ya hizo sita, wakitoka sare mbili na kufungwa moja na wametikisa nyavu mara 11 na wao wamefungwa mabao 10.

Mchezo huu unawakutanisha makocha ambao tayari wameshaanza kunyooshewa vidole na mashabiki wao kutokana na kiwango cha vikosi vyao kutowafurahisha.

Kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer anaonekana kuwa kwenye wakati mgumu baada ya kuanza vizuri mchezo wa kwanza wa ligi, lakini sasa mambo yanaonekana kwenda ndivyo sivyo, huku yule wa Arsenal Unai Emery naye atajwa kuwa anashinda kupanga kikosi chake.

Man United walianza vizuri kwenye Ligi Kuu na walikuwa na nafasi ya kushika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, lakini wameanguka tena.

Na sasa wanakutana na wapinzani wao Arsenal leo Jumatatu kwenye mchezo wa Ligi Kuu na presha kubwa ipo kwa kocha, Solskjaer anayetakiwa kujithibitishia ubora wake.

Timu hizi mbili ni kama pande mbili za sarafu moja kwenye viwango vyao kwenye Ligi Kuu katika miaka ya hivi karibuni.

United imekuwa imara zaidi kwenye ulinzi hadi sasa, ikicheza mechi kadhaa bila kuruhusu nyavu zao kutikiswa, lakini matatizo zaidi yapo kwenye safu yao ya ushambuliaji.

Kwa upande mwingine, Arsenal wanafunga mabao vizuri tu, lakini wao wanavyoruhusu nyavu zao kutikiswa ni sawa tu na mabao wanayofungwa.

**Kikosi kinachoweza kuanza cha Man United**

De Gea, Wan-Bissaka, Lindelof, Maguire, Young, Matic, McTominay, Pereira, Pogba, James, Martial

Marcus Rashford aliumia kwenye mchezo dhidi ya West Ham, na anatarajiwa kuukosa mchezo huu.

Solskjaer amesema kwamba ana matumaini kwamba Anthony Martial na Mason Greenwood wanaweza kucheza, huku Paul Pogba akionekana kupona kutoka majeruhi.

**Kikosi kinachoweza kuanza cha Arsenal**

Leno, Chambers, Sokratis, Luiz, Kolasinac, Xhaka, Guendouzi, Torreira, Ceballos, Pepe, Aubameyang.

Ainsley Maitland-Niles atakosa mchezo huu baada ya kutolewa nje kwenye mchezo dhidi ya Aston Villa, huku Hector Bellerin na Kieran Tierney bado hawajawa fiti kamili.

Alexandre Lacazette bado anauguza majeraha ya kifundo cha mguu na anatarajiwa kurudi uwanjani Oktoba.

Manchester United haijafungwa kwenye mechi zake 12 za mwisho za Ligi Kuu dhidi ya Arsenal kwenye Uwanja wa Old Trafford, tangu walipofungwa 1-0 Septemba 2006.


Arsenal itakuwa na nafasi ya kuandikisha ushindi mfululizo wa Ligi Kuu wakishinda dhidi ya United kwa mara ya kwanza tangu waliposhinda mechi zote katika msimu wa 2006-07.

Mechi zote za ugenini za Arsenal walizoshinda dhidi ya Man United zilichezwa siku ya Jumatano, Jumamosi na Jumapili.

Hii ni mara yao ya tatu wanakutana na Man United kwenye mchezo wa Ligi Kuu ukichezwa Jumatatu. Mara ya kwanza walikutana Januari 2000 na wakatoka sare ya kufungana bao 1-1 na mara ya pili ilikuwa ni Desemba 2010 wakafungwa 1-0.

Arsenal wamepata penalti moja na kupigiwa penalti tatu katika mechi zao nne zilizopita. Manchester United imepoteza mechi tatu kati ya sita zilizopita za Ligi Kuu.

**NDANI YA 18**



MSHAMBULIAJI wa Tottenham, Harry Kane, amefunga katika mechi ya sita mfululizo alizocheza dhidi ya Southampton kwenye Ligi Kuu England- ni Robin van Persie dhidi ya Stoke (mabao nane), Jimmy Floyd Hasselbaink dhidi ya West Ham (saba) na Romelu Lukaku dhidi ya West Ham (saba) waliofunga zaidi yake mfululizo dhdi ya mpinzani mmoja kwenye ligi hiyo.

Nipashe
# Spotika



MSIMU mpya wa 2019/20 umeanza kushika kasi sasa, huku Ligi Kuu barani Ulaya zikishuhudia timu zikiwa zimesha-cheza mechi tano au sita, na tayari tume-shuhudia kocha wa kwanza ametimuliwa katika klabu yake.

**Uk. 16-17**

# FATI

## ANAVYOTEMBELEA MWAMVULI WA MESSI




**BARCELONA, Hispania**

WAKATI watu wachache walishuhudia na kuukubali uwezo wa Ansu Fati ambao umekuja katika umri wa miaka 16 tu, Barcelona kamwe hawakuwa na shaka kuhusu kiwango chake na wanaonekana kumpa nafasi zaidi ya kung'ara msimu huu.

Akiwa zao kutoka kitalu cha kuzalisha wachezaji cha La Masia pamoja na Ilaix Moriba - Fati alikuwa kwenye rada za Barca katika kikosi cha kwanza kwa muda mrefu.

Na kocha Ernesto Valverde hakusita kumpandisha na kumpa nafasi wakati majeraha ya Ousmane Dembele yalipofungua mlango wa kucheza kikosi cha kwanza kwa kinda huyo.

Kuwa mchezaji wa kwanza mwenye umri mdogo zaidi kwa miamba hao wa Catalunya tangu mwaka 1941, wakati alipocheza dhidi ya Real Betis Agosti, haraka mshambuliaji huyo kinda akawa mvunja rekodi.

Fati kwa sasa ndiye mchezaji wa Barcelona mwenye umri mdogo zaidi kufunga kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, wakati alipotikisa nyavu dhidi ya Osasuna.

Na pia ndiye mchezaji wao mwenye umri mdogo zaidi kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati alipoanza kwenye mchezo wa kwanza wa Barca hatua ya makundi dhidi ya Borussia Dortmund uliomalizika kwa sare ya bila kufungana.

Umekuwa mwanzo rahisi wa kung'ara kwa maisha ya soka ya kinda huyo na kuonyesha muunganiko mzuri zaidi kwenye safu ya ushambuliaji ya Barca.

"Ni mchezaji ambaye ana kitu fulani maalumu. Katika umri wake anaonyesha kupevuka zaidi," alisema Valverde baada ya Fati kutoa pasi ya mwisho ya bao kwenye mchezo dhidi ya Valencia.

"Kile unachokiona mazoezini ndicho kile unachokiona hapa."

Wakati haraka akijijengea jina lake pale Camp Nou, miamba hao wa Catalunya walitakiwa kutumia nguvu ya ziada kumbakisha kikosini kipindi cha majira ya joto, huku klabu kama Real Madrid, Sevilla, West Ham na Nice zilipigana vikumbo kuwania saini yake kabla ya Fati kushawishika kusaini mkataba mpya.

Sababu kubwa ya kukubali kusaini mkataba mpya ni baada ya kuhakikishiwa na Barcelona kwamba atacheza kama winga na si namba tisa kama alivyokuwa akicheza wakati akiwa pale kwenye kituo cha kulelea vipaji cha La Masia.

Kubadilishwa huko kwa nafasi ya kucheza, ilionekana kama njia bora zaidi ili kuweza kumpa nafasi, lakini pia kuongeza nafasi zaidi ya kucheza.

Na nafasi hiyo hadi sasa imelipa kwa wote, Barca na Fati, huku kinda huyo akionekana kuwa hatari zaidi akicheza katika winga zote mbili.

Pia hajapoteza asili yake ya kufunga mabao, kwani hadi sasa ametikisa nyavu mara mbili kwenye mechi za Ligi Kuu.

Mabao yote mawili kwa mzaliwa huyo wa Guinea-Bissau aliyafunga baada ya kuingia kwenye eneo la boksi na akacheza kwa urahisi zaidi.

Pamoja akiwa anajifunza mengi kutoka kwa nyota wa Barca akiwa uwanjani, Fati pia anapata msaada mkubwa wa usimamizi kutoka kwa Rodrigo Messi, kaka wa Lionel, ambaye alikuwa wakala wake kipindi cha majira joto kilichopita.

Kama ilivyokuwa kwa Ronaldinho na wakala wake ambaye alikuwa kaka yake Roberto de Assis, alimsaidia zaidi Messi wakati akipenya kwenye kikosi cha kwanza.

Na sasa kinda huyo pia amepata nafasi ya kusaidiwa na kaka wa nyota wa Barca, Messi kupenya kwenye kikosi cha kwanza, hivyo majaliwa yake yanaonekana kuwa hapo Camp Nou, kwani mkataba mpya wa Fati una kipengele cha kumuuza kwa euro milioni 100.

Wakiwa wamewaruhusu nyota wengine wenye vipaji kutoka La Masia, Xavi Simons na Takefusa Kubo kwenda kucheza sehemu nyingine, Barcelona wamemhakikishia Fati kwamba hatafuata nyayo zao.

Ingawa Fati amepitwa miaka sita na Dembele, lakini haraka ameonekana kuwa na kiwango cha kuvutia zaidi.

"Popote unapokuwapo, mchezaji anayepata nafasi ya kucheza ni yule anayecheza, hakuna siri katika hilo, makocha wanataka wachezaji kuwatumia hasa wanapokuwa vijana kwani wanakuwa na nguvu zaidi," alisema Valverde wiki iliyopita.

**USILOLIJUA**

Manchester City imefunga mabao 27 katika mechi zake saba za ufunguzi za Ligi Kuu msimu huu, idadi ambayo ni kubwa zaidi kuwahi kufungwa katika mechi saba za ufunguzi kwa msimu tangu Everton ilipofanya hivyo msimu wa 1894-95 (ilipotupia mabao 27).



# Utekelezaji agizo la JPM Magereza wazaa matunda

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

AGIZO la Rais John Magufuli kwa Jeshi la Magereza nchini kuhakikisha linajitegemeza kwa chakula cha wafungwa limeanza kufanikiwa, ambapo kwa sasa limefikia asilimia 70 ya kujitegemea kutokana na kuongeza uzalishaji.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Kamishna wa Jeshi la Magereza, Sheria na Uendeshaji, Uwesu Ngarama, alipokuwa anafunga mafunzo ya uongozi daraja la kwanza kwa askari magereza 915 ambao walitunukiwa cheo cha ukoplo.

Mafunzo hayo yalikuwa yanafanyika katika Chuo cha Magereza Kiwira kilichopo wilayani Rungwe, ambapo Kamishna Ngarama alisema tangu Rais Magufuli atoe agizo la jeshi hilo kujitegemea, wameongeza uzalishaji kwa kiwango kikubwa.

Alisema jeshi hilo linatekeleza agizo hilo kwa awamu na linatarajia kuanza kujitegemea kwa asilimia 100 baada ya muda mfupi kutokana na kasi yake kuwa kubwa.

"Ni mwaka mmoja pekee tangu tulipoanza kutekeleza agizo hilo la Mheshimiwa Rais, lakini tumefikia asilimia zaidi ya 70 na kutokana na kasi hii nina uhakika tutafanikiwa kuanza kujitegemea kwa asilimia 100 baada ya miaka michache ijayo," alisema Kamishna Ngarama.

Kamishna Ngarama alisema mafunzo yatasaidia kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa jeshi hilo na kuendana na kasi ya serikali ya awamu ya tano inayotarajia kuliingiza taifa kwenye nchi za uchumi wa kati.

Aliwataka wahitimu kwenda kuwafundisha wenzao mbinu walizojifunza ikiwamo namna bora ya kuishi na wafungwa na kuongoza shughuli mbalimbali zinazofanyika.

Mkuu wa Chuo cha Magereza Kiwira, Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Magereza, Adriano Mduda, alisema mafunzo ambayo askari hao wameyapata ndio msingi wa uongozi ndani ya Jeshi la Magereza nchini.

Alisema mafunzo hayo yalianza Juni 15 mwaka huu na kwamba walianza askari 952, lakini waliohitimu wako 915 kufuatia wengine 37 kushindwa kumaliza kutokana na sababu mbalimbali.

Mmoja wa wahitimu hao, Koplo Zahara Majumba, alisema mafunzo hayo hayamaanishi kuwa wao hawakuwa askari bali ni kwa ajili ya kuwaongezea baadhi ya vitu vya kiuongozi ambavyo walikuwa hawajavipata katika ngazi ya awali.



Askari wa Jeshi la Magereza wakionyesha ukakamavu wakati wa hafla ya kuwatunuku cheo cha ukoplo baada ya kumaliza mafunzo ya uongozi katika Chuo cha Magereza Kiwira mkoani Mbeya. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Tanesco yatakiwa kubuni vyanzo zaidi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHIRIKA la Umeme Tanzania (Tanesco), limeshauriwa kubuni vyanzo vingine vya kuzalisha nishati ya umeme badala ya kutegemea chanzo cha maji ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi ambayo inaikabili dunia kwa sasa.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, wakati wa mkutano kati ya watendaji wa Tanesco na wateja wakubwa wa shirika hiyo kutoka katika mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi.

Alishauri kuongeza nguvu katika kuwekeza kwenye umeme unaotokana na Joto Ardhi, huku akieleza kuwa vyanzo vya aina hiyo vipo vingi na wataalamu wamethibitisha kuwa vina uwezo wa kuzalisha umeme mwingi. "Hata hapa kwetu Mbeya vyanzo vya aina hiyo vipo vya kutosha, kwenye Ziwa Ngozi wataalamu wamethibitisha kuwa joto ardhi lililopo linaweza likatusaidia kuzalisha umeme mwingi na hiyo ndio mbinu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi," alisema Chalamila.

Meneja wa Tanesco Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Magharibi, Mhandisi Salome Nkondola, alisema lengo la mkutano huo ni kuzungumza na wateja wakubwa na kujua changamoto zinazowakabili ili kuzitafutia suluhisho.

Alisema wateja wakubwa wanaliingizia shirika fedha nyingi, na kwamba ndio maana wameona waanzishe utaratibu wa kukutana nao na kuzungumza nao kuhusu changamoto zinazowakabili.

Alisema asilimia 50 ya mapato ya Tanesco yanachangiwa na wateja wakubwa na asilimia 50 inayobakia inachangiwa na makundi mengine yanayobakia hivyo akasisitiza kuwa kundi hilo ni mhimu kwenye maendeleo.

"Shirika kwa sasa limeanzisha kitengo maalumu kwa ajili ya kuwahudumia wateja wakubwa ili kuwarahisishia upatikanaji wa huduma, maana kundi hili lina upekee wake katika uchangiaji wa mapato ya shirika," alisema Mhandisi Nkondola.

Katika hatua nyingine Nkondola alisema kwa sasa shirika hilo halina changamoto kubwa ya taasisi za umma kulimbikiza madeni kama ilivyokuwa awali.

Alisema kwa sasa yapo madeni ya kawaida ambayo yanalipika na kwamba shirika linaendelea na utaratibu wa kutoa elimu na kuhamasisha wananchi na taasisi kulipia huduma hiyo.

Vilevile alipongeza kwa kutekeleza miradi mikubwa ya umeme ambayo iliasisiwa miaka mingi, lakini ilikuwa haijatekelezwa ukiwamo mradi wa Nyerere Hydro- Electric Power ambao alidai utamaliza changamoto ya uhaba wa umeme nchini.

Meneja wa Tanesco Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Fadhili Kalisa, alisema mkutano huo utalisaidia shirika kupata maoni ya wateja hao wakubwa na kuyatumia katika kuboresha huduma.

Baadhi ya wateja wakubwa walisema wanaridhishwa na huduma wanazopatiwa na Tanesco, kwa maelezo wanatembelewa hadi kwenye maeneo yao ya kazi na kuwauliza kama kuna changamoto zinawakabili.

## Jafo akumbushia alivyonusurika ajali

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amekumbushia namna alivyonusurika kwenye ajali ya gari mwaka 2016 wilayani Rungwe akiwa Naibu Waziri wa Wizara hiyo.

Alikumbushia tukio hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kata ya Isongole wilayani Rungwe wakati alipokabidhi kwa niaba ya Rais John Magufuli mchango wa Sh. milioni 30 kwa wananchi wa kata hiyo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa kituo cha afya.

Kwenye makabidhiano hayo aliutaka uongozi wa Wilaya ya Rungwe kukamilisha ujenzi wa kituo hicho ndani ya mwezi mmoja ili kifunguliwe na wananchi waanze kupata huduma.

Alisema Septemba 5 mwaka 2016 akiwa Naibu Waziri wa Tamisemi, alitoa maagizo makali kwa viongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Rungwe (Makandana) na wakati akiwa njiani kuelekea Mbeya Mjini, alipata ajali pamoja na wasaidizi wake.

"Nina historia na wilaya hii, niliwahi kutoa maagizo katika Hospitali ya Makandana nikiwataka viongozi wafunge mfumo wa ukusanyaji mapato, sasa tukiwa njiani tulipata ajali ambayo hata hivyo tulinusurika, nilifikiria kwamba hawa watu yawezekana hawakufurahishwa na maagizo yangu," alisema Jafo. Hata hivyo, alisema Wilaya ya Rungwe inafanya vizuri kwenye utekelezaji wa miradi ya afya ambayo inafadhiliwa na serikali, huku akiwasifia wabunge wa wilaya hiyo kwa ufuatiliaji wa fedha za miradi hiyo pamoja na usimamizi.


Alisema kituo cha kwanza cha majaribio kutekelezwa kwa kutumia mfumo wa akaunti ya dharura (Force Acount) ni cha Ikuti kilichopo wilayani humo na kwamba ndiyo wilaya iliyopewa vituo vingi kwa Mkoa wa Mbeya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema Kata ya Isongole ina wananchi 10,016 ambao wanashiriki ujenzi wa kituo cha afya kwa nguvu zao na kwamba kitanufaisha na kata zingine jirani. Alimshukuru Rais John Magufuli kwa mchango aliowapatia wananchi hao, na kwamba Mbeya ni miongoni mwa mikoa iliyopata upendeleo kwenye ujenzi wa vituo vya afya kwa maelezo kuwa imepewa vituo 14 ambavyo baadhi vimeshakamilika.

"Mheshimiwa Waziri, umesema mpaka kufikia Oktoba 30 kiwe kimekamilika, lakini mimi nashusha mpaka Oktoba 20 kitakuwa kimekamilika, tunapoondoka hapa wataalamu wanabaki hapa kufanya kikao na kesho watanileteea taarifa ya namna ya kuitumia hiyo Sh. milioni 30," alisema Chalamila.

Alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kupeleka Sh. milioni 25 ambazo waliahidi kuzipeleka katika kituo hicho ili zifanye kazi pamoja na zilizotolewa na Rais.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Julius Chalya, alisema wilaya hiyo imepewa vituo vya afya vitano ambavyo serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi na kwamba katika Halmashauri ya Rungwe vinajengwa vitatu na Busokelo viwili.





# Walimu wa kutengeneza mashine za nukta nundu kupewa mafunzo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeanza mchakato wa kufundisha walimu 20, ambao watakuwa wakufunzi wa wengine kwenye utengenezaji wa mashine za nukta nundu (braille machine) kwa ajili ya wanafunzi wasioona.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mratibu wa Elimu Maalum wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Mkali, wakati wa kikao na walimu mafundi wa kutengeneza mashine hizo kilichoandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Sense International (EA) Tanzania linalojihusisha na kuwawezesha watoto wasioona. Alisema lengo la mkakati huo ni kuwezesha walimu wanaofundisha katika shule za wanafunzi wenye mahitaji maalum kupata fursa ya kusoma bila kuwapo kwa vikwazo.

"Changamoto kubwa iliyopo kwa hawa wanafunzi wasioona katika shule zetu maalum ni kuharibika kwa mashine hizo na kukosa mafundi, hivyo kuwakosesha fursa ya kushiriki masomo watoto ambao wanatumia mashine hizo, lakini tukiwafundisha hawa 20, wataweza kwenda kufundisha wengine," alisema.

Mkali alisema wakufunzi hao watakuwa walimu wa walimu ambao watakwenda kusaidia katika shule za wanafunzi wenye mahitaji maalum hasa wale wasioona takribani shule 180, katika kanda zote za kielimu.

Mmoja wa walimu wa elimu maalum ambaye ni fundi wa kutengeneza mashine hizo, Veronica Kasidi, alisema kuwa wanakabiliwa na changamoto nyingi katika kuwezesha watoto wasio ona kufikia malengo yao.

"Hali bado ni mbaya sana hivi sasa toka serikali itangaze elimu bila malipo wazazi hawawaficha tena watoto wenye ulemavu wa macho nyumbani, hivyo tunakabiliwa na changamoto ya uhaba wa mashine hizi," alisema.

Alisema pamoja na kukabiliwa na changamoto ya uhaba wa mashine pia bado ukarabati wake ni wa gharama ya juu sana.

"Hali katika maeneo yetu bado ni mbaya mashine hizi kwanza hakuna spea, wakati fulani tunalazimika kufoji (kughushi) hata spea za baiskeli tuu, lakini inapoanguka basi haifanyi kazi tena," alisema.

Naye Mkufunzi Elimu Maalum kutoka Chuo cha Ualimu Katavi, Lucas Kivuyo, alisema suala la uelewa kwa jamii bado ni changamoto, lakini vifaa kama karatasi kwa ajili ya kuandikia katika mashine hizo zinauzwa bei kubwa ambayo ni vigumu kuimudu.

Mkurugenzi mkazi wa Shirika hilo, Naomi Lugoe, alisema shirika hilo limesajiliwa kufanya kazi na wadau wanaoshiriki katika kutoa elimu kwa watoto wasio ona ili kuwawezesha kufikia ndoto zao. "Leo hii hapa tumewaita walimu wapatao 40, kutoka shule za wanafunzi wenye ulemavu wa macho, lakini ni mafundi wa mashine katika maeneo yao ili kuweza kujadiliana changamoto wanazokutana nazo pamoja na kuwajengea uelewa katika teknolojia mpya," alisema Lugoe.




Meneja Masoko na Uendelezaji Biashara wa TBL, Edith Bebwa (kushoto), akimkabidhi cheti mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya kuendeleza wajasiriamali inaoshirikiana nao kibiashara, Monica Kimaro (kulia), katika mahafali yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine pichani ni maofisa waandamizi wa kampuni hiyo, Sylvester Sizya (kulia) na Amanda Walter. Mafunzo hayo yaliandaliwa na TBL na tayari yamefikia wajasiriamali 183 tangu yalipoanzishwa mwaka jana kutoka mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watakiwa kutoa elimu ya malisho kwa wafugaji

**Na Renatha Msungu,** MPWAPWA

SERIKALI imewaagiza wataalamu wa malisho kwenye halmashauri kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu matumizi bora na endelevu ya nyanda za malisho.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alitoa agizo hilo wakati akifungua mafunzo ya wataalamu kwa wadau wa malisho nchini yaliyofanyika mwishoni mwa wiki katika Chuo cha Mifugo LITA kampasi ya Mpwapwa.

Alisema elimu ya utunzaji malisho ni muhimu kwa wafugaji kwa sababu itawasaidia kujua nini wanatakiwa kufanya ili kudhibiti uhaba wa malisho pale unapotokea.

Mkuu huyo alisema lengo lao ni kuona maofisa ugani hao wanatumia nafasi walionayo kutoa elimu hiyo kiufanisi kwa wafugaji katika halmashauri wanazotoka ili kusaidia kupunguza migogoro baina ya wafugaji na wakulima kugombea maeneo ya malisho.

"Mafunzo mliopata mkayatoe kwa wafugaji katika sehemu mnazotoka, tumieni nafasi yenu ili kuisaidia serikali ya awamu ya tano kuboresha sekta ya mifugo," alisema Shekimweri.

Aidha, aliwataka kuhamasisha na kuongeza uvunaji wa malisho na matumizi ya teknolojia rahisi za kukata, kufunga na kuhifadhi majani na masalia ya mazao ili yatumike wakati wa uhaba wa malisho. Alisema wakifanya hivyo ana imani itasaidia wafugaji kujenga utamaduni wa kusindika masalia ya nafaka na kuchakata kwa ajili ya kulisha mifugo yao.

Aliipongeza Wizara ya Mifugo kwa kutoa mafunzo kwa maofisa ugani mara kwa mara ambayo yanasaidia kuwakumbusha majukumu yao ya kazi.

Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo ya Ugani, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angello Mwillawa, alisema uzalishaji wa malisho bora ni nyenzo muhimu katika kukabiliana na mahitaji makubwa ya lishe bora na uhakika kwa mifugo sambamba na ongezeko la mahitaji makubwa ya nyama na maziwa nchini.

Alisema wizara imekuwa ikitekeleza moja ya mikakati yake wa upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo kwa kuielekeza jamii jinsi ya kutunza maeneo ya malisho bora kwa mifugo. Alibainisha wizara kwa kushirikiana na halmashauri nchini zimeanzisha mashamba ya mfano ya malisho bora ambayo yanalenga kuwajengea uwezo wafugaji wote nchini kuzalisha malisho bora katika maeneo yao.

# Wenye ulemavu waaswa mikopo

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

NAIBU Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu wenye Ulemavu), Stella Ikupa, amewaasa watu wenye ulemavu kuheshimu fedha za mikopo wanazokopeshwa ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuachana na kuwa ombaomba.

Ikupa alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizindua mafunzo ya wajasiriamali kwa makundi maalum ya watu wenye ulemavu yaliyofanyika wilayani humo.

Alisema mikopo hiyo inalenga kuwaondoa kwenye umaskini, hivyo itumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

"Fedha za mikopo siyo za ruzuku, bali zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwamo kukuza mitaji ya biashara zao, na urejeshwaji kwa wakati, ili watu wengine waweze kukopeshwa mikopo hiyo," alisema.

Hata hivyo aliwataka watu wenye ulemavu kuachana na tabia ya kukaa barabarani na mitaani, kwa kutegemea kuomba omba badala yake watumie nafasi hiyo kubuni miradi ambayo itawasaidia kujiongezea kipato.

"Naomba muunde vikundi na muwe wabunifu ili muweze kupatiwa mikopo itakayowawezesha kujiajiri na kuwaajiri wengine, pia mbali na hilo ninawaomba mjikite kwenye kilimo cha kisasa ambacho kitawaondoa kwenye changamoto wanazokabiliana nazo badala ya kukaa barabarani na mitaani, " alisema.

Mkurugenzi wa Taasisi isiyo ya kiserikali ya Nakua na Taifa Langu ambaye ni Mratibu wa mafunzo hayo, alisema mafunzo hayo yanafanyika kwa malengo ya kuwawezesha kufanya shughuli mbalimbali zinazoweza kuwapatia kipato bila kujali aina ya ulemavu walionao.

Mshama alisema kuwa katika jamii walemavu wengi wamekataa tamaa na kuona kuwa mlemavu hawezi kufanya shughuli yoyote jambo ambalo si kweli.

"Mimi kama mjasiriamali Mtanzania malkia wa nguvu ninayependa kujishughulisha na ujasiriamali nimeamua kuwapatia mafunzo haya bure, ili kuwafanya watu wenye ulemavu kuondokana na tabia ya utegemezi kutoka kwa wasamaria wema," alisema.

Naye Yusuph Mnyabahi aliiomba serikali kuwatafutia masoko ya bidhaa wanazozalisha ili wasiweze kukataa tamaa ya kutojihusisha na utengenezaji wa bidhaa.

# Serikali kutilia mkazo afya ya wananchi

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema itaendelea kutilia mkazo suala la afya za wananchi kwa kuwapatia dawa bora na sahihi ili kuimarisha hali zao za afya.

Hayo aliyasema Naibu Waziri wa wizara hiyo, Harusi Said Suleiman, kwenye maadhimisho ya Siku ya Wafamasia Duniani yaliyofanyika mjini Zanzibar.

Alisema kuwa wafamasia wanajukumu kubwa la kuhakikisha wanatumia taaluma yao, ili kuwasaidia wagonjwa na kuonekana afya zao zinaimarika.

Aliwataka kutumia kauli nzuri na kuwaelekeza wagonjwa matumizi sahihi ya dawa ili kulinda afya zao na kuepusha matatizo yasioyo ya lazima. "Ni jukumu lenu wafamasia kulinda afya za wagonjwa na muwe na kauli nzuri kwao mnapowaelekeza kuhusu matumizi ya dawa ili kuepuka athari," alisema Naibu Waziri huyo. Aliwataka wafamasia kutoa mafunzo kwa jamii iliyowazunguka kuhusu matumizi sahihi ya dawa ili kuacha tabia ya kutumia dawa bila kupata maelekezo kutoka kwa daktari.

Naye Kaimu Mfamasia Mkuu wa Wizara ya Afya, Zaharani Ali Hamadi, alisema watahakikisha wanatimiza lengo lililokusudiwa la kuwapa maelekezo mazuri wagonjwa wanapopatiwa dawa.

Alisema taifa kuwa na afya bora linahitaji maelekezo na miongozo mizuri hivyo watatumia taaluma yao kuhakikisha wanawasaidia wananchi.

Mkurugenzi Mkuu Idara ya Utafiti wa Dawa Wizara ya Afya, Mayasa Salum, alisema mtu anapoumwa lazima amuone daktari na kuacha kutumia dawa bila maelekezo.

Aliwashauri wananchi wanapopata matatizo ya kuumwa kuacha kutumia dawa zilizobakishwa na mgonjwa mwingine kwa kuwa kufanya hivyo ni kuhatarisha afya zao.

"Ninawaomba kuacha kutumia dawa za mgonjwa mwingine ama zilizokaa kwa muda mrefu kwa kuwa kufanya hivyo ni kuhatarisha afya zenu," alisema.



Wateja katika Soko la Tandale wilayani Masasi mkoani Mtwara, wakiangalia matikitiki maji jana. Wakazi wa wilaya hiyo wamehamasika kula matunda baada ya kupatiwa elimu na wataalamu wa masuala ya afya.
**PICHA: HAMISI NASIRI**

# Wanawake watakiwa kuanzisha miradi maendeleo

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahamuod, amewataka wanawake wa mkoa huo kuanzisha miradi ya kimaendeleo itakayowawezesha kujitegemea kiuchumi.

Aliyasema hayo katika ufunguzi wa mkutano wa Baraza la Wanawake wa Umoja wa Wanawake wa CCM (UWT) Mkoa wa Kusini.

Alisema wanawake wakiamua kuanzisha miradi ya kimaendeleo itawasaidia katika maisha na kuepukana na umaskini na utegemezi.

Ayoub alisema kwa sasa ameanza rasmi kufuatilia changamoto zote zilizopo katika mkoa huo hasa kwa upande wa wanawake na vijana.

Aliwashauri wanawake hao kuhamasisha wenzao kujiandikisha katika daftari la kupiga kura ili wakipe kasi na ushindi Chama Cha Mapinduzi.

Ayoub ambaye ameteuliwa hivi karibuni kuwa mkuu wa mkoa huo baada ya kuondolewa Mkuu wa Mkoa wa Mjini, aliishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendeleza maendeleo na kuwataka wananchi kushirikiana katika kudumisha maendeleo mbalimbali yaliyomo ndani ya mkoa huo.

Akisoma risala kwa niaba ya umoja huo, Mjumbe wa Baraza Kuu la UWT, Amina Daud Hassan, alisema wilaya hiyo inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo uharibifu wa mazao ya wakulima hali ambayo imekuwa ni changamoto katika kuendeleza shughuli za kilimo.

Alieleza kuwa wanawake wa mkoa huo shughuli yao kuu ni kilimo, lakini kimekuwa kikihujumiwa na mifugo pamoja na wizi wa mazao yao.

# Cuba yaombwa nafasi za masomo sekta kilimo

**Na Rahma Suleiman**, ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amefanya mazungumzo na ujumbe kutoka Jamhuri ya watu wa Cuba kwa lengo la kuimarisha sekta ya elimu nchini.

Katika mazungumzo hayo, aliuomba ujumbe huo kuisaidia Zanzibar kupata nafasi za masomo hasa katika sekta ya kilimo ambayo tayari nafasi kama hizo zimetolewa katika sekta ya afya.

Alisema watakaa na wataalamu wa fani mbalimbali na kuorodhesha fani ambazo zinahitajika ili kupatiwa nafasi hizo za masomo ndani ya nchi hiyo.

Aliutaka ujumbe kujifunza Kiswahili kwa kuwa ni miongoni mwa lugha zinazotambulika kimataifa.

"Mje Zanzibar kuja kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwa kuna walimu wazuri wa lugha ya Kiswahili, hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ndio kitovu cha lugha hiyo fasaha," alisema.

Naye Mkuu wa masuala ya Uhusiano wa Kimataifa kutoka Wizara ya Kilimo inayoshughulikia masuala ya Kimataifa ya Jamhuri ya Watu wa Cuba, Antonio Buides Lazanas, alisema wapo tayari kuisaidia Zanzibar katika sekta ya elimu kutokana na ushirikiano mzuri ulipo kati ya Zanzibar na Cuba.

Antonio aliitaka Wizara ya Elimu kuorodhesha fani zote wanazohitaji na baadaye kuziwasilisha katika Ubalozi wa Jamhuri ya Watu wa Cuba na kufanyiwa utaratibu wa kupatiwa nafasi hizo kwa wanafunzi wa Zanzibar.

Aliipongeza Zanzibar kwa kukuza ushirikiano na Cuba na kuendeleza amani na utulivu nchini.

# Biteko asisitiza zebaki kutotumika migodini

**Na Mwandishi Wetu**

MATUMIZI ya zebaki katika uchimbaji wa madini umeelezwa kuwa hatarishi kwa afya ya binadamu hasa kwa watumiaji ambao ni wachimbaji wadogo wa madini pamoja na mazingira yanayozunguka eneo husika.

Akizungumza wakati wa kufunga maadhimisho ya siku tatu ya Miaka 50 ya Taaluma ya Jiolojia mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, Waziri wa

Madini, Doto Biteko, alisema wizara imeingia mkataba unaozuia matumizi ya zebaki duniani kwani ni kemikali ambayo si rafiki kwa afya ya mwanadamu pamoja na mazingira yanayozunguka.

"Saidieni katika kuhakikisha umoja wenu unasaidia taifa hasa katika kutunza rasilimali zetu. Tuungane na serikali kuhakikisha madini yetu yanachimbwa kihalali, huku tukizingatia usalama wa wachimbaji, watu wanaowazunguka na mazingira kwa ujumla ili kuleta tija kwa nchi yetu," alisema.

Alisema jiolojia ni moja ya taaluma inayogusa karibia nyanja zote za

maisha na kuwaomba wanajiolojia kushirikiana na serikali katika kuhakikisha mbadala wa zebaki unasisitizwa kama njia moja wapo ya kupunguza athari ambazo zingepelekea uharibifu wa mazingira.

Waziri Biteko alisema taaluma ya jiolojia ni muhimu sana hasa katika sekta ya madini kwani sekta hiyo ni muhimu kwa ajili ya uchumi wa nchi, hivyo kuna kila sababu ya wanajiolojia kufanya kazi zao kikamilifu na kuunga mkono azma ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo 2025.

Aidha, Waziri Biteko alisema NEMC watatangaza kipindi cha mpito juu ya matumizi ya zebaki na kuwataka wadau kutoa ushirikiano stahiki.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa

Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema matumizi ya zebaki katika uchimbaji wa madini ni hatari kiafya na serikali haiwezi kuacha watu wake wakapoteza maisha kwasababu yakupata faida.

Alisema ina lengo la kuwafanya wachimbaji wadogo kukua na kuwa wachimbaji wakubwa.

"Tutatafuta njia mbadala ili wachimbaji wadogo waachane na matumizi

ya zebaki na afya zao kuimarika zaidi na kufaidika na kile wanachokivuna. Hatutaki ifike mahali tuwe na matahira wengi na watu wenye utindio wa ubongo," alisema Dk. Gwamaka.

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema kuwa kuna tatizo kubwa katika mbinu bora

za uchimbaji, hivyo kuchangia jali nyingi zaidi katika migodi na hasa utumiaji wa vitendea kazi duni katika uchimbaji.

"Kuna umuhimu wa kuwapa elimu iliyojitosheleza ya kijiolojia kwa wachimbaji wadogo wa madini. Bila hivyo tutaendelea kuwa na ajali hadi hapo tutakapopata njia ya kuwasaidia wachimbaji wadogo," alisema.



Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Sima, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Mtwara kuhusiana na jinsi Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ambalo lipo chini ya ofisi yake kwa namna linavyopambana kuweka mazingira rafiki ili kuendelea kuwavutia wawekezaji nchini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Minada isiyo na vyoo kufungwa

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

MKUU wa Wilaya ya Bunda, Lydia Bupilipili, ameagiza minada yote ya ng'ombe wilayani humo kuwa na vyoo kwani kutokuwapo kwa vyoo kunahatarisha afya za watu wanaofika maeneo hayo kwa ajili ya biashara na shughuli nyingine za kibinadamu.

Alitoa agizo hilo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, ambacho kilikuwa ni cha kupokea taarifa ya utekelezaji ya robo ya mwisho katika mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Bupilipili alisema mnada ambao hautakuwa na vyoo vinavyotumika ataufunga kwa kuwa hali hiyo inahatarisha afya za watu wanaofika katika maeneo hayo, na kwamba watu wengi wamekuwa wakijisaidia katika vichaka vilivyo karibu na minada hiyo.

"Nikikuta mnada unafanyika wakati hakuna vyoo vinavyotumika nitaufunga, maana hali hiyo inahatarisha afya za watu wanaofika katika eneo hilo," alisema Bupilipili.

Aidha, alisema halmashauri hiyo haisimamii ipasavyo miradi ya maendeleo na kuwa hali hiyo imekuwa ikisababisha kushindwa kukamilika kwa muda uliopangwa, na kwamba hiyo ni changamoto ya kurudisha maendeleo nyuma.

Aliwataka wataalamu katika halmashauri hiyo kutumia utaalamu wao vizuri, ikiwa ni pamoja na kuwasaidia madiwani ili kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazoikabili halmashauri hiyo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Isack Mahela Kabugu, alisema wameyapokea maelekezo na mapendekezo yote yaliyotolewa na serikali, na kwamba Baraza la Madiwani litahakikisha linakabiliana na changamoto hizo, hususani katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na ukusanyaji wa mapato.

Wakichangia katika kikao hicho baadhi ya madiwani walilalamikia baadhi ya barabara kuwa mbovu, ambapo sehemu za vijijini nyingine hazipitiki, na kwamba wanaopotoa kero hiyo kwa meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) hasikii kilio chao, na kusema kuwa ipo haja ya watu wa Tarura kuitwa kwenye vikao vya baraza hilo.

"Hali ya barabara hasa za vijijini ni mbaya sana, ukiangalia mfano barabara ya kutoka Busambara kwenda Iramba ni mbovu sana... magari yanapita kwa shida sana, ninaiomba Tarura itengeneze barabara hiyo," alisema Majura Erasto wa Kata ya Iramba (CCM).

## TGNP Mtandao yazindua ilani

**Na Yasmine Protace**

TGNP Mtandao imezindua ilani ambayo inaendeleza madai ya wanawake watetezi wa haki za ushiriki katika uongozi wa kisiasa tangu kupatikana uhuru mpaka sasa.

Pia ilani hiyo, inawalenga wanawake kwa vile wamechoka kuwa wasindikizaji.

Hayo yalisema na mwanachama wa Bodi ya TGNP Mtandao, Prof. Ruth Meena, wakati akizindua ilani hiyo.

Alisema ilani hiyo ni ya tatu katika maandishi na imekuwa ikiongozwa na TGNP Mtandao, katika kuleta sauti ya pamoja.

"Ilani imetokana na mchakato wa wanawake katika kudai uongozi na kauli mbiu yake ni ajenda ya mwanamke nguvu ya ushindi," alisema.

Aliongeza kuwa ilani inamlenga mwanamke kwa vile amechoka kuwa msindikizaji katika kutoa maamuzi.

Aliongeza kuwa ilani hiyo inavilenga pia vyama vya siasa kutokana na wanawake kujitokeza wengi, lakini wanaochaguliwa ni wachache.

Alisema ilani hiyo pia inavilenga vyombo vya habari kwa kuwa vina uwezo wa kuwasaidia wanawake.

Julius Mbilinyi, Mkurugenzi Idara ya Jinsia kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alisema Tamasha la Jinsia sio tamasha la wanawake pekee, bali ni tamasha la kimapinduzi kwa wanawake na wanaume.

Alisema nchi inatambua usawa wa kijinsia na jamii shirikishi ni muhimu kwa taifa kwa ajili ya kuleta uchumi wa kati.

Alisema kuwa upo mpango mkakati kwa ajili ya kushughulikia masuala ya kijinsia.

"Ukombozi na usawa wa kijinsia unaweza na utaleta mafanikio makubwa kwa taifa," alisema.

Aliongeza kuwa serikali mwaka jana iliamua suala la kuchangia asilimia 10 kwa halmashauri, asilimia nne wanawake, asilimia nne vijana na asilimia mbili wazee.

Alisema fedha hizo zinatolewa bila riba na kuitaka jamii kuchangamkia fursa hiyo ambayo itakuwa mkombozi kwake.

## 500 waokolewa kwenye mateso jengoni Nigeria

**ABUJA, Nigeria**

TAKRIBANI watu 500 wanaume na wavulana wameokolewa kutoka katika jengo moja kaskazini mwa mji wa Kaduna, ambapo walikuwa wakizuiliwa katika jumba hilo, huku wakinyanyaswa kingono na kuteswa.

Watoto wadogo wa hadi miaka mitano ni miongoni mwa wale waliokuwa wamekutwa katika jumba hilo.

Ofisa wa Polisi wa Kaduna, Ali Janga, aliiambia BBC kwamba jumba hilo lilivamiwa kufuatia habari kutoka kwa watu wasiojulikana kufuatia vitendo vilivyotiliwa mashaka katika jumba hilo.

Mmoja wa mateka katika jumba hilo, Issa Ibrahim (29), anasema alipelekwa katika jumba hilo wiki tatu zilizopita na familia yake, katika kilichotarajiwa kuwa ni kuirekebisha tabia yake na kudai kuwa alijaribu kutoroka siku moja kabla ya uvamizi wa polisi.

Aliwaeleza polisi kwamba alifungwa kwenye jenereta la zamani na kukabiliwa na adhabu za kikatili, inayofahamika kama "Tarkila", ambapo mikono yake ilifungwa juu na kichwa kuning'inia kutoka kwenye paa.

"Nina majeraha karibu sehemu nzima ya mwili wangu na hata ukilala wanatumia fimbo kukuamsha," alisema.

**BBC**

## Trump aonya wafuasi wake

**NEWYORK, Marekani**

RAIS wa Marekani, Donald Trump, ambaye anaandamwa na mchakato wa bunge wa kutaka ang'olewe madarakani kufuatia tuhuma za matumizi mabaya ya ofisi, amewaonya wafuasi wake kwamba nchi hiyo ipo pabaya zaidi kuliko wakati wowote ule uliopita.

Ujumbe huo kwa njia ya video aliouchapisha katika ukurasa wake wa Twitter ni jibu kwa wabunge wa chama cha Democratic wanaotaka uchunguzi dhidi ya madai kuwa Rais Trump alijaribu kumshawishi au kumshinikiza rais wa Ukraine kutoa maelezo ya kumpaka tope Joe Biden ambaye anatafuta nafasi ya kuwania urais na kuwa mshindani mkuu wa Trump katika uchaguzi mkuu ujao.

Trump amesema kwamba haki za Marekani zinatishiwa na Wademocrats. Mapema wiki hii, Spika wa Bunge Nancy Pelosi alitangaza kuunga mkono uchunguzi baada ya ufichuzi kuwa Trump alitafuta msaada wa kisiasa kutoka kwa Rais wa Ukraine kumsaidia kuchaguliwa tena mwaka ujao.

**DW.**

# Waasi Yemen wadai kukamata wanajeshi wengi wa Saudia

**SANAA, Yeman**

WAASI wa Houthi nchini Yemen wanasema wamewakamata sehemu kubwa ya wanajeshi wa Saudi Arabia baada ya shambulio kubwa karibu na mpaka kati ya mataifa hayo mawili.

Msemaji mmoja wa Houthi ameileza kwamba vitengo vitatu vya Jeshi la Saudia vilijisalimisha karibu na mpaka na mji wa Saudia wa Najran.

Amesema maelfu ya wanajeshi walikamatwa na wengine wengi kujeruhiwa. Maofisa nchini Saudia hawajathibitisha taarifa hizo.

Operesheni hiyo ilikuwa kubwa ya aina yake tangu kuzuka mzozo, msemaji huyo alieleza.

Kanali Yahiya Sarea, amesema vikosi vya Saudi Arabia vilikabiliwa na hasara kubwa kwa 'kupoteza maisha na mashine pia'.

Wote waliokamatwa walitarajia kuonyeshwa hadharani katika televisheni ya kundi hilo la waasi Al Masirah TV, aliongeza.

Waasi wa Houthi wanasema walishambulia vituo vya mafuta vya Saudia kwa makombora na ndege zisizokuwa na rubani mnamo Soetmba 14 hatua iliyoathiri masoko ya kimataifa.

Lakini Saudia inasema na kuungwa mkono na Marekani, Uingereza Ufaransa na Ujerumani ambazo zote zimeituhumu Iran kuhusika na mashambulio hayo, tuhuma ambazo Tehran inakana.

Yemen imekuwa katika vita tangu 2015, wakati Rais Abdrabbuh Mansour Hadi na baraza lake la mawaziri lilipolazimishwa na waasi wa Houthi kutoroka mji mkuu Sanaa ambao wanadhibiti sehemu kubwa za eneo la kaskazini mwa nchi hiyo.

Saudi Arabia inamuunga mkono Rais Hadi, na imeongoza muungano wa mataifa ya kieneo katika mashambulio dhidi ya waasi hao wanaungwa mkono na Iran.

Muungano huo hufyatua makombora karibu kila siku, wakati waasi wa Houthi hurusha makombora dhidi ya Saudia.

Vita hivyo vya kiraia vimesababisha janga baya duniani la kibinadamu, huku asilimia 80 ya idadi ya watu ambayo ni zaidi ya watu milioni 24 wakihitaji usaidizi wa kibinadamu au ulinzi, wakiwamo watu milioni 10 wanaotegemea chakula cha misaada ili kuendelea kuishi.

Zaidi ya watu 70,000 wanaaminika kufariki tangu 2016 kutokana na mzozo huo, Umoja wa Mataifa unakadiria. ***BBC***



Waasi wa Houthi nchini Yemen, wanaodaiwa kudhibiti sehemu kubwa ya kaskazini mwa nchi hiyo. **PICHA: BBC**

# Bukavu waandamana kupinga makanisa

**BUKAVU, DRC**

MAMIA ya wakazi wa mji wa Bukavu katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wameandamana na kuzingira makanisa ya Kikatoliki kupinga hatua ya shule za kanisa hilo kuomba ada za shule kwa wazazi na kushinikiza walimu wasitishe mgomo.

Waandamanaji wenye hasira wameyavamia majengo ya Parokia za Kikatoliki na makanisa ya Kiprotestanti kuwataka makasisi kutoa wito kwa walimu wa shule kurudi madarasani ili kuwafundisha watoto ambao wamesalia nje bila kusoma kutokana na mgomo wa walimu wanaodai malipo yao kutoka kwa serikali.

Katika Kanisa Kuu la Kikatoliki mjini Bukavu maarufu kama Notre Dame, wazazi hao walichoma matairi mlangoni mwa kanisa, hali kama hiyo ilishuhudiwa pia kwenye Parokia ya Cimpunda wilayani Nguba na sehemu nyingine za mji wa Bukavu.

Waandamanaji walibeba mabango yaliokuwa na ujumbe wa kuwataka walimu warudi shuleni ingawa hata hivyo kuna sehemu ya ambao hawakufurahishwa kwa mgomo huo akiwamo Bisafi Bitondo anayesema amekerwa na hatua hiyo akieleza kwamba 'haifai kuharibu ibada ya Mungu'.

Hali ilitulia kidogo wakati maofisa wa polisi walipofika katika sehemu hizo na kuutawanya umati wa waandamanaji wa kutumia gesi ya kutoa machozi.

Walimu nchini humo wanataka utekelezaji wa mkataba wa Bibwa, ambao unaeleza kuwa mwalimu wa elimu ya wastani anastahili kupata mshahara wa dola za Marekani 300 kwa mwezi. Mkataba wa Bibwa, ni mkataba kati ya serikali na muungano wa walimu nchini DRC unaozungumzia mishahara wanayostahili kulipwa walimu nchini kulingana na kiwango cha elimu walio nayo.

Serikali ya DRC iliidhinisha elimu ya bure katika shule za msingi za umma kwa lengo la kutekeleza yaliyomo katika Katiba ya mwaka 2005, ambao inasisitiza elimu ya bure kwa watoto wa shule za msingi.

Tangu mwaka 1993, wazazi wamekuwa wakilipa walimu ada ya mafunzo na hivi sasa serikali imeamua kuwalipa mishahara.

Lakini baadhi ya walimu mpaka sasa wana shaka kuhusu utekelezaji wa hatua hiyo mpya ya serikali. Walimu walitishia kuanza mgomo ikifika tarehe 20 Septemba ikiwa serikali haitawalipa mshahara wa kutosha.

"Amechukua (Felix Tshisekedi) hatua hiyo ya kusema wazazi wasilete tena pesa na sisi tulimuunga mkono, hapa kwani nina walimu ambao hawajawahi kupokea pesa kutoka kwa serkali, nadhani ni muhimu kulipa walimu, kama walimu hawatalipwa haraka, itakuwa athari sana," Mwalimu Moju alisema.

Gharama ya elimu ya bure kwa watoto wa shule ya msingi ni kama 40% ya bajeti ya nchi ambayo ni ya dola za Marekani karibu bilioni sita. ***BBC***

# Waziri, Diamond Platnumz wapanda Mlima Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

KAMPENI maalum ya 'Kili Challenge 2019, Twenzetu Kileleni' iliyoasisiwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, ili kuhamasisha Watanzania kuupigia kura Mlima Kilimanjaro ushinde na kutangazwa kuwa kivutio bora cha utalii duniani, imezinduliwa rasmi.

Dk. Kigwangalla atakuwa waziri wa kwanza tangu nchi ilipopata uhuru wake mwaka 1961, kupanda Mlima Kilimanjaro hadi kufika Kilele cha Uhuru chenye urefu wa mita 5,895 (futi 19,340).

Akizungumza wakati anazindua kampeni hiyo jana, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira alisema: "Mheshimiwa Waziri Kigwangalah, naomba niseme dhamira yako ya kupanda Mlima Kilimanjaro hadi kileleni, inaenda kuandika historia ya pekee katika nchi yetu.

"Hakuna Waziri wa Maliasili na Utalii aliyewahi kupanda mlima na kufika kileleni. Ninakuombea ufike kileleni na urudi na ushuhuda huo pamoja na wenzako wote mnaopanda."

Mlima Kilimanjaro unawania tuzo hiyo na vivutio vingine duniani ambavyo vimetangazwa katika tuzo za Taasisi ya Kimataifa ya World Travel 2019. Mlima huo uliopo nchini, tayari umeorodheshwa kama moja wapo ya vivutio bora na adimu Afrika na duniani.

Kwa mujibu wa Dk. Mghwira, lengo la kampeni hiyo ni kuhamasisha utalii wa ndani na kuchangisha fedha kwa ajili ya kuunga mkono jitihada za serikali za kupambana na Virusi vya Ukimwi.

Alisema kampeni hiyo pia imelenga kuhamasisha Watanzania na wadau mbalimbali duniani kuupigia kura Mlima Kilimanjaro ili utangazwe kuwa kivutio bora cha utalii duniani.

Mwishoni mwa wiki, Waziri Kigwangalla na watu wengine 130, walianza rasmi safari ya siku sita ya kwenda kilele cha Uhuru. Katika kundi hilo wamo wanasiasa, viongozi wa serikali, wasanii maarufu nchini na waandishi wa habari.

Dk. Mghwira alimtaka Waziri Kigwangalla atakapomaliza kampeni hiyo, kutoa msimamo wa serikali iwapo bado wazo la serikali lipo hai la kutaka kuanzisha utalii wa siku, kwa kutumia magari maalum ya umeme maarufu kiberenge.

"Ninaamini pia kwamba baada ya tukio hili la kupanda na kufika kileleni, (waziri) utatusaidia kuhitimisha na kuongoza mjadala wa matumizi ya kiberenge katika Mlima Kilimanjaro, kama unakuja ama hauji ama unafaa au haufai," Dk. Mghwira alisema.

Njia iliyokuwa inapendekezwa kutumika kwa kiberenge cha utalii ni ile ya Machame ambayo kwa mujibu wa watoa huduma, ndiyo njia inayotumika na wageni zaidi kuliko njia nyingine zote kuelekea mlimani.

Baada ya kuzindua kampeni hiyo, Mkuu wa Mkoa huyo alimshukuru Kamishna Mkuu wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Dk. Allan Kijazi, kwa uongozi mzuri uliolifanya taifa kushuhudia hivi karibuni shirika hilo likiongezewa hifadhi nyingine tatu zaidi.

Waziri Kigwangala alisema Mlima Kilimanjaro umepata tuzo sita kwa kipindi cha miaka 10 na kuufanya mlima huo kujulikana zaidi duniani.

Msanii maarufu wa muziki wa Bongo Fleva, Nassib Abdul 'Diamond Platnumz', naye alieleza dhamira yake ya kuweka rekodi ya msanii wa Tanzania kuwahi kuupanda na kufika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro.

Akizungumzia kampeni hiyo, Mwana FA alisema pamoja na nchi kujaliwa vitu vizuri ambavyo havilipiwi kwa Mungu, wasanii bado hawajafanya kazi yao ipasavyo.

Mwigizaji maarufu nchini, Jacob Steven 'JB', pia alieleza furaha yake, akisema watu wamekuwa wakimtisha kwa mwili wake kuwa hatafika kileleni, lakini safari hii atawaonyesha maajabu na kuwa msaada kwa wengine.

Baada ya kampeni hiyo kuzinduliwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Kemirembe Lwota, alisema kamati yake itaendelea kusimama kidete kuona vivutio vyote vya utalii nchini vinaendelea kulindwa kwa manufaa ya taifa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), akisaliamiana na Meneja wa Benki ya NBC Kanda ya Ziwa, Japhet Mazumira, wakati wa maonyesho ya Wiki ya Madini na Teknolojia yaliyofanyika mkoani Geita katika viwanja vya CCM Kalangalala hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# DC ahimiza tahadhari tabianchi

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, amezitaka shule za msingi na sekondari mkoani Dodoma, kuunda klabu zitakazosaidia kuhamasisha utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Ndejembi aliyasema hayo jijini Dodoma juzi, alipokuwa akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, katika kilele cha kampeni ya 'Linda Uhai'.

Alisema kuwa mabadiliko ya tabianchi ni janga la kidunia na linaathiri kwa kasi kubwa hivyo, klabu hizo zitasaidia kupinga uharibifu wa mazingira unaofanyika hivi sasa ikiwamo ukataji wa miti ovyo.

"Klabu shuleni ni muhimu ziundwe na zifanye kazi vyema hasa katika masuala ya kampeni ya mabadiliko ya tabianchi," alisema Ndejembi.

Alibainisha kuwa ana imani kuwa klabu zitasaidia kuwapata wanafunzi bora watakaokuwa mabingwa wa kutunza mazingira katika maeneo yao.

Akisoma risala Batlet William, kutoka Shule ya Sekondari ya Kiwanja cha Ndege Dodoma, alisema athari za mabadiliko ya tabianchi zinaonekana kwa uwazi nchini na katika sekta mbalimbali kama kilimo, maji, afya, nishati, misitu, utalii, makazi na miundombinu.

Aliongeza kuwa takwimu zinaonyesha jotoridi limeongezeka kwa wastani wa nyuzi joto 1.0 tangu mwaka 1960 (sawa na wastani wa asilimia 0.23) kwa muongo.

"Kiwango cha mvua kimeendelea kupungua kwa wastani wa asilimia 3.3 kwa muongo na zaidi ya mvua zimekuwa hazitabiriki na matukio ya mafuriko yamekuwa yakitokea mara kwa mara na kwa viwango visivyo vya kawaida," alisema William.

Aidha, alisema takwimu za tabianchi zinaonyesha jotoridi la Bahari ya Hindi limepungua kwa nyuzi joto moja toka mwaka 1950.

# Uboreshaji miundombinu ya umwagiliaji wainua kilimo mpunga

**Na Mwandishi Wetu, TABORA**

UBORESHAJI wa miundombnu ya umwagiliaji katika Halmashauri ya Sikonge mkoani Tabora umeongeza uzalishaji wa zao la mpunga na kuinua kipato cha wakulima wilayani humo.

Akizungumza na waandishi wa habari na maofisa toka Tume ya Taifa ya Umwagiliaji mwishoni mwa wiki, Katibu wa Chama cha Wamwagiliaji cha Skimu ya Ulyanyama wilayani Sikonge, Simon Kalosa, alisema baada ya serikali kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji wa skimu, uzalishaji wa mpunga umeongezeka tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema wastani wa uzalishaji wa mpunga kwa sasa katika skimu ya Ulyanyama ni tani nane kwa hekta, wakati kabla ya uboreshaji wa miundombinu uzalishaji ulikuwa ni magunia sita hadi nane kwa ekari.

Kutokana na ongezeko hilo, Kalosa alisema hali za maisha ya wananchi wengi zimekuwa bora na wameweza kujenga nyumba za kisasa na kusomesha watoto wao.

Skimu ya Ulyanyama ina jumla ya wakulima 306 ambao hujishughulisha na kilimo cha umwagiliaji na wengi wao wamefaidika na uwekezaji uliofanywa na serikali katika kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika skimu hiyo.

Akizungumza awali mkulima wa kilimo hicho, Happiness Mpunda, alisema kilimo cha umwagiliaji kimebadilisha maisha yake na familia kwa kuwa anajitosheleza kwa chakula na kuinua kipato cha familia.

Naye Mwenyekiti wa chama cha wamwagiliaji, Dikson Simbila, alisema ili kuongeza thamani ya mpunga wao, chama kilinunua kinu cha kukobolea na kupandisha madaraja mbalimbali ya zao katika soko.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**

**SHAURI LA MADAI YA NDOA/TALAKA NA. 46/2019**
**MDAI...............STEVEN SAMWEL**
**DHIDI YA**
**MDAIWA.....................LUCIA D/O JOSIA**

AMRI

Unaamriwa na Mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 2/10/2019 saa 2:30 asubuhi bila kukosa. Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo, na kutolewa uamuzi. Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa mahakama leo Jumanne tarehe 17 mwezi Septemba, 2019.

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

SALVAN CHACHA KABATI anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH yenye namba za usajili T.218 CTF, yenye Engine namba 3SFE5693214 na Chassis namba SR500068283, Model namba SR50.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya polisi.
KAH/TR/RB/762/2019.

115437202

---

## HATI YA KIAPO

**Mimi MICHAEL SIMBA wa S.L.P ..........,** Tanga, Mkistro, mtu mzima na mwenye akili zangu timamu, Nathibitisha katika kiapo changu hichi na kuyatamka haya yafuatayo na kama ifuatavyo:-

- Kwamba ndiye mmiliki halali kwa sasa wa Kiwanja Na. 251 Kitalu **"D"** Kilichoko katika eneo la Kange, Kata ya Masiwani Shamba, Tanga Mjini.
- Kwamba nimejaribu kuitafuta kwa juhudi zangu zote sikufanikiwa, Nimetoa taarifa Polisi na kupatiwa TAN/RB/.............2019 ya tarehe 26/09/2019.

Nakiri na kuapa kiapo hichi na kuyatamka haya yote nikiwa na akili zangu timamu na bila ya kushawishiwa na mtu yoyote yule na kukiri kwa kuweka saini yangu hapa hichi kama ifuatavyo:-

215437802

---

**Uza,**
**Chenye Thamani**
**Kubwa Kwa Kutangaza**
**Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0767 223311**

---

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223 311

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SIMEONE: REFA ANAJUA ALICHOSEMA RAMOS

**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Atletico Madrid, Diego Simeone, amedai "mwamuzi msaidizi anajua" nini Sergio Ramos alichosema wakati nahodha huyo wa Real Madrid akijikuta kwenye matatizo.

Wawili hao walionekana kubwatukiana maneno, huku Ramos akimvaa mwamuzi msaidizi kwa maneno yaliyotafsiriwa kama matusi.

Ramos aliripotiwa kumtukana mwamuzi msaidizi wakati wa mchezo wa Jumamosi kati ya Real Madrid na Atletico katika dimba la Wanda Metropolitano ambao ulimalizika kwa sare ya bila kufungana, ambako hakuchukuliwa hatua yoyote.

Diego Costa alifungiwa mechi nane kwa kumtukana mwamuzi, Jesus Gil Manzano wakati klabu hiyo ikifungwa na Barcelona msimu uliopita.


Alipoulizwa kuhusu kauli ya Ramos, Simeone aliwaambia waandishi wa habari: "Kinachotokea uwanjani kinazungumzwa uwanjani, lakini mwamuzi msaidizi anajua nini alichosema."

Hakuna kati ya Atletico au Madrid walioweza kuzifumania nyavu na hivyo kujikuta wakigawana pointi moja moja.

Matokeo hayo yameiacha Madrid ikiongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania kwa tofauti ya pointi moja dhidi ya majirani zao Atletico.

"Katika kipindi cha kwanza tulitawala mchezo na tulishindwa kufunga," alisema Simeone.

# GUARDIOLA: IPO KAZI KUIFUKUZA LIVERPOOL



**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amebainisha ugumu wa kupoteza mechi nyingi zaidi ya Liverpool wakati Manchester City ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Everton.

Mabingwa hao watetezi waliingia kwenye mchezo huo wa Jumamosi pale katika Uwanja wa Goodison Park wakiwa wamepitwa pointi nane na Liverpool, ambao walimfunga Sheffield United bao 1-0.

Dominic Calvert-Lewin alisawazisha bao la Gabriel Jesus kabla ya mapumziko, lakini Riyad Mahrez alifunga la pili kwa shuti lililomshinda golikipa Jordan Pickford katika dakika ya 71 kabla ya Raheem Sterling kufunga la tatu na kuihakikishia Man City pointi tatu.

Sasa pengo limebaki la pointi tano na Guardiola anajua kwamba anatakiwa kushinda kila mchezo uliopo mbele yake.

"Tulijua kwamba Liverpool imeshinda tena na tulikuwa na pengo la pointi nane, ambazo ni nyingi," alisema mara baada ya mchezo huo.

"Hivyo, tulishinda pointi tatu na sasa tumepitwa pointi tano, huku kukiwa na mechi nyingi za kucheza.

"Tulijua kwamba tunacheza na timu gani kwa sasa wameshinda mechi saba mfululizo, ni mabingwa wa Ulaya na wanacheza soka la kuvutia.

"Hawa ni wapinzani wetu na tunajua kwamba hatutakiwi kupoteza pointi yoyote kwa sasa."

# BUFFON AVUNJA REKODI YA MALDINI

**TURIN, Italia**

GOLIKIPA wa Juventus, Gianluigi Buffon, amevunja rekodi ya kucheza mechi nyingi zaidi katika ngazi ya klabu akimpiku Paolo Maldini.

Buffon alirudi kwenye dimba la Turin baada ya msimu mmoja kule Paris Saint-Germain na kucheza mechi yake ya 903 akiwa na Juventus Jumamosi wakati wakishinda mabao 2-0 dhidi ya SPAL na kumpiku Maldini.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 41, Buffon aliifikia rekodi ya Maldini wiki iliyopita baada ya ushindi dhidi ya Hellas Verona kabla ya kukaa benchi kwenye mchezo wa Jumanne dhidi ya Brescia.

Baada ya kuipiku rekodi ya Muitaliano mwenzake Maldini, Buffon aliwaambia waandishi wa habari: "Nimeridhishwa, sikuwa na uhakika kama nitaifikia na kuivunja rekodi hii, niligundua baada ya mchezo. Niliambiwa nimeifikia rekodi ya Paolo Maldini.

"Imenifanya kuwa na furaha kubwa na najisikia fahari kwa kile nilichokifanya, nina furaha kwa sababu nimefika hapa kwa juhudi zangu mwenyewe. Ndicho ninachofikiri kwa sasa.

"Halafu, nikaongeza tena, mara zote nitawashukuru wazazi wangu na mke wangu, ambaye amekuwa akihusika kwa karibu katika mafanikio yangu."




Buffon alirudi Juve baada ya kukaa kwa msimu mmoja kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, akiwa na klabu ya PSG, awali akiwa ameitumikia Parma.

Tofauti na Maldini, ambaye alitumia muda wake wote akiwa na AC Milan, Buffon ametumia muda wake na klabu tatu.

## HABARI MICHEZO



# NEYMAR:

## MASHABIKI WA PSG WANA TABIA ZA KIKE

**PARIS, Ufaransa**

NEYMAR amezungumzia uhusiano wake na mashabiki wa Paris Saint-Germain, akisisitiza kwamba "ni kama mwanamke, wakati mwingine unabishana naye na muda mwingine unakaa kimya bila kuzungumza".

Nyota huyo wa PSG, Neymar amekuwa na wakati mzuri tangu aliporudi kwenye timu hiyo baada ya uhamisho wake wa kurudi Barcelona kushindikana, na amefunga mabao matatu katika mechi nne.

Uamuzi wa Neymar kutaka kurudi kule Barca uliwakasirisha mashabiki wa PSG ambao walimtukana na kubeba mabango wakati nyota huyo wa Brazil aliporudi kuichezea PSG dhidi ya Strasbourg, Septemba 14, mwaka huu.

Lakini Neymar hajaathirika na matusi hayo, kwani juzi Jumamosi alifunga bao pekee lililoipa ushindi PSG dhidi ya Bordeaux na alipuuzia uhusiano wake na mashabiki.

"Kama mwanamke. Kuna wakati unabishana naye na muda mwingine unakaa bila kuzungumza lolote," alisema Neymar akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"Hata hivyo, kwa mapenzi na hamasa, unarudi katika hali yako ya kawaida. Nipo hapa kuisaidia PSG na nitafanya kila kitu dimbani kwa ajili ya timu hii."

Neymar aliongeza kuiambia beIN SPORTS: "Nina furaha kubwa! Napenda kuisaidia timu, iwe kufunga au kutoa pasi ya mwisho! Nipo hapa kwa hilo, na nina kila kitu kwa hilo."

%

# Pulisic alilia nafasi kucheza Chelsea

**LONDON, England**




CHRISTIAN Pulisic amebainisha kwamba, "inamuumiza mno" kwa kukosa nafasi ya kucheza kwenye Ligi Kuu ya England chini ya kocha Frank Lampard.

Pulisic mwenye umri wa miaka 21, hakutumika licha ya kuwa kwenye benchi wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Brighton and Hove Albion juzi Jumamosi.

Pulisic alijiunga na Chelsea akitokea kwa miamba ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Borussia Dortmund kwa kitita cha pauni milioni 58.

Hata hivyo, mchezaji huyo raia wa Marekani amecheza mara moja tu katika mechi saba zilizopita, akiwa amecheza kwenye mchezo wa Kombe la EFL wakati Chelsea ikiibuka na ushindi wa mabao 7-1 dhidi ya Grimsby Town, Jumatano iliyopita.

"Ndiyo, bila shaka, inaniumiza mno, lakini nitaendelea kufanya mazoezi kwa bidii, kwa sababu nataka kucheza," alisema Pulisic akiiambia NBC Sports baada ya mchezo wa Jumamosi.

Alipoulizwa kama amepata ushauri wowote kutoka kwa kocha, Lampard, Pulisic alisema: "Si mara nyingi.

"Aliniambia niendelea kuwa na bidii kwenye mazoezi na natakiwa kujiimarisha mimi mwenyewe ili kupata nafasi kwenye kikosi cha kwanza.

"Haitakuwa kazi rahisi, lakini nitajitahidi kuhakikisha napata nafasi ya kucheza, maana inaniumiza."

# Ramos asimulia ugumu Atletico

**MADRID, Hispania**

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos, amesema haikuwa kazi rahisi kuondoka na pointi moja katika mchezo wa Ligi Kuu Hispania dhidi ya Atletico Madrid kwenye Uwanja wa Wanda Metropolitano juzi, Jumamosi.

Real na Atletico Madrid zilishindwa kufungana kwenye mchezo huo wa mahasimu wa kwanza kuchezwa msimu huu wa 2019/20 baina yao.

"Ulikuwa mchezo mgumu sana uliohusisha matumizi ya nguvu kupita kiasi. Uwanja ule ni kati ya viwanja vigumu karibu msimu mzima. Bao lingetufanya kupata alama tatu, ilishindikana lakini jambo jema ni kutofungwa.

"Tulipata nafasi kupitia kwa Karim, lakini Oblak aliokoa. Tulikuwa kwenye nafasi ya kushinda zaidi kuliko Atletico, tunatakiwa kuendelea kuonyesha kiwango kama hiki," alisema.

Kocha wa Atletico, Diego Simeone alisema anataka kuona kikosi chake kikiimarika kwenye michezo inayofuata kulingana na kiwango walichokionyesha dhidi ya mahasimu wao.

"Mchezo ulikuwa mgumu. Kila timu ilicheza kwa kuzuia, tulikuwa bora kipindi cha kwanza, lakini tulishindwa kufunga, kipindi cha pili kilikuwa chao na zilikuwa juhudi binafsi za Oblack ambaye alicheza mpira wa kichwa kutoka kwa Benzema," alisema.

HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHEZ AANZA KUTUPIA INTER MILAN NA UMEME

Nyekundu hiyo aliipata baada ya kujirusha, hivyo kuonyeshwa kadi ya pili ya njano iliyoambatana na...

**MILAN, Italia**

ALEXIS Sanchez alifunga na kutolewa nje kwenye mchezo wake wa kwanza kuichezea Inter wakati timu yake ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Sampdoria juzi, Jumamosi.

Sanchez alikuwa akiichezea kwa mara ya kwanza Inter Milan baada ya kutua hapo akitokea Manchester United ya England na katika mchezo wake huo wa kwanza aliweza kuwapo kwenye ubao wa wafungaji.

Inter huo ulikuwa ni mchezo wake wa sita kushinda katika mechi sita za Ligi Kuu ya Italia, Serie A, na kuwawezesha kuongoza msimamo kwa tofauti ya pointi mbili dhidi ya Juventus.

Mabao mawili ndani ya sekunde 128 za kipindi cha kwanza kutoka kwa Stefano Sensi na Sanchez yaliwazesha vijana hao wa Antonio Conte kupata ushindi huo.

Sanchez alilimwa kadi nyekundu ['umeme'] baada ya kuonyeshwa ya pili ya njano kwa kujirusha kipindi cha pili na Sampdoria wakapata bao kupitia Jakub Jankto, lakini Roberto Gagliardini akaongeza la tatu kwa Inter.

Baada ya dakika 20 za mwanzo, Inter ilifunga mabao mawili kwa haraka.

Kwanza, Sensi ambaye yupo kwenye kiwango cha juu alifunga kwa shuti akiwa umbali wa yadi 30 kabla ya Sanchez kufunga.

Halafu Inter walifanya shambulio jingine la hatari, wakati Sensi ambaye alipiga shuti kali lililopanguliwa na golikipa, kabla ya Sanchez kuonekana akiwa ameotea.

Bao la Antonio Candreva lilikataliwa wakati Sanchez ambaye alitoa pasi kuonekana ameotea, kabla ya Lautaro Martinez kupiga shuti lililomlenga moja kwa moja golikipa.

Inter walimaliza kipindi cha kwanza wakiwa wametawala mchezo kwa asilimia kubwa na kuonekana kama wangeibuka na ushindi wa mabao mengi.

Sanchez alionyeshwa kadi ya kwanza ya njano kwa kumfanyia faulo Albin Ekdal kabla ya kulimwa ya pili kwa kujirusha.

Shambulio kali la Samprodia lilizaa bao wakati Jankto alipoitumia vizuri pasi ya Karol Linetty kabla ya kuutumbukiza wavuni mpira na hilo lilikuwa bao lake la kwanza kuifungia klabu hiyo.

Dakika sita baadaye, Jankto alionekana kuwa na nafasi nzuri ya kufunga, lakini shuti lake liliokolewa kwa urahisi.

## KWA UFUPI

**SOUTHGATE KUMRITHI POCHETTINO**
TOTTENHAM inamtaka Kocha wa England, Gareth Southgate kubeba mikoba ya meneja Mauricio Pochettino. ***(Star Sunday)***

**BRONCKHORST AANDALIWA CITY**
MANCHESTER City imempa majukumu ya ndani kocha Mholanzi Giovanni van Bronckhorst, kama njia ya kujiandaa na maisha pasipo Pep Guardiola. ***(Sunday Mirror)***

**ZIDANE KUMPISHA MOURINHO**
KOCHA wa zamani wa Chelsea na Manchester United, Jose Mourinho anajiandaa kurudi Real Madrid, na Rais wa klabu hiyo, Florentino Perez anataka Mreno huyo kurithi mikoba ya Zinedine Zidane. ***(Sunday Times)***

**LIVER YAHOFU KLOPP KUSEPA**
LIVERPOOL inahofia kocha wao, Jurgen Klopp atakuwa majaribuni na kazi ya kuinoa Ujerumani pindi Joachim Low atakapoachana na jukumu hilo. ***(Sunday Mirror)***

**RICE KUZUIWA UNITED**
WEST Ham inajiandaa kuweka mezani pauni milioni 100 kwa kiungo wa England, Declan Rice ili kuizuia mbio za Manchester United kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Sunday Express)***

**BARCA KUMRUDIA WILLIAN**
BARCELONA inajiandaa kurejea mchakato wake wa kumsajili winga wa Chelsea, Willian, 31. Mkataba wa nyota huyo wa kimataifa wa Brazil na klabu hiyo unamalizika mwishoni mwa msimu. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

**GUARDIOLA AITOA CITY SOKONI**
KOCHA Pep Guardiola amesema Manchester City haitanunua mchezaji yeyote katika dirisha la usajili la Januari kwa sababu haina pesa. ***(Sky Sports)***

**LAMPARD AKARIBIA KWA GELHARDT**
KOCHA wa Chelsea, Frank Lampard anaongoza vita ya kuinasa saini ya mshambuliaji wa Wigan, Joe Gelhardt, 17. ***(Sunday Express)***

**NERES ATAKIWA LIVERPOOL**
LIVERPOOL inataka kumsajili mshambuliaji wa Brazil, David Neres kutoka Ajax. ***(Calciomercato)***

**CITY KUMSAJILI SOYUNCU**
MANCHESTER City inataka kumsajili beki wa kati wa Leicester City, Mturuki Caglar Soyuncu, 23. ***(Fotospor via Metro)***

**SPURS WAHOFU KOCHA KUONDOKA**
WACHEZAJI wa Spurs wameanza kuamini kocha wao Mauricio Pochettino haraka ataondoka klabuni hapo, na Manchester United ndiko kunakoonekana kuwa kituo chake kinachofuata. ***(Sun on Sunday)***

**LINDELOF CHUPUCHUPU BARCA**
WAKALA wa beki wa Manchester United, Victor Lindelof, 25, amesema nyota huyo wa kimataifa wa Sweden alitakiwa na Barcelona majira ya joto. ***(Sport Bladet via Manchester Evening News)***



## HABARI MICHEZO

# KAMUSOKO, LWANDAMINA WAELEZA WALIPOSHIKWA YANGA

**Na Somoe Ng'itu**

KIUNGO wa Zesco FC ya Zambia, Thabani Kamusoko na Kocha Mkuu wa klabu hiyo, George Lwandamina, wamesema kikosi cha Yanga kimeimarika na kimekuwa imara tofauti na walivyokutana katika mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika ambao ulimalizika kwa sare ya bao 1-1, lakini wakieleza walipowashikia wawakilishi hao wa Tanzania kimataifa.

Hata hivyo, Zesco wamesonga mbele katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), baada ya juzi waliporudiana kwenye Uwanja wa Levy Mwanawasa mjini Ndola kupata ushindi wa mabao 2-1.

Akizungumza na Nipashe juzi, Kamusoko, alisema Yanga walijaribu kupambana na kufanikiwa kuwadhibiti katika eneo la katikati, lakini mbinu yao ya kushambulia kupitia pembeni iliwasaidia kusawazisha na baadaye kupata bao la kuongoza katika mchezo huo.

Kamusoko alisema Yanga ilikuwa na mipango imara na kama si kutumia uzoefu waliokuwa nao, mchezo huo ungekuwa mgumu zaidi kwa upande wao.

"Yanga walikuja na mipango, walikuwa imara zaidi na wamebadilika tofauti na tulivyokutana nao katika mchezo wa kwanza, walifanikiwa kutudhibiti katikati, tukalazimika kufanya mashabulizi kupitia pembeni na tunashukuru tulipata bao la kuongoza," Kamusoko alisema.

Naye Kocha wa Zesco FC, Lwandamina, alisema kikosi cha Yanga kimeimarika na kimewasumbua tofauti na walivyotarajia.

"Wameimarika, leo ( juzi), wamecheza vizuri zaidi kuliko walivyokuwa katika mechi ya mkondo wa kwanza, wakiendelea hivi, watafanya vizuri katika ligi na mashindano mengine watakayoshiriki," alisema kocha huyo wa zamani wa Yanga.

Zesco imetinga hatua ya makundi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Yanga sasa imehamia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika ambapo itacheza mechi moja ya mchujo na ikipata matokeo ya jumla nyumbani na ugenini itatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo ya pili kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

# Jang'ombe, Chipukizi sasa kukipiga J'tano

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KAMATI ya mashindano ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imeusogeza mbele mchezo wa namba 22 wa Ligi Kuu Zanzibar kati ya Jang'ombe Boys na Chipukizi kutokana na Chipukizi kushindwa kusafiri kutoka kisiwani Pemba kuja Unguja kucheza mchezo huo.

Awali ratiba ilikuwa ikionyesha mechi hiyo ilipaswa kuchezwa jana, Jumapili katika Uwanja wa Amaan, lakini timu ya Chipukizi ilishindwa kufika Unguja kutokana na changamoto ya usafiri ikiwamo kuchelewa kupata tiketi ya meli kwa wakati.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana kupitia kwa Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussen Ahmada Vuai, ilieleza kuwa mchezo huo sasa utachezwa keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Amaan majira ya saa kumi alasiri huku timu ya Chipukizi ikitarajiwa kuwasili Unguja kesho.

**"Kama tunavyojua usafiri wa Pemba haupo kila siku na kwa siku inaenda meli moja tu na inarudi siku ya pili, na meli huwa zinajaa hivyo kamati ilichelewa kukata tiketi mapema kwa ajili ya kuisafirisha timu, kwa hiyo Chipukizi itakuja Unguja Jumanne na watacheza Jumatano," alisema Vuai.**

Aidha, kamati hiyo ya mashindano pia imeusogeza mbele na kubadili uwanja wa mchezo wa Taifa Jang'ombe dhidi ya Miembeni wa Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja ambao kwa mujibu wa ratiba ya ligi hiyo ulitakiwa kuchezwa leo, Jumatatu katika Uwanja wa Mao na badala yake utachezwa Alhamisi katika Uwanja wa Amaani.

Akizungumzia sababu ya kubadilishwa kwa uwanja kwa mchezo huo, Vuai alisema ni kutokana na sababu za kiusalama zaidi.

# Simba kuanza kujifua uwanja wake wa Bunju

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wanatarajia kuanza kutumia uwanja wake wa Bunju kwa ajili ya kufanya mazoezi ili kujiandaa na mechi za ligi hiyo na mashindano mengine mbalimbali watakayoshiriki kuanzia Oktoba mwishoni, imeelezwa.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, mwekezaji wa klabu hiyo, Mohammed "Mo" Dewji, alisema mchakato wa ujenzi wa uwanja wa nyasi bandia na nyasi halisi unaendelea vizuri na utakamilika mwezi ujao na timu itaanza kuutumia muda si mrefu.

Dewji alisema kuwa ujenzi wa vyumba vya kubadilishia nguo umekamilika na kuufanya mradi huo kwenda na malengo waliyojiwelea mapema mwaka huu.

Leo (juzi), nilitembelea uwanja, maendeleo ni mazuri, uwanja wa nyasi bandia na nyasi halisi uko katika hatua za mwisho, utakamilika Oktoba mwishoni, na mara tu ukikamilika, timu yetu (Simba) itaanza kufanya mazoezi hapa," alisema Dewji.

Baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya uwanja huo, mwekezaji huyo ataendelea na mchakato wa kutengeneza majukwaa kwa ajili ya mashabiki watakaofika kuwaona mabingwa hao.

Hivi karibuni, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe, aliweka jiwe la msingi kwenye uwanja huo.



Mwanafunzi wa Shule ya Awali ya Fountain Gate Academy tawi la Mwema Tabata Segerea jijini Dar es Salaam, Britney Fredrick akiwaonyesha wenzake namna ya kucheza mchezo wa mpira wa kikapu ['basketball'] katika Siku ya Tamasha la Michezo lililofanyika shuleni hapo mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# MATOLA ALILIA BAHATI KIPIGO RUVU SHOOTING

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kushuhudia kikosi chake kikikubali kipigo cha bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ruvu Shooting, Kocha Mkuu Polisi Tanzania, Selemani Matola, amekubali matokeo hayo lakini akilia na bahati kutokuwa upande wao.

Katika mechi hiyo, iliyopigwa Uwanja wa Meja Isamuhyo, Mbweni nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam, bao pekee la Ruvu Shooting lilizamishwa nyavuni na Yassin Salum katika dakika ya tano.

Hata hivyo, Matola aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wake walipambana vilivyo katika mchezo huo, lakini hadi mwisho Ruvu Shooting ndiyo waliokuwa na bahati zaidi.

Polisi Tanzania ambayo hiyo ni mechi yake ya pili msimu huu, baada ya kuanza ligi hiyo kwa kuichapa Coastal Union, juzi ilionja kipigo cha kwanza.

"Wachezaji walijituma na kwa kweli waliweza kuhimili mikikimikiki ya wapinzani, lakini mwisho wa siku tukashindwa kupata matokeo.

"Mchezo wetu ulikuwa mgumu na kwa kiasi kikubwa wachezaji wangu walijituma na kufuata maelekezo kwa hilo ninawapongeza ila kwa kukosa matokeo ni sehemu ya mchezo, ligi bado inaendelea na sisi tutajipanga zaidi kwa mechi zijazo," alisema.



Michezo

Jumatatu Septemba 30, 2019

Nipashe



Sanchez aanza kutupia Inter Milan na umeme

HABARI UK 30

PASUA...



Kiungo wa Manchester City, Kevin De Bruyne akikabiliana na upinzani kutoka kwa beki wa Everton (chini), wakati akitaka kupasua ngome ya timu hiyo kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Goodison Park juzi na City kushinda 3-1. **HABARI UK. 28**

# SIMBA INAJIPIGIA TU

## Kagere, Miraji washika usukani wa kuchana nyavu, shuti la Ndemla nusura lizue jambo kwa....

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuvuna pointi tatu dhidi ya Kagera Sugar Alhamisi iliyopita, mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba jana, waliendeleza vipigo katika ligi hiyo baada kuipiga Biashara United kwa mabao 2-0 katika mechi kali iliyochezwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

Mshambuliaji Meddie Kagere ndiye aliyekuwa wa kwanza kuiandikia Simba bao la kwanza katika dakika ya 22 kabla ya Miraji Athumani kutupia la pili kipindi cha pili dakika ya 74.

Kagere ambaye katika mechi dhidi ya Kagera Sugar alifumania nyavu mara mbili wakati wakishinda 3-0, jana alifunga bao hilo akiitendea haki krosi ya Miraji kutoka wingi wa kulia ambaye jana alianza kwa mara ya kwanza msimu huu, baada ya mechi zilizopita Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mbelgiji Patrick Aussems kuwa na utamaduni wa kumchezesha akitokea benchi.

Miraji kwa upande wake alifunga bao la pili kwa kichwa akiunganisha nyavuni mpira wa faulo iliyopigwa na Ibrahimu Ajibu.

Kwa matokeo hayo, Simba imeendelea kukaa kileleni ikiwa na pointi 12 baada ya kushinda mechi zake zote nne ilizocheza msimu huu na sasa inarejea Dar es Salaam, na huenda ikacheza mechi yake iliyokuwa imeahirishwa dhidi ya KMC kabla ya Kalenda ya Fifa ambayo inaanza Oktoba 7 hadi 19, mwaka huu.

Aidha, Kagere naye ameendelea kukaa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora akiwa na mabao sita, huku Miraji akifuata kwa kucheka na nyavu mara tatu.

Hata hivyo, baada ya kalenda hiyo ya Fifa, inaonyesha Simba itakutana dhidi ya Azam FC Oktoba 23 na kisha siku tatu baadaye kuifuata Singida United kabla ya Oktoba 30, mwaka huu kwenda Shinyanga kuivaa Mwadui FC.

Katika mechi ya jana, Simba ambayo ilimiliki mpira mwanzo mwisho, kama ingekuwa makini ingeweza kupata mabao mengi zaidi kwani Kagere alishindwa kuiandikia timu yake bao la pili dakika ya 29 akiwa amebaki na kipa kabla ya Hamisi Ndemla dakika ya 40 kushindwa kuwa makini kwa kumhadaa mlinda mlango wa Biashara United na badala yake akaachia shuti kali lililoishia kifuani kwa kipa ayepata maumivu na kuhitaji kupatiwa huduma ya kwanza.

Biashara United ilikuwa ya kwanza kufanya mabadiliko katika dakika ya 51 kwa kumtoa Victor Hangaya na nafasi yake kuchuliwa na Jerome Lembele kabla ya dakika ya 72 Simba kumtoa Hassan Dilunga na kumwingiza Francis Kahata, huku dakika moja baadaye Mussa Khamis akimpisha Ramadhan Chombo kwa upande wa 'Wafanyabiashara' hao wa Musoma.

Dakika ya 77 Kocha wa Simba, Aussems alifanya mabadiliko kwa Ajibu kumpisha Sharaf Shiboub na dakika sita baadaye Miraji akitoka na nafasi yake kuchukuliwa na Deo Kanda.

## Zahera afunguka njia makundi Caf

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kutolewa katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera, amesema anahitaji kuona wanafunga mabao mengi katika mchezo wa Kombe la Shirikisho ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Yanga imeondolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya juzi kufungwa mabao 2-1 na Zesco FC ya Zambia na hivyo kuiaga michuano hiyo kwa kichapo cha jumla ya mabao 3-2 na sasa imehamia katika Kombe la Shirikisho kwa mujibu wa kalenda.

Wawakilishi hao pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa baada ya Simba, Azam FC, Malindi FC na KMKM kuondolewa mapema, watawajua wapinzani wao kwenye mchezo huo wa mtoano ifikapo Oktoba 9, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Zahera, alisema watapambana kuhakikisha wanapata ushindi mnono katika mchezo wa kwanza au wa nyumbani ili kujiweka katika nafasi "salama" kwa malengo ya kutinga hatua ya makundi.

Zahera alisema mashindano yote ni magumu na wachezaji wanatakiwa kuongeza umakini katika mechi zinazokuja za michuano ya Kombe la Shirikisho kutokana na kila timu kuhitaji kucheza hatua ya makundi ya mashindano hayo.

"Malengo yetu katika mashindano ya Kombe la Shirikisho ni kufunga mabao mengi, si bao moja kama ilivyokuwa kwenye mechi zilizopita, tunahitaji kufunga mabao mawili au matatu ili kuwa salama, yatatukinga zaidi, yatatusaidia kuelekea mbele," Zahera alisema.

Kocha huyo alisema kilichotokea katika mchezo wa juzi ni kukosa bahati ya kutumia vema nafasi walizopata ingawa wenyeji walikuwa wa kwanza kupata bao la kuongoza.

"Siwezi kumlaumu Makame (Abdul-Aziz) kwa kosa la kujifunga, hii ni hali ya kawaida, huwa inawatokea hata wachezaji wakubwa duniani, kwa kifupi hatukuwa na bahati katika mashindano haya, hatujafunga mabao mengi kwenye mechi zote zilizopita, hili ndio lililochangia kushindwa kusonga mbele," alisema Zahera.

Aliongeza kuwa beki wake, Lamine Moro, hakucheza katika kiwango chake cha kila siku kutokana na kuwa majeruhi wa nyama za paja, huku akishindwa kumchezesha Juma Abdul kwa sababu hakuwa fiti kucheza mechi hiyo iliyokuwa na ushindani mkali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >